# Sauti ya Kweli Kimataifa

(The Voice of Truth International)

Toleo la 96

Mzalishaji (Producer):
**World Evangelism Team**

Nakala ya Kiswahili (Swahili copy):
**Swahili Gospel Team**

Mawasiliano:

+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 784 880 470
+255 (0) 765 098 981

Taarifa (Notice):

Kitabu hiki hakiuzwi, kinatolewa bure na kanisa la Kristo kupitia taasisi ya ***World Evangelism Team (WET).***
This book is not for sale, it is freely given by the church of Christ throuth the institution ***World Evangelism Team (WET).***

# Sauti ya Kweli Kimataifa


**WAFANYAKAZI**

| | |
|---|---|
| ***Mhariri:*** | Louis Rushmore |
| ***Mhariri Mshirika:*** | Jerry Bates |
| ***Mhariri Mstaafu***: | Byron Nichols |
| ***Mhariri Mwanzilishi***: | J.C. Choate |
| ***Mpangilio:*** | Betty Burton Choate |
| ***Meneja wa Ofisi:*** | Paula Bates |
| ***Usajili:*** | Barbara Wright |
| ***Wataalamu wa Kompyuta:*** | Bradley S. Choate |
| | Dennis Larson |

## WAANDISHI

| | |
|---|---|
| George Akpabli | Wayne Jackson |
| Felix O. Aniamalu | Ancil Jenkins |
| Rex Banks | Jeff Jenkins |
| Wayne Barrier | John Kachelman, Jr. |
| Paula Bates | Dayton Keesee |
| Roy Beasley | David R. Kenney |
| Mike Benson | Dalton Key |
| Ron Bryant | Michael L. King |
| Charles Burch | Robert C. Lupo |
| Kyle Butt | J. Randal Matheny |
| Frank Chesser | Cecil May, Jr. |
| Betty B. Choate | Wes McAdams |
| Glenn Colley | Colin McKee |
| Lance Cordle | Stan Mitchell |
| Sunny David | Kevin L. Moore |
| Hans Dederscheck | Owen D. Olbricht |
| David Deffenbaugh | David Pharr |
| Clarence DeLoach, Jr. | Neal Pollard |
| Bill Dillon | Mark Posey |
| Bobby G. Dockery | Steve Reeves |
| Hershel Dyer | Andy Robison |
| Earl Edwards | Martha Rushmore |
| Demar Elam | Rebecca Rushmore |
| Raymond Elliott | David A. Sargent |
| Reuben Emperado | Darrell Surrette |
| David Everson | David Tarbet |
| Royce Frederick | J.J. Turner |
| Gary C. Hampton | Ken Tyler Allen |
| Jack Harriman | Webster |
| Parker Henderson | R.H. Tex Williams |
| Gordon Hogan | Nathan Wright |



# Mamlaka ya Ukimya wa Kibiblia

Louis Rushmore

**Wakati mwingine ukimya wa kibiblia unazungumza kama maelezo yoyote ya Maandiko. Kile ambacho Biblia haisemi kinamchango mkubwa katika mamlaka ya Biblia kama tu kile Biblia inachosema katika mada yoyote husika. Ni sahihi kwa sababu Biblia inaposema jambo fulani kuhusu mada ambayo husababisha ukimya wa kibiblia katika mada hiyohiyo, basi ukimya huo ni mamlaka.** Ingawa, katika maeneo ambayo Biblia haitamki chochote, katika maeneo hayo, ukimya haufanyiki kuwa mamlaka ya Biblia.

Muziki katika ibada ya Agano Jipya huonesha ukweli wa usemi huu. Maandiko kwa uwazi yanaalalisha **uimbaji** kama aina ya muziki unaotakiwa kutumika katika ibada ya Agano Jipya (Waefeso 5:19; Wakolosai 3:16). Kwa hiyo, ukimya kuhusiana na aina nyingine za muziki unaimarisha kile Mungu alichokisema. Kuimba bila kufungua midomo, kupiga miluzi, sauti nyingine, kupiga makofi, kupiga ngoma na

kutumia ala za muziki ni: (1) kinyume na kile Mungu alichosema, (2) kinyume cha ukimya wa kibiblia, (3) nyongeza katika Biblia na upingaji wa Maandiko, na (4) dhambi. Mambo hayo **yanavuka mamlaka ya Kristo** na fundisho lake (Wakolosai 3:17; 2 Yohana 9 – 11).

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alitarajia kwamba wasomaji wa waraka wake wangetambua **ukimya kama suala lenye mamlaka katika mambo ambayo tayari yamezungumzwa na Mungu**. Kulingana na maelezo ya Agano la Kale na Agano Jipya, Yesu hastahili kuwa kuhani katika dunia (Waebrania 8:4; 7:13).

Waebrania 7:14 ni hoja kutoka katika ukimya wa Maandiko kuthibitisha jambo hilohilo la ukimya wa Maandiko. ***"Maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambayo Musa hakunena neno lo lote juu yake katika mambo ya ukuhani."***

Mwandishi aliyevuviwa alitumia ushahidi wa ukimya wa Maandiko kama mamlaka ya kibiblia. Vivyo hivyo, sisi pia, tunapaswa kutambua kanuni ya kutafsiri ukimya wa kibiblia pale inapotakiwa. Hata hivyo, wahusika wa inayodaiwa kuwa ni kanuni mpya ya kutafsiri Maandiko wanapuuza wajibu wa ukimya wa kibiblia au kuudharau vikali. Hivyo, ndugu wanaokosea wanahatarisha roho zao wenyewe na kuziweka njia panda hali za kiroho za wengine wengi. Ukimya wa kibiblia na Neno la Mungu yote mawili yanahitajika kutumiwa kwa usahihi.

**Hoja ya mwandishi wa kitabu cha Waebrania kuhusu kanuni ya ukimya wa kibiblia.**

Waebrania 7:14

*"Maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambayo Musa* ***hakunena neno lo lote*** *juu yake katika mambo ya ukuhani."*

Katika ugawaji wa majukumu katika Agano la Kale kwa kila kabila, Maandiko yaliishia kusema tu kabila ipi itashika nafasi ya ukuhani (Walawi). Lakini haikutamka lolote kuhusu kabila nyingine kushika nafasi hiyo. Je, hilo lingeweza kumruhusu mtu wa kabila yoyote kushika nafasi hiyo? Ikiwa jibu ni hapana, kwa nini basi tufikiri kuwa tunaweza kutumia ala za muziki katika ibada wakati Biblia inasema tuimbe (Efe. 5:19; Kolo. 3:16)?

**Shadrack S. Msambaza**



# Uungu Wa Yesu

**Jerry Bates**

Fundisho la utatu ni moja kati ya mafundisho yanayokanganya sana na gumu kueleweka katika Maandiko. Linaonekana kujipinga. Inawezekanaje Mungu kuwa Mungu mmoja na wakati huohuo kuwa na nafsi tatu? Watu wana hoja kadhaa tofauti katika suala hili. Baadhi yao wanakana waziwazi fundisho hili. Baadhi wanalitafsiri katika namna ambayo inaeleweka; pamoja na hayo, jaribio la jinsi hiyo huishia kukana Utatu. Wengine ubinua mabega yao na kukataa kuzungumzia hilo, kwa kuwa hawawezi kuelewa hata hivyo. Tunataka maelezo ya uhakika ambayo yanatatua suala hili. Lakini, hayapo.

Wengi wanahoji kwamba kwa kuwa hatuwezi kuelewa Utatu, basi haliwezi kuwa ni jambo la kweli, na wanagoma kuamini suala hili. Hata hivyo, kwa sababu tu hatuwezi kuelewa jambo fulani haimaanishi kuwa jambo hilo si la kweli. Kwa mfano, hatuwezi kwa hakika kuelewa hisia. Mtu mmoja alisema kuhusu upendo, “Hatupaswi kufikiri kwamba tumeuelewa, kwa sababu si tatizo; ni jambo la siri na daima litakuwa hivyo.” Je, hilo linamaanisha hisia kama za upendo na chuki hazipo? Wanasayansi wanapata shida kuelezea mwanga, lakini ni hakika nuru ipo.

Jambo moja muhimu katika fundisho hili ni uhusiano wa Yesu na Mungu na Yesu kuvaa mwili. Wengi wanakana Uungu wa Yesu au kujaribu kuweka uhusiano wake chini ya Mungu (mfano, anakuwa mdogo kuliko Mungu Baba). Bila shaka, siwezi kuzungumzia kila kitu

kuhusu somo hili katika makala hii fupi, lakini hebu! tuangalie vitu vichache muhimu vya kuzingatia kuhusiana na Uungu wa Yesu.

Aya kadhaa zinaeleza kwa uwazi kwamba Yesu alikuwa na sehemu katika uumbaji kama tu Mungu Baba alivyokuwa nayo (Yohana 1:3; Wakolosai 1:16-17). Kwa kuwa ni Mungu pekee awezaye kuumba kitu chochote, Yesu ni lazima awe Mungu kama Mungu Baba alivyo.

Yesu pia habadiliki, ***"Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele" (***Waebrania 13:8). Bila shaka, mwandishi wa Waebrania alisema kuhusu Yesu, ***"Na kama mavazi utazizinga, nazo zitabadilika; Lakini wewe u yeye yule, Na miaka yako haitakoma"*** (Waebrania 1:12). Ni Mungu pekee ndiye asiyebadilika; kwa hiyo, kwa mara ya kwanza tunaona kwamba Yesu ni Mungu.

Pia tunaweza kuona katika Maandiko kwamba Yesu ni wa milele. Hakuanza kuwepo alipozaliwa; isipokuwa, alijinyenyekeza na kuvaa mwili katika kuzaliwa kwake. Yesu alikuwepo tangu mwanzo, katika uumbaji pamoja na Baba na alikuwa Mungu (Yohana 1:1). Alikuwepo na daima atakuwepo ***"Baba wa milele, Mfalme wa amani"*** (Isaya 9:6). ***"Matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele"*** (Mika 5:2). Ni Mungu pekee ndiye awezaye kuwa wa milele.

Kwa kiwango fulani, Yesu aliacha uweza wake wa uungu wakati alipokuwepo hapa duniani; hivyo, mara nyingi tunasoma akiwa mtiifu kamili kwa Baba yake. Hata hivyo, hilo halimaanishi kuwa hakuwa (au sio) Mungu. Paulo aliandika, ***"ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu;"*** (Wafilipi 2:6-7). Katika kifungu hiki Paulo alieleza kwamba Yesu alikuwa sawa na Mungu Baba kabla hajafanyika kuwa mwili na kabla hajachagua kwa hiari kuondoa fursa za uungu pindi alipofanyika mwanadamu.

Pamoja na hayo, hata alipokuwa duniani, Yesu bado alikuwa Mungu. Yesu hakuwa nabii wa kawaida. Hakuwa mjumbe mdogo kutoka kwa Mungu. Utimilifu wote wa Mungu ulikuwa ndani ya Neno

lililovaa mwili. Paulo alisema, ***"Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae;"*** (Wakolosai 1:19). Katika Wakolosai 2:9, Paulo aliongeza, ***"Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili."*** Paulo alitaka wasomaji wake waelewe kwamba utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani ya Mwana wa Mungu. Yesu alikuwa ni muungano wa Mungu na mwanadamu yeye ni Mungu. Katika kumrejelea Kristo, neno "utimilifu" (Kiyunani: *pleroma*) linamaanisha ujumla wa nguvu na wa sifa ambazo zinamilikiwa na Mungu, ambazo pia zinamilikiwa na Kristo. Kwa maneno mengine, sifa zozote zinazomfanya Mungu kuwa Mtakatifu au Mkuu zinapatikana pia kwa Yesu.

Katika Maandiko, Yesu kama Mwana amerejelewa kama Mungu katika maeneo mengi. Wayahudi wanafahamika kwa msimamo wa kihafidhina juu ya imani ya uwepo wa Mungu mmoja. Walijua kwamba kuna Mungu mmoja pekee; lakini, walielewa kuwa Yesu pia alikuwa ni Mungu. Yohana alithibitisha kwamba Yesu sasa ni ***"ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele"*** (1 Yohana 5:20). Paulo alisema kuwa Yesu sasa, ***"ndiye aliye juu ya mambo yote, Mungu, mwenye kuhimidiwa milele"*** (Warumi 9:5). Kama Wakristo, tunatakiwa, ***"tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu;"*** (Tito 2:13). Angalia Yesu amerejelewa kama Mungu na Mwokozi. Kwa Mwana ilisemwa ***"Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele;"*** (Waebrania 1:8). Yesu alipowatokea mitume wake wote baada ya kufufuka, tunamwona Tomaso akikiri ***"Bwana wangu na Mungu wangu"*** (Yohana 20:28). Neno Mungu kwa Kiyunani ni *Theos,* ni neno lilelile ambalo daima hutumika kumrejelea Mungu Baba. Zaidi sana, Yesu hakumkemea Tomaso; hivyo, hii ni sawa na madai yake mwenyewe kuwa yeye ni Mungu.

Zaidi sana, tunaona Yesu alikubali kuabudiwa akiwa hapa duniani. Agano la Kale lilikataza mtu yeyote kuabudiwa isipokuwa Mungu (Kutoka 20:1-4; Kum. 5:6-90. Wanadamu hawapaswi kuabudiwa (Matendo 10:25-26; 14:11-15). Hata malaika hawatakiwi kukubali kuabudiwa (Ufunuo 22:8-9). Yesu alikubali kuabudiwa baada

ya kufufuka (Mathayo 28:9, 17). Kwa kuwa ni Mungu pekee anayetakiwa kuabudiwa, na Yesu alikubali kuabudiwa nyakati zote mbili kabla na baada ya kufa kwake, kwa hakika, tunaweza kuhitimisha kwamba Yesu alijua kuwa yeye ni Mungu, na wengine walijua kuwa yeye ni Mungu. Pia tunaweza kuhitimisha kwamba kama ilikubalika kumwabudu Yesu wakati akiwa duniani, bila shaka inakubalika kumwabudu Kristo aliyetukuzwa. Hata hivyo, Yesu Kristo alifundisha kwamba waabuduo katika Ukristo kimsingi wanatakiwa kumwabudu Mungu Baba, kwa mfano, katika maombi (Mathayo 6:6, 8-9). Angalia pia, ***"Yesu akamwambia, Mama, unisadiki, saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala kule Yerusalemu…Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu"*** (Yohana 4:21, 23).

Baadhi ya wakosoaji wanadai kwamba Yesu kamwe hakudai kuwa ni Mungu. Ni wazi, ingawa, Yesu Kristo alidai kuwa ni Mungu, na wakosoaji wake wa Kiyahudi walifahamu vizuri madai ya Bwana wetu. ***"Akawajibu, Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi. Basi kwa sababu hiyo Wayahudi walizidi kutaka kumwua, kwa kuwa hakuivunja sabato tu, bali pamoja na hayo alimwita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu. Basi Yesu akajibu, akawaambia, Amin, amin, nawaambia,"*** (Yohana 5:17-18). ***"Yesu akawajibu, Kazi njema nyingi nimewaonyesha, zitokazo kwa Baba; kwa ajili ya kazi ipi katika hizo mnanipiga kwa mawe? Wayahudi wakamjibu, Kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa kukufuru, na kwa sababu wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u Mungu."*** (Yohana 10:32-33). ***"Wayahudi wakamjibu, Sisi tunayo sheria, na kwa sheria hiyo amestahili kufa, kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu."*** (Yohana 19:7). ***"Lakini akanyamaza, wala hakujibu neno. Kuhani Mkuu akamwuliza tena, akamwambia, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wake Mtukufu? Yesu akasema, Mimi ndiye, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni. Kuhani***

***Mkuu akararua nguo zake, akisema, Tuna haja gani tena ya mashahidi? Mmesikia kufuru yake; mwaonaje ninyi? Wote wakamhukumu kuwa imempasa kuuawa"*** (Marko 14:61-64).

Angalia maelezo haya mengine mawili kutoka katika kinywa cha Yesu. Katika Yohana 10:30, tunamwona Yesu akisema, ***"Mimi na Baba yangu tu Umoja."*** Hakuna mcha Mungu yeyote wa Kiyahudi ambaye kamwe angeweza kuweka maelezo kama hayo vinginevyo alikuwa akidai kuwa yeye ni Mungu. Pia alisema ***"Aliyeniona mimi amemwona Baba;"*** (Yohana 14:9). Ni wazi, Yesu hakuwa anazungumzia mwonekano wa kimwili kama Mungu, kwa kuwa Mungu hana mwili wa kidunia. Alikuwa anamaanisha kwamba alikuwa na sifa zote za Uungu alizonazo Mungu Baba.

Ni dhahiri, huu ni mjadala mfupi sana wa somo gumu, lakini natumaini, hakuna atakayetilia shaka Uungu wa Yesu. Yesu ni Mungu kama alivyo Mungu Baba, na hili ni moja kati ya mafundisho mazuri ya Biblia. Mungu akafanyika mwili (1 Yohana 4:2) ili kuleta upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Kamwe hatupaswi kumweka Yesu katika daraja la chini kuliko Mungu, kwa sababu kwa uwazi Biblia inafundisha vinginevyo.

## MASWALI AMBAYO WANAULIZA

1. Kama Yesu ni Mungu ni wapi anaposema kuwa "mimi ni Mungu?" **Jibu:** je! Nahitajika kusema kuwa mimi ni binadamu ili nionekane kuwa mwanadamu? Vitendo vinazungumza.
2. Yesu alipokufa kwa hiyo Mungu alikufa? **Jibu:** Kinachokufa ni mwili wala si roho. Mungu ni Roho. Yesu alikufa mwili sio Roho.
3. Yesu kama ni Mungu mbona aliona njaa na kiu? **Jibu**: Kwa sababu alivaa mwili wa kibinadamu. Malaika pia kuna wakati walikula kama wanadamu (Mwanzo 18).
4. Kama Yesu ni Mungu mbona alizaliwa? **Jibu:** Hakuzaliwa roho alizaliwa mwili. Mama zetu hawazai roho zetu wanazaa miili yetu.

**Shadrack S. Msambaza**



# Mbinguni Kutakuwaje?

J.C. Choate

**1932 - 2008**

Biblia inafundisha kwamba sisi sote tutakufa, au kuuvua mwili wa kidunia katika Ujio wa Pili wa Kristo (1 Wathesalonike 4:16-17). Pia tunaambiwa kwamba, ***"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu;"*** (Waebrania 9:27).

Mtume Paulo alisema, ***"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya"*** (2 Wakorintho 5:10).

Pengine swali muhimu katika hatua hii lingekuwa ni, "Kitu gani hutokea katikati ya kufa kwa mtu na hukumu?" Kwa maneno mengine, katika muda huo, mtu huyo anakuwa wapi? Je, bado anaishi? Je, bado anafahamu? Au je, anaendelea kubaki kaburini au katika eneo la wafu bila ya kuwa na ufahamu?

Katika Luka 16:19-31, Kristo alisimulia kisa cha tajiri na Lazaro. Alisema kwamba watu hawa wawili hatimaye wakafa. Roho ya fukara ilichukuliwa na malaika na kupelekwa kifuani mwa Ibrahimu au katika eneo la wafu wenye haki, ambalo linaelezewa kuwa ni Paradiso. Hata hivyo, roho ya tajiri ilienda katika eneo la mateso lenye mwali wa moto. Kisha akalia kwa sauti kumwambia Baba Ibrahimu amwonee huruma na amtume Lazaro achovye kidole chake kwenye maji ili aupoze ulimi wake. Ibrahimu akamkumbusha tajiri kwamba katika

maisha yake alipata vitu vyote vizuri ambavyo hupatikana katika ulimwengu wa kimwili lakini maisha ya Lazaro yalikuwa ya shida yasiyo na kitu. Alihitimisha kwa kusema kwamba sasa Lazaro alikuwa akifarijiwa wakati tajiri alipokuwa akiteswa.

Ibrahimu alieleza kwamba Lazaro hasingeweza kuja kwake kwa kuwa kuliwekwa kizuizi kikubwa baina yao na hakuna mtu ambaye angeweza kuvuka kwenda kwa mwingine. Kisha tajiri akamwomba Ibrahimu amtume Lazaro aende kwenye nyumba ya baba yake kuwaonya ndugu zake wasije wakaja katika sehemu ile ya mateso.

Ibrahimu akamjibu kuwa wanao Musa na manabii, na kama wasipowasikia wao, wasingesikiliza hata kama mtu akifufuka kutoka kwa wafu na kuwaonya. Ukweli uliowazi umefundishwa hapa ya kwamba wafu hawezi kubadilisha nafasi zao, wala hawawezi kurudi duniani kwa kuwatokea wanadamu walio hai.

## Je! Ufufuo na Hukumu Itakuwa Lini?

Bado, kuna mtu anaweza kukataa, "katika maelezo ya Yesu, tajiri alikuwa tayari katika mateso na Lazaro alikuwepo tayari Paradiso. Vipi kuhusu ufufuo (Yohana 5:28-29), ufufuo wa pamoja na hukumu kwa ajili ya wote?" hakuna tatizo hapa. Katika maisha haya, kama mwuaji akikamatwa, hutupwa mahabusu mpaka siku yake ya hukumu na muda wa kushitakiwa ili kulipa kwa makosa yake. Maandiko, kwa hivyo, yanafundisha kwamba wakati mtu mwenye haki au Mkristo mwaminifu anapokufa basi moja kwa moja ataenda Paradiso, katika sehemu ya wafu wenye haki; lakini pindi mtu mwovu anapokufa, haraka sana ataenda katika mateso, katika sehemu ya watu waovu.

Pamoja hayo, Kristo atakaporudi (1 Wathesalonike 4:16), wote watasikia sauti yake, na miili ya nyama itafufuliwa kutoka makaburini na kukutanishwa roho ambazo zilikuwa paradiso au katika mateso, ili kubadilishwa katika mwili usioharibika na kukusanyika mbele za Bwana kwa ajili ya hukumu na kuhukumiwa (Matendo 17:31; Mathayo 25:31-46). Mwishowe, Maandiko yanasema katika maneno ya Yesu kwamba waovu, ***"Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele;***

***bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele"*** (Mathayo 25:46).

## Je! Hii ni Mithali?

Wakati wengine wanasema kisa cha tajiri na Lazaro ni mfano tu, lakini hauitwi hivyo katika Maandiko. Pia katika vitabu hakuna mfano ambao wanatajwa kwa jina. Bila kujali ni mfano au sio, ukweli uliofundishwa haubadiliki. Hilo linamaanisha, kwamba wale wanaokufa wanaendelea kuwa na ufahamu wa kuwa wao ni nani, nini walichokifanya na watu waliowajua katika ulimwengu huu.

Roho zinaenda Paradiso au katika Mateso, kulingana na kama wameokoka au wamepotea. Katika Siku ya hukumu, inaonekana kwamba maisha yao yatakuwa kitabu kilichofunuliwa na hivyo wataruhusiwa kuzungumza ili kujitetea (Ufunuo 20:12; Mathayo 25:31-46). Watahukumiwa na Hakimu mwenye haki kwenda katika mateso ya milele pamoja na shetani na malaika zake au kuishi pamoja na Bwana milele katika mbingu na nchi mpya pamoja na wote waliookoka.

Kifo na hukumu vitakuwa mwisho, na hatima ya mtu itakuwa ni ya milele. Hakutakuwa na **nafasi ya pili**, wala hakutakuwa na waovu. Roho zitaishi milele, iwe ni mbinguni au sehemu ya mateso.

## Je! Maandiko Yanaielezeaje Mbingu?

***"Kwa maana viumbe vyote pia vilitiishwa chini ya ubatili; si kwa hiari yake, ila kwa sababu yake yeye atiyevitiisha katika tumaini; kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu. Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa"*** (Warumi 8:20-22).

***"Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea. Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo***

***mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka?Lakini, kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake"*** (2 Petro 3:10-13)

***"Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena"*** (Ufunuo 21:1).

Rafiki yangu, tunapaswa kujiandaa leo hii kukutana na Bwana na kuzifanya roho zetu kuwa tayari kuishi katika uumbaji ule mpya na mkamilifu. Tafadhali usiupuuze wokovu wako na kumsikia Bwana akisema ***"ondoka kwamgu"*** na kupotea kwa milele yote.

## EZEKIELI

Je! Mimi ninafurahia kufa kwake mtu mwovu? Asema Bwana MUNGU; si afadhali kwamba aghairi, na kuiacha njia yake, akaishi? Maana mimi sikufurahii kufa kwake afaye, asema Bwana MUNGU; basi ghairini, mkaishi. (18:23, 32)

Waambie, Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa, Enyi nyumba ya Israeli? (33:11)

## ZABURI

Ina thamani machoni pa Bwana Mauti ya wacha Mungu wake. (116:15)

## UFUNUO

Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao. (14:13)

## 2 PETRO

Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba. (3:9)



# Dakika 5 Za Kujifunza Biblia

Paula Bates

## Injili

1. Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi_______wake, bali uvumilie mabaya pamoja nami kwa ajili ya___, kwa kadiri ya ______ya Mungu; **2 Timotheo 1:8**
2. Maana ni kweli, sisi nasi __________habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa__________hao, kwa sababu halikuchanganyika na______ ndani yao waliosikia. **Waebrania 4:2**
3. Basi nilipofika_____ kwa ajili ya Injili______, nikafunguliwa mlango katika_________, **2 Wakorintho 2:12**
4. Kwa maana siionei_____ _____; kwa sababu ni uweza wa______ uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. **Warumi 1:16**
5. kwa nguvu za ishara na maajabu, katika nguvu za Roho Mtakatifu; hata ikawa tangu_________, na kando kando yake, mpaka _____nimekwisha kuihubiri_____ ya Kristo kwa utimilifu; **Warumi 15:19**
6. Nanyi pia, ninyi wenyewe mnajua, enyi Wafilipi, ya kuwa katika _________wa Injili, nilipotoka Makedonia, hakuna_________lingine lililoshirikiana nami katika habari hii ya kutoa na kupokea, ila ninyi peke yenu. **Wafilipi 4:15**
7. Tukamtuma Timotheo ndugu yetu,________wa Mungu katika________ ya Kristo, ili kuwafanya ninyi imara na kuwafariji kwa habari ya imani yenu; **1 Wathesalonike 3:2**

**Majibu:**

1. Mfungwa, Injili, nguvu
2. Tumehubiriwa, halikuwafaa, imani
3. Troa, ya Kristo, Bwana
4. Haya, Injili, Mungu
5. Yerusalemu, Iliriko, Injili
6. Mwanzo, kanisa
7. Mtumishi, Injili

# Yaliyomo

## Mungu

"Nakupenda"……………………………Betty Burton Choate……………………………18
Baadhi ya Vitu ambavyo Yesu Hasema…………Bill Dillon………………………….21
Asiyeonekana lakini si asiyejulikana…………………..David R. Pharr………………..23

## Ushahidi

Uumbaji na mageuko……………………..Rex Banks…………………………………………26

## Neno la Mungu

Yesu katika vitabu 66 vya Biblia………………………..Dave Hart……………………..27
Kitabu kinachopuuzwa zaidi………………………..Dalton Key………………………….30

## Wokovu

Umechelewa mno kulisimamisha gari moshi……….Bobby Dockery……………..31
Gharama kubwa ya maisha ya chini………………Michael L. King……………………34

## Kanisa

Nina ndoto……………………………Ronald D. Reeves…………………………………….39
Kwa nini lisiwe kanisa la chaguo la Bwana?...........Maxie B. Boren……………..42

## Fundisho La Kuishi Kwalo

Msaada katika udhaifu wetu………………………..Wayne Barrier……………………45
Somo katika Yeremia sura 37 – 39…………………David Conley…………………….47

## Ukristo Katika Vitendo

Ukristo wa karne ya 1 katika ulimwengu wa karne ya 21……Derek Broome…50
Paulo alifanya nini huko Arabuni……………………..Kevin L. Moore………………..52
Juhudi kwa ajili ya Mungu lakini s katika maarifa………Sunny David………….54

## Ibada

Unaleta Nini Ibadani?...............................Patrick Morrison………………………58

## Maisha Ya Kila Siku Ya Kikristo

Faida na Hasara………………………………J. Randal Matheny…………………………..63
Hakuna Awezaye Kuufuga Ulimi…………..........Alvin Jennings………………………..64
"Shukuruni kwa Kila Jambo"………………………Raymond Elliott……………………66

## NYUMBA YA KIKRISTO

Ulinzi wa Wazazi Wacha Mungu……………….Darrell Surrett……………………….68
Kuzijenga Ndoa Nzuri……………………………Dan R. Owen…………………………..71

## MASOMO KATIKA KIFUNGU

Mtakatifu na Heshima Ndilo Jina Lako……………Dennis Gulledge………………..73

## WAHUSIKA KATIKA BIBLIA

Uongo Mkuu wa Shetani………………Gary C. Hampton………………………………76
Mfano wa Epafra…………………………Neal Pollard……………………………………78

## MASWALI KATIKA BIBLIA

Vipi Kuhusu Mwizi Msalabani?...............Brian R. Kenyon…………………………81
Je! Wanahitaji Kujua Nini Kabla Hawajabatizw?.......Wes McAdams……………85

## MAJEDWALI NA MIHTASARI

Mambo Manne katika Ukristo……………Mark N. Posey…………………………….89

## HISTORIA YA KANISA

Kupambana na Utawala……………………Jeremy W. Barrier………………………..91

## VIPENGELE, MASHAIRI NA VIJAZI

Mamlaka ya Ukimya wa Kibiblia……………….Louis Rushmore……………………….4
Uungu wa Yesu…………………………………………Jerry Bates…………………………….6
Mbinguni Kutakuwaje?..............................J.C. Choate…………………………….11
Dakika 5 za kujifunza Biblia……………Paula Bates…………………………………….15
Rubi za Robison……………………………..Andy Robison……………………………22, 80
Tafuta Aya………………………………………………Jerry Bates………………………….37
Mzizi wa Dhambi……………………….Bonnie Rushmore………………………………..41
Je! Ulijua?.......................................Rebecca Rushmore…………………………..43
Tafuta katika Biblia………………………Martha Rushmore……………………………..44
Sarafu za Kenney………………………….David R. Kenney…………………………48, 74
Maoni ya Haraka……………………………Betty Burton Choate……………………….49
Vichekesho – Mithali 17:22…………………Jerry Bates………………………………….60
Unapimaje?.......................................Betty Burton Choate…………………………62
Msaka Tonge……………………………………Rebecca Rushmore…………………………..75
Mambo 25 Ambayo ShetaniHawezi Kufanya………Tim Childs…………………….77

# "Nakupenda"

Betty Burton Choate

Ni mara nyingi kiasi gani mfalme wa imaya atayageukia moja kati ya masomo yake na kujinyenyekeza hata hatua ya kutangaza kwa uwazi upendo wa kina na udumuo kwa ajili ya hilo, hata kabla ya maneno au maelezo ya upendo hayajaoneshwa kwa mfalme? Soma upya Kum. 7, nilishangazwa na ukweli kwamba Mungu alieleza upendo wake kwa kurudia rudia kwa ajili ya taifa teule la Israeli, akijiweka wazi kwa uwezekano wa kweli kwamba upendo aliokuwa akiutoa ungeweza kukataliwa.

***"Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako; Bwana Mungu wako, amekuchagua kuwa watu wake hasa, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi. Bwana hakuwapenda ninyi, wala hakuwachagua ninyi, kwa sababu mlikuwa wengi kuliko mataifa yote, maana mlikuwa wachache kuliko watu wote; bali kwa sababu Bwana anawapenda, na kwa sababu alitaka kuutimiza uapo wake aliowaapia baba zenu, ndiyo sababu Bwana akawatoa kwa mkono wa nguvu, akawakomboa katika nyumba ya utumwa, katika mkono wa Farao, mfalme wa Misri. Basi jueni ya kuwa Bwana, Mungu wenu, ndiye Mungu; Mungu mwaminifu, ashikaye agano lake na rehema zake kwao wampendao, na kushika amri zake, hata vizazi elfu; naye huwalipa wamchukiao mbele ya uso wao, kuwaangamiza. Hatakuwa mlegevu kwake yeye amchukiaye, atamlipa mbele ya uso wake. Basi zishike amri, na sheria, na hukumu ninazokuamuru leo, uzitende. Na itakuwa, kwa sababu mwazisikiliza hukumu hizi, na kuzishika na kuzitenda, basi Bwana, Mungu wako, atakutimilizia agano na rehema aliyowaapia baba zako; naye atakupenda na kukubarikia na kukuongeza tena ataubarikia uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, nafaka zako na divai yako, na mafuta yako, maongeo ya ng'ombe zako, na wadogo wa kondoo zako, katika nchi***

***aliyowaapia baba zako kuwa atakupa."*** (Kumbukumbu la Torati 7:6-13).

Halafu, katika maneno yafuatayo kuna subira kwa ajili ya kurudishiwa upendo wa uaminifu. ***"Laiti wangekuwa na moyo kama huu ndani yao sikuzote, wa kunicha, na kushika amri zangu zote sikuzote, wapate kufanikiwa wao na watoto wao milele!"*** (Kum. 5:29).

Leo kanisa ni watu waliochaguliwa na Mungu, Israeli wake wa kiroho, watu anaowapenda, si kwa sababu sisi ni wema na wenye nguvu katika ulimwengu bali ni kwa sababu ametufanya kuwa wake. 1 Yohana 4:10 inatuambia kile alichoambiwa Israeli ***"Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu."*** Lakini bado kuna utofauti mkubwa baina ya jinsi Waisraeli walivyomjua Mungu na namna sisi tunavyomjua.

Siku chache zilizopita, tulikuwa na ngurumo za radi, ngurumo ya radi hiyo ilikuwa ya sauti kubwa na miale ya umeme mkali ya kutisha akipiga tena na tena. Umewahi kufikiria kwa makini maelezo ya matukio pindi Mungu alipojitokeza katika Mlima Sinai, akionesha ukuu wake kwa Waisraeli? Kutoka 19:16-19 inasema:

***"Ikawa siku ya tatu, wakati wa asubuhi, palikuwa na ngurumo na umeme, na wingu zito juu ya mlima, na sauti ya baragumu iliyolia sana. Watu wote waliokuwa kituoni wakatetemeka. Musa akawatoa hao watu katika kituo, akawaleta ili waonane na Mungu; wakasimama pande za chini za kile kilima. Mlima wa Sinai wote pia ukatoa moshi, kwa sababu Bwana alishuka katika moto; na ule moshi wake ukapanda juu kama moshi wa tanuu, mlima wote ukatetemeka sana. Na hapo sauti ya baragumu ilipozidi kulia sana, Musa akanena, naye Mungu akamwitikia kwa sauti."***

Kama ningekuwa nimesimama kando ya Mlima huo na kushuhudia radi ya kutisha na umeme, moto, moshi ukifunika kila kitu, tetemeko la ardhi likitikisa Mlima wote, ngurumo kubwa ya radi na

kisha Sauti kubwa kupita kiasi ikizungumza, huenda ningeogopa kama Waisraeli walivyoogopa.

Hata hivyo, je, Mungu anajitokezaje kwetu katika Ukristo wa nyakati hizi? Kama Baba yetu mwenye huruma, anatupenda kiasi cha kumruhusu Mwanawe wa pekee afe msalabani ili atupatanishe kwa ajili ya dhambi zetu. Hivi umegundua kwamba katika kipindi cha Agano la Kale, kwa kawaida watu hawakumchukulia Mungu kama "Baba"? kupitia damu iliyomwagika msalabani, tumeasiliwa kama watoto halisi wa Mungu wa Mbinguni (Wagalatia 4:4-7), na ahadi ambayo ni Ndugu yetu ambaye daima anatuombea: ***"Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea. Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?"*** (Warumi 8:34,35).

## NANI ALIYEUPENDA ULIMWENGU? MUNGU AU YESU?

Yohana alisema, ***"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele"*** (Yohana 3:16). Yesu alisema, ***"Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake"*** (Yohana 15:13). Jibu: ***"Mimi na Baba tu umoja"*** (Yohana 10:30).

**Shadrack S. Msambaza**

## Mungu

# Baadhi Ya Mambo Ambayo Yesu Hakusema

Bill Dillon

Mara nyingi watu huzungumzia kile alichokisema Yesu, lakini kuna mambo mengi ambayo watu udhani Yesu alisema ambayo hakusema.

1. Yesu hakusema, “Mtakuwa waaminifu katika imani zenu na uaminifu wenu utawaweka huru.” Bali alisema, ***“tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru”*** (Yohana 8:32). Inawezekana kwa watu wema kuwa waaminifu katika dini zao na kwa uaminifu huo kukosea.
2. Yesu hakusema, “Juu ya mwamba huu nitayajenga makanisa yangu na watu wataabudu katika mojawapo watakalolichagua.” Hata hivyo, alisema, ***“…juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda”*** (Mathayo 16:18). Kama watu wanaweza kuabudu katika kanisa wanalolichagua, basi wanaweza kumwabudu Kristo watakayemchagua. Yesu alijenga kanisa moja pekee, na yeye ndiye kichwa cha kanisa hilo (Waefeso 1:21-22). Yesu hakusema, “Ye yote atakayemwacha mkewe kwa sababu yo yote na kumwoa mwanamke mwingine yuko huru na uzinzi na anaweza kuendelea na njia yake.” bali alisema, ***“Nami nawaambia ninyi, Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini”*** (Mathayo 19:9). Kulegeza katika kile ambacho viapo vya ndoa vimechukuliwa na kuvunjwa ni fedheha kubwa sana isiyopimika.
3. Yesu hakusema, “Yeye aaminiye ataokoka na anaweza kubatizwa baadaye kama akitaka.” Badala yake, alisema, ***“Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa”*** (Marko 16:16).

Agizo alilolitoa Yesu ni kuamini, kubatizwa na kisha wokovu, sio kuamini, kuokoka na kisha kubatizwa. Tafakari kuhusu hilo!

4. Yesu hakusema, "Mwanadamu anaweza kumwabudu Mungu kulingana na kujifunza kwake kwa asili, kulingana na kadiri awezavyo kujielezea." Hata hivyo, Yesu alisema, ***"Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli"*** (Yohana 4:24). Kwa kuwa "kweli" ni Neno la Mungu (Yohana 17:17), njia zetu za kumwabudu Mungu ni lazima zionekane katika Agano Jipya, mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu kwa nyakati hizi. Je, unaweza kuonesha katika Agano Jipya matendo uyafanyayo wakati unapomwabudu Mungu?
5. Yesu hakusema, "Vumilia makosa ya kidini, watu wote wana haki ya kidini kukosea, licha ya yote, hakuna shambulio lolote lililofanyika." Alisema, ***"Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki!...Enyi nyoka, wana wa majoka, mtaikimbiaje hukumu ya jehanam?"*** (Mathayo 23:13, 33). ***"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni"*** (Mathayo 7:21).

## Rubi za Robison

Paulo alipokwenda Thesalonike katika karne ya kwanza, kama ilivyoandikwa katika Matendo 17, alitumia mbinu za hoja za kimantiki kuweka shauri lake kuhusu Kristo. Alihojiana nao kutoka katika Maandiko ya Agano la Kale, akionesha unabii kuhusu Kristo. Alikuwa ***"akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu."*** Hilo ni, Maandiko ya Agano la Kale yakitabiri mateso na kufufuka kwa Kristo. Yesu wa Nazareti alitimiza Maandiko hayo katika kile kilichoandikwa, kwa wakati ule, kisa hicho hakikuwa cha muda mrefu. Paulo aliyaweka Maandiko upande mmoja na ushahidi upande upande mwingine na kulinganisha, kuhoji, kuelezea na kuonesha. Kama ilivyokuwa kawaida, baadhi waliamini, na baadhi walikasirika. Baadhi ya vitu havibadiliki.

# Asiyeonekana Lakini Si Asiyejulikana

**David R. Phart**

Petro alipowaandikia Wakristo waliokuwa wakiishi katika miji ya Asia Ndogo, lengo lake lilikuwa ni kuwatia moyo wadumu katika uaminifu wao hata wanapokabiliwa na ***"msiba"*** kutoka kwa adui zao (1 Petro 1:7; 4:12). Hayo yalitarajiwa kwa sababu ya upendo na imani yao kwa Mwokozi. Alieleza: ***"Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona, ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu"*** (1 Petro 1:8). Wao binafsi hawakuwahi kumwona Yesu, lakini walimpenda na kumwamini. Katika imani yao, **hakuwa anaonekana, lakini siye asiyejulikana!**

Baadhi ya watu leo wanadhani kwamba ilikuwa ni rahisi sana kwa watu walioishi katika nyakati za Agano Jipya kuwa waamini kwa sababu walikuwa karibu na muda ambao Kristo alikuwa duniani. Ukweli ni kwamba Wakristo wengi katika kanisa la awali hawakuwahi kumwona Yesu. Huduma yake ilikuwa imeenea katika eneo dogo sana la dunia, ingawa alionekana na watu wengi wa nchi yake, hicho kilikuwa ni kipande kidogo sana cha watu. Kilicho cha muhimu zaidi ni kwamba ni ufufuko wake ambao ndio msingi wa imani yetu, na wachache pekee – wachache sana – waliomwona baada ya kufufuka. Katika 1 Wakorintho 15:4-8, Paulo alitoa orodha ndogo ya wale waliomwona, katika hiyo Mariamu Magdalene anaweza kuongezwa, baadhi ya wanawake wengine, na Kleopa na rafiki yake waliokuwa wakitembea naye kuelekea Emau. Msisitizo upo kwa mitume, ambao kwao Yesu

***“aliwadhihihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi”*** (Matendo 1:3). Paulo alikuwa ni mtu wa mwisho kupewa fursa hii (1 Wakorintho 15:8).

Ni sahihi kuuliza, kwa hiyo, “Ilikuwaje watu wengi kumwamini Yesu aliyefufuka wakati hawakuwahi kumwona?” Jibu ni kwamba walishawishika kwa ushuhuda wa mitume mashahidi wa kuona. Hiyo ndiyo ilikuwa njia ya Bwana iliyoelezewa katika Matendo 10:40-42, ambapo mtume alimzungumzia Kristo kuwa alifufuka na kujionesha dhahiri; ***“si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, ndio sisi*** [mitume]***,”*** Njia ya kiroho ni kwamba ukweli kuhusu Kristo ufunuliwe kwa ulimwengu kwa njia ya ushuhuda wa mitume waliochaguliwa kwa ajili ya kazi hii. Akiwapa kazi, Yesu alisema, ***“nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya”*** (Luka 24:48; linganisha na Matenso 1:8). Hivyo, mahubiri yao yalikazia, ***“Yesu huyu Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake”*** (Matendo 2:32).

Hata hivyo, hili linaibua swali: Kwa nini ushuhuda wa watu hawa ukubalike? Nini kinachowafanya wao kuaminika?” Yesu alieleza kwamba ushuhuda wao utaunganika na Roho Mtakatifu (Yohana 15:26-27; Matendo 5:32). Roho aliwaongoza katika ***“kweli yote”*** (Yohana 16:13), jambo ambalo linatuhakikishia kwamba Roho aliongoza ushuhuda wao katika Agano Jipya. Lakini, tunawezaje kujua kwamba ushuhuda wao ni kweli? Kila shahidi wa kuona ni lazima apimwe kwa vipimo hivi vifuatavyo.

**Je, mashahidi walikuwa na ustadi?** Je, walikuwa na uwezo wa kutoa ushahidi wenye mantiki? Agano Jipya lenyewe linaonesha mantiki na uwezo wao. Watu wasio na uwezo wasingeweza kuzalisha nakala ya namna hiyo.

**Je! Walikuwa katika nafasi ya kujua ukweli?** Mtu hawezi kushuhudia mpaka awe ameona jambo na isipokuwa amelitambua jambo hilo aliloliona. Yesu hakuwa mgeni kwa mitume. Pindi alipowaonesha kuwa alikuwa anaishi ***“kwa dalili nyingi”*** (Matendo 1:3), walijua bila shaka alikuwa ni yeye na kwamba walimwona akifa na kuzikwa.

**Je! Ushahidi wao ulikuwa kwa sababu ya matarajio?** Je! Walikuwa na matarajio sana kwamba angefufuka kiasi kwamba wakajenga picha kuwa ilikuwa ni kweli? Ukweli ni kwamba hawakutarajia kabisa kwamba angefufuka. Walidhani kwamba msalaba ndio ulikuwa mwisho wa matumaini yao na hawakuweza kuamini mpaka Yesu alipowathibitishia kuwa ni yeye.

**Je! Mashahidi walikubaliana miongoni mwao?** Ilikuwa inakubalika kwamba mashahidi wawili au watatu wanaweza kuthibitisha jambo. Lakini, hata mashahidi wa kweli wawili au watatu wanaweza kuwa na kutokukubaliana. Miongoni mwa mashahidi wa kitume, hata hivyo, hakuna ukinzani. Ushuhuda wao ni sahihi na unakubaliana kwa asilimia mia moja.

**Hatimaye, ni wazi kwamba mashahidi hawawezi kuaminika isipokuwa tumeshawishika kuwa ni watu wa kuaminika.** Je! Tunaweza kuwa na uhakika kwamba mitume walikuwa ni watu wanaoaminika kuwa wanasema ukweli? Kwa hakika tunaweza, kwa sababu walikuwa tayari kufa kwa ajili ya ushuhuda wao. Watu wanaweza kufanya mambo mengi kuficha uwongo, lakini hakuna atakayekufa kwa sababu anayoijua kuwa ni uwongo.

Hatujamwona Yesu, lakini tunamjua kwa njia ya ujumbe wa Injili (Yohana 20:30-31). Katika maneno ya Simoni Petro, ***“Nasi tumesadiki, ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu”*** (Yohana 6:69). **Haonekani, lakini si asiyejulikana!**

**2 Wakorintho 5:7**

**“Basi siku zote tuna moyo mkuu; tena twajua ya kuwa, wakati tuwapo hapa katika mwili, tunakaa mbali na Bwana. Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona”**

# Uumbaji au Mageuko

**Rex Banks**

Kama alivyoshuhudia majaribio ya kusikitisha ya viongozi wa kidini katika karne ya 19 kupatanisha maelezo ya Biblia kuhusu uumbaji na nadharia ya mageuko. Thomas Huxley mtu wa kufuru aliiondoa Biblia "…kitabu cha ajabu chenye kunyumbulika ambacho kinaweza kufanywa kimaanishe chochote ambacho mtumiaji wake anaweza kutamani kimaanishe!" Miaka 50 baadaye katika kipindi kilichoitwa *"Scopes Monkey Trial,"* waandishi walidhihaki majaribio ya William Jennings Bryan na wabunifu kutetea kitabu cha Mwanzo kwa kulinganisha "siku" za uumbaji na "miaka" mingi ya Jiolojia.

Biblia iliteseka pindi "ilipotetewa" na wale ambao walitafuta kuitafsiri upya ili kuendana na mafundisho ya sasa ya mageuko. Jitihada hizo zilizopotoshwa, chimbuko lake ni kushindwa kutambua kwamba **nadharia ya mageuko ni adui wa kimwili wa Ukristo.** Kwa upande mwingine, viongozi wengi watetezi wa nadharia hii, kwa uwazi hutambua kwamba fundisho la mageuko ni jiwe la pembeni la wapinga Ukristo wa leo wenye sumu kali sana katika mfumo wa fikra. Zingatia baadhi ya maadui wakubwa zaidi wa Ukristo – Atheism (fundisho linalosema hakuna Mungu), Ukomonisti, nk – katika baadhi ya maoni yafuatayo kwa kuwaongoza wanamageuzi.

Baadhi ya wanamageuko wanaweza kupinga kwamba wanaikubali Biblia kama Neno la Mungu na kukataa mawazo mengine ya imani tofauti. Hata hivyo, hili linawezekana kwa wale tu ambao wana uwezo wa kupuuzia uhusishaji wa nadharia hiyo. Mmoja kati ya wanamageuko wakubwa wa siku za leo, bwana Arthur Keith, aliandika katika kitabu chake, *Mageuko na Maadili (Evolution and Ethics),* "Sheria ya Kristo haipatani na sheria ya mageuko, maadamu sheria ya mageuko imefanya kazi hata sasa. Hivyo, sheria hizo mbili ziko vitani zikishindana; sheria ya Kristo kamwe haiwezi kushinda mpaka sheria ya mageuko iharibiwe." Yesu alisema, ***"Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri."*** (Mathayo 7:18).

# Yesu Katika Vitabu 66 Vya Biblia

Dave Hart

- Katika Mwanzo:
  Uzao wa Mwanamke
- Katika Kutoka:
  Mwana-kondoo wa Pasaka
- Katika Mambo ya Walawi: Kuhani Mkuu.
- Katika Hesabu:
  Wingu na Moto
- Katika Kumbukumbu la Torati:
  Nabii Kama Musa
- Katika Yoshua:
  Nahodha wa Wokovu Wetu
- Katika Waamuzi:
  Jaji na Mtoa Sheria
- Katika Ruthu:
  Mkombozi wa Jamaa wa Karibu
- Katika 1 na 2 Samweli:
  Nabii wa Bwana
- Katika 1&2Wafalme, 1&2 Mambo ya Nyakati:
  Mfalme Anayetawala
- Katika Ezra:
  Mwandishi Mwaminifu
- Katika Nehemia:
  Mjenzi wa Kuta Zilizovunjika
- Katika Esta:
  Mordekai
- Katika Ayubu:
  Mchana kutoka Juu
- Katika Zaburi:
  Bwana Aliye Mchungaji Wetu
- Katika Mithali na Mhubiri:
  Hekima
- Katika Wimbo Ulio Bora:
  Mpenzi na Bwana Harusi
- Katika Isaya:
  Mfalme wa amani.
- Katika Yeremia na Maombolezo:
  Nabii anayelia.
- Katika Ezekieli:
  Magurudumu ya kugeuka.
- Katika Danieli:
  Mtu wa 4 katika tanuru la kutisha.
- Katika Hosea:
  Bwana arusi aliyemwoa mwanamke mzinzi.

- Katika Yoeli:
  Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto
- Katika Amosi:
  Mbeba mizigo.
- Katika Obadia:
  Mwokozi Mwenye Nguvu.
- Katika Yona:
  Mungu Mwenye Kusamehe.
- Katika Mika:
  Mjumbe mwenye miguu mizuri.
- Katika Nahumu:
  Mlipiza kisasi kwa ajili ya wateule wa Mungu
- Katika Habakuki:
  Mwinjilisti Mkuu, Akililia Uamsho.
- Katika Sefania:
  Mrejeshaji wa Urithi wa Mungu Uliopotea.
- Katika Hagai:
  Chemchemi ya Utakaso.
- Katika Zekaria:
  Baba Mwenye Huruma
- Katika Malaki:
  Mwana wa Haki, Akiinuka na Uponyaji katika mbawa zake
- Katika Mathayo:
  Masihi
- Katika Marko:
  Mfanyakazi wa Maajabu
- Katika Luka:
  Mwana wa Adamu.
- Katika Yohana:
  Mwana wa Mungu.
- Katika Matendo:
  Bwana Aliyepaa.
- Katika Warumi:
  Mwenye Haki.
- Katika 1 na 2 Wakorintho:
  Karama za Roho.
- Katika Wagalatia:
  Anayetuweka huru
- Katika Waefeso:
  Kristo wa utajiri
- Katika Wafilipi:
  Mungu anayekidhi kila hitaji letu.
- Katika Wakolosai:
  Utimilifu wa Uungu
- Katika 1 & 2 Wathesalonike:
  Mfalme ajaye hivi karibuni.
- Katika 1 & 2 Timotheo:
  Mpatanishi baina ya Mungu na mwanadamu.
- Katika Tito:
  Mchungaji Mwaminifu.
- Katika Filemoni:
  Rafiki aliye karibu kuliko ndugu.
- Katika Waebrania:
  Damu inayoondoa dhambi zangu.
- Katika Yakobo:
  Tabibu Mkuu.

- Katika 1 & 2 Petro: Mchungaji Mkuu.
- Katika 1, 2 & 3 Yohana: Upendo wa milele.
- Katika Yuda: Bwana aliyeshuka na watakatifu 10,000.
- Katika Ufunuo: Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

- **2 Petro 1:21** Kwa maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

- **1 Wakorintho 2:13** Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho; tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.

- **Zaburi 119:105** Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu.

- **Waebrania 4:12** Maana Neno la Mungu li hai, lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudio. ya moyo

- **Zaburi 19:7** Sheria ya Bwana ni kamilifu huiburudisha nafsi.

# Neno la Mungu
# Kitabu Kinachopuuzwa Zaidi

Dalton Key

Biblia ni kitabu bora na pia ni moja kati ya vitabu vyote vinavyopuuzwa ulimwenguni. Kwa sababu ni bora, inastahajabisha kinapuuzwa namna hiyo.

Biblia inafanya kazi kama mbegu, inawaleta watoto katika familia ya Mungu. Katika mfano wa Yesu wa Mpanzi, ililiweka hili bayana kwamba ***"Mbegu ni neno la Mungu"*** (Luka 8:11), na ***"Mpanzi huyo hulipanda neno"*** (Marko 4:14). Ni kwa njia ya Neno la Mungu pekee ndipo watoto wa Mungu huzaliwa (1 Petro 1:23). Jambo moja rahisi ni kwamba mtu hawezi kuja katika familia ya Mungu wakati anaipuuza au kuipita mbegu hii. Hata hivyo, roho nyingi zisizojali katika siku zetu za leo wanashindwa kuiruhusu mbegu ya Neno la Mungu kuota mizizi katika mioyo yao.

Biblia inaishi na inatenda kazi na ina ***"ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili"*** kama inavyochoma katika moyo, inayatambua mawazo ya makusudi ya moyo (Waebrania 4:12). Watu katika Matendo 2 walilisikia Neno lililovuviwa, ***"wakachomwa mioyo yao"*** (mst. 37), waliambiwa ***"Tubuni mkabatizwe…mpate ondoleo la dhambi zenu"*** (mst. 38), na wakawa watiifu katika ujumbe wa Mungu, hivyo, wakafurahia uhuru kutoka katika kifungo chao cha dhambi. Tofauti wasikiaji hawa wenye hekima, roho nyingi zisizojali katika siku zetu za leo na wapuuzi wanapuuza kitabu kimoja chenye suluhisho la tatizo lao kuu – tatizo la dhambi.

Biblia inaitwa ***"upanga wa Roho"*** (Waefeso 6:17). Kama upanga, unamlinda askari wa Kikristo anaposimama kuzipinga ***"hila za Shetani"*** (Waefeso 6:11). Kwa sababu ***"mshitaki…Ibilisi, kama simba angurumaye,..akitafuta mtu ammeze"*** (1 Petro 5:8). Sisi sote tunahitaji silaha zinazotolewa na Mbingu. Lakini Wakristo wengi sana wanaonekana kuridhika kukabiliana na Ibilisi bila ya kuwa na silaha na kutokujali kuhusu hila zake (2 Wakorintho 2:11). Je! Inaleta maana yoyote kwamba kitabu hicho chenye utekelezaji na faida kwamba itakuwa ni huzuni sana kukipuuza? Je! Biblia yako imepuuzwa?

# Umechelewa Mno Kulisimamisha Gari Moshi

**Bobby Dockery**

Huduma ya jamii kwenye Runinga imewaasa madereva kuzingatia onyo wakati wanakaribia kuvuka reli. Kulingana na taarifa, gari moshi linasafiri kwa mwendo wa maili 30 kwa saa ikichukua nusu maili ili kusimama. Ajali nyingi mbaya zimekuwa ni matokeo ya uzembe wa madereva wanapofika kwenye reli inakuwa vigumu kwa gari moshi linalokuja kusimama.

Habari ya mfalme Yosia kwenye Biblia inatoa habari sambamba. Yosia alikuwa mfalme bora katika wafalme wa Yuda ingawa hakuwa mwenye hekima kuliko wote, tajiri, au mwenye jeshi kubwa. Hakuna mfalme mwingine aliyekuwa na moyo wa dhati wa kujitoa kwa Mungu! Wakati Yosia alipoanza utawala wake, alianzisha sera ya mageuzi yenye lengo la kutakasa nchi kutoka katika ibada ya sanamu na uasi. Alianza ukarabati wa Hekalu la Yerusalemu, ambalo lilikuwa limeanguka katika magofu. Wakati kazi hii ilipokuwa inaendelea, Hilkia kuhani alipata kitabu cha sharia za Mungu kwenye magofu. Wakati neno la Mungu liliposomwa mbele ya uwepo wa mfalme Yosia, alirarua mavazi yake kwa kelele! Alitishwa na kutambua kuwa watu wake wamejitenga mbali na mapenzi ya Mungu kwa sababu wameacha kujihusisha na neno lake.

Yosia alituma watu ili asikie kutoka kwa manabii wa Mungu nini hatima ya taifa lake. Baadaye lilikuja onyo kwamba Mungu atamimina ghadhabu yake juu ya Yerusalemu na Yuda kwa sababu ya dhambi ya kupuuza neno lake! Ingawa Yosia peke yake ataepushwa, lakini uharibifu utakuja na hakuna atakayeweza kuzuia maandamano yasiyoweza kuepukika. Mapinduzi ya Yosia yalikuja kwa kuchelewa sana! Mungu tayari alikuwa ameshaanzisha mchakato wa historia wa

kuiangamiza Yerusalemu. Ilikuwa kuchelewa mno kusimamisha gari moshi.

Somo linaeleweka: Kuna hatua ya hakuna kurudi nyuma kwa Mungu jinsi anavyoshughulika na watu wake:

1. Huu ni ukweli kwa mataifa. Binadamu katika karne ya 21 amejaribu kumwondoa Mungu kwenye historia. Tunatarajia kuwa nyanja ya uendeshaji wa Mungu ni kanisa, wakati mambo ya serikali yanaongozwa na makongamano na bunge. Tunaongea kwa upole kuhusu "kutengwa kwa kanisa na serikali" ingawa mambo haya yanaonekana yanawezekana! Ni hapana na kamwe haitakuwa. Mungu hawezi kutengwa na serikali kwa sababu serikali zinainuka na kuanguka kwa mapenzi yake. Matendo 17:26 inaeleza kuwa Mungu anaainisha nyakati zilizowekwa za mataifa na anaweka mipaka ya makazi yao. Historia si kitu bali kumbukumbu za Mungu katika kutenda kazi na mataifa. Biblia inathibitisha kuwa Mungu kwa kurudia ameangusha mataifa wakati kikombe chao cha ghadabu kinapokuwa kimefurika (Warumi 1:18). Vipi kuhusu Afrika? Ombea isije ikawa kuchelewa mno kusimamisha gari moshi.
2. Hii ni kweli kuhusu familia. Watu wengi wakiulizwa watakubaliana na hitaji la mafundisho ya kiroho kwa watoto wao. Bado, wengi wao hawaendi kanisani mara nyingi. Mwelekeo wa maisha ya kiroho umepuuzwa. Wameridhika kujiahidi wenyewe, "siku fulani tutaanza kuwapeleka watoto katika madarasa ya Jumapili na kanisani….. wakati mwingine tutatafuta muda wa kuwa na Mungu!" Lakini Sulemani aliwaonya kuwa tutasubiri sana! ***"Mkumbuke muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja siku zilizo mbaya, wala haijakaribia miaka utakaposema, mimi sina furaha katika hiyo"*** (Mhubiri 12:1). Tunaweza kusubiri sana kuwaleta familia zatu kwa Mungu!

3. Hii ni kweli kwa watu binafsi. Tunaweza kusubiri hadi itakapokuwa tumechelewa sana kuepuka matokeo ya dhambi. Mungu ana sheria za asili na vilevile sheria za kiroho. Kwenye enzi zote tutavuna tulichokipanda (Wagalatia 6:7-8). Kuna uwezekano wa kuwa nje ya Kristo kwa muda mrefu hadi kukosa nafasi ya kutubu (Waebrania 12:17). Mioyo inaweza kufanyika migumu kwenye kupuuza; tunaweza kunasa kwenye dhambi hadi tukaona vigumu kunasuka! Hakuna hatua ya kurudi kwa roho.

Ingawa watu wengi wanajaribu kutokufikiria kuhusu hilo, kuna siku inayokuja ya kuhesabiwa na Mungu. Wakati wa kujiandaa kwa siku hiyo inayokuja ya hukumu ni sasa. Wakati utakuja ambao utakuwa umechelewa sana.

**Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi, waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao; bali wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane, pakawa na kelele, Haya, bwana arusi; tokeni mwende kumlaki. Mara wakaondoka wanawali wale wote, wakazitengeneza taa zao. Wale wapumbavu wakawaambia wenye busara, Tupeni mafuta yenu kidogo; maana taa zetu zinazimika. Lakini wale wenye busara wakawajibu, wakisema, Sivyo; hayatatutosha sisi na ninyi; afadhali shikeni njia mwende kwa wauzao, mkajinunulie. Na hao walipokuwa wakienda kununua, bwana arusi akaja, nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa. Halafu wakaja na wale wanawali wengine, wakasema, Bwana, Bwana, utufungulie. Akajibu akasema, Amin, nawaambia, siwajui ninyi. Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa.** (Mathayo 25:1-13).

# GHARAMA KUBWA YA MAISHA YA CHINI

Michael L. King

Wahusika wengi wa Biblia na watu wa zama za kizazi chetu wanaweza kushuhudia ukweli huu kwamba ***"mshahara wa dhambi ni mauti"*** (Warumi 6:23). Ufafanuzi rahisi wa kifo ni "kutengwa." Wakati mtu anapopokea malipo kwa dhambi zake, inamtenga na kila kitu kinachosimama kwa haki na uzuri. Dhambi inatenganisha wanafamilia, inasambaratisha ndoa na kuwatawanya waumini wa kanisa, siyo tu kwa Mungu wao bali na kwa ndugu wa kiroho na dada katika Kristo. "Maisha ya chini" yanasababisha mtu kutengwa kwenye maisha haya katika kifo halisi kutokana na mazoea na mwenendo wa kibinafsi unaotishia afya na usalama wake. Watu wengi wanaishi maisha ambayo yana mgongano na umilele badala ya kupatana.

Dunia yetu leo inasumbuliwa na matatizo ya mahusiano ya ngono haramu, kama vile Ukimwi, Kaswende, Kisonono, misongo ya mawazo, matatizo ya uzazi na kuzaa nje ya ndoa. Kile ambacho kinaweza kuonekana kuwa cha kufurahisha wakati wa kujihusisha na tabia hizi ni sawa kwa kulinganisha na maisha duni wanayounda. Gharama kubwa halisi ya maisha haya ya chini inaweza isionekane wazi kwenye maisha haya, lakini itajionyesha yenyewe kwenye hukumu, kumfanya mtu asikubalike kabisa kuingia Mbinguni. Tunapaswa kuandamwa na mawazo ya kumsikia Bwana akisema katika hukumu. ***"Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mlio laaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake"*** (Mathayo 25:41).

Kuna gharama kubwa kumwakilisha Mungu wa Mbinguni na miungu ya ulimwengu huu-kupenda mali! Tumeonywa kuwa ***"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilicho duniani, yaani tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi***

***cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele"*** (1 Yohana 2:15-17). Umegundua utengano mwingine kwenye kifungu hiki? Ukiipenda dunia na vitu vya dunia upendo alionao mtu kwa Mungu hufa (mst 15). Hatuna cha kuonyesha katika maisha marefu ya upotevu kwa juhudi za ubinafsi kwa kutojali kabisa "kuweka hazina mbinguni" na kufurahia faida iliyopatikana wakati unaishi hapa (Mathayo 6:33). Wazo lingine la uchochezi linachukuliwa kuwa kitendawili katika Maandiko. ***"Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakaye poteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona"*** (Mathayo 16:25).

Mwanampotevu ni mfano halisi wa mtu aliyelazimika kulipa gharama kubwa kwa maisha ya chini (Luka 15:12-14). Kutengana kulikuwa kwa hiari yake; hakushurutishwa au kulazimishwa na mvuto wowote wa nje, bali kutoka ndani ya moyo wake mwenyewe wenye tatizo. Kwa tafsiri baba kwenye mfano huu ni Mungu na mwana mpotevu anawakilisha mtu aliyejitenga katika kutafuta utimilifu wa shauku ambayo haiwezi kuvumiliwa na baba yake. Yakobo anashauri kwamba hili linatokea na linaweza kumtokea mtu yeyote. ***"Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti"*** (Yakobo 1:14-15). Dhambi humpeleka mtu mbali, humuweka muda mrefu zaidi na hufanya uharibifu mwingi sana kuliko tunavyoweza kufikiria.

Jamii nzima ya kibinadamu ilidhulumiwa na wanadamu kwa uamuzi mbaya wa Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni kwa kula tunda lililokatazwa. Hapa tena tunaona utengano uliotokea, kwa kuingia katika himaya ya Mungu waliyokatazwa, ***"Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini, wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani"*** (Mwanzo 3:8). Walijitoa wenyewe "kwenye uwepo wa Mungu" kwa sababu hapakuwa na makubaliano kati ya alichokitaka Mungu na kile walichokuwa wakikifanya (Mwanzo 3:23-24). Walibadilisha uzuri wa


bustani kuwa taabu, kutindua ardhi na kupata chakula kwa jasho la nyuso zao. Je, umeshawahi kujiuliza kuwa ni vitu gani vingekuwa kama wangetii mapenzi ya Mungu kuhusu matunda ya mti huo? Nyongeza ni kwamba uchungu uliongezeka kwa mwanamke wakati wa kuzaa, ardhi ilijaa miba na michongoma, na kifo kikapita juu ya wanadamu wote (Mwanzo 3:14-18). Hata nyoka alipata adhabu mbaya kwa sababu ya kuwafanya Adamu na Hawa kuendea maisha ya chini kwa kutokutii; kwa hiyo, akafanywa kutambaa kwa tumbo lake na kula mavumbi siku zote za maisha yake (mst 14).

Kuna suluhisho la kijinga la kurekebisha tatizo la dhambi na maisha ya chini, ambalo kwalo mtu huinuliwa kumtukuza na kuonekana kwenye uwepo wa Mungu. Hakuna gharama lakini hutoa gawio. Yakobo anaelezea ***"Basi mtiini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbia. Mkaribisheni Mungu naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi,na kuisafisha, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. Huzunikeni na kuomboleza na kulia. Kucheka kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza, na furaha yenu kuwa hamu. Jidhilini mbele za Bwana, naye atawakuza"*** (Yakobo 4:7-10). Kuna wakati watu wa Mungu, Wayahudi, waliharibika sana wakaliacha hekalu (Ezekieli 11:23). Baadaye Aliwarudia walipofanya uwepo mtakatifu kwake. (**Shekinah** inamaanisha Mungu ambaye yupo ndani yao). Ni jinsi gani inasikitisha na kuogopesha kwa Mungu kujitoa Mwenyewe kwenye mioyo au maisha ya leo?

**"Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai"**

**Waebrania 10:31**

# TAFUTA AYA




1. Taja mambo manne ambayo Paulo alisema yaliwatokea akina baba wote wa Kiyahudi walipokuwa jangwani. (mst. 1-4)
2. Nani alikuwa Mwamba wa kiroho ambaye kutoka kwake wote walikunywa kinywaji? (mst. 4)
3. Nini kiliwatokea wengi wao jangwani na kwa nini? (mst. 5)
4. Mambo yaliyowatokea Waisraeli yalikuwa______kwetu kusudi sisi tusiwe watu wa____________kama wale nao________ (mst. 6)
5. Msiwe___________kama wengine wao walivyokuwa (mst. 7)
6. Hatupaswi kufanya__________kama wengine wao walivyofanya. (mst. 8)
7. Wangapi walikufa katika siku kwa sababu ya dhambi? (mst. 8)
8. _________kama wengine wao walivyomjaribu wakaharibiwa na_______ (mst. 9)
9. Kwa nini haya yote yaliandikwa? (mst. 11)
10. Anapaswa kufanya nini mtu anayejivuna yeye mwenyewe na nafasi yake na kwa nini? (mst. 12)
11. Je, kuna mtu yeyote aliyewahi kujaribiwa tofauti na mtu mwingine yeyote? (mst. 13)
12. Je, Paulo alimaanisha nini aliposema “Mungu ni mwaminifu”? (mst. 13)

13. Paulo alisema nini kuwa Mungu pia atafanya kwa ajili ya watu wake wanapokabiliana na majaribu? (mst. 13)

**1** Kwa maana, ndugu zangu, sipendi mkose kufahamu ya kuwa
baba zetu walikuwa wote chini ya wingu; wote wakapita kati ya bahari;
**2** wote wakabatizwa wawe wa Musa katika wingu na katika bahari;
**3** wote wakala chakula kile kile cha roho; **4** wote wakanywa kinywaji
kile kile cha roho; kwa maana waliunywea mwamba wa roho
uliowafuata; na mwamba ule ulikuwa ni Kristo. **5** Lakini wengi sana
katika wao, Mungu hakupendezwa nao; maana waliangamizwa
jangwani.

**6** Basi mambo hayo yalikuwa mifano kwetu, kusudi sisi tusiwe
watu wa kutamani mabaya, kama wale nao walivyotamani.
**7** Wala msiwe waabudu sanamu, kama wengine wao walivyokuwa;
kama ilivyoandikwa, Watu waliketi kula na kunywa, kisha wakasimama
wacheze. **8** Wala msifanye uasherati, kama wengine wao walivyofanya,
wakaanguka siku moja watu ishirini na tatu elfu. **9** Wala tusimjaribu
Bwana, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaharibiwa na nyoka.
**10** Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyonung'unika,
wakaharibiwa na mharabu. **11** Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa
jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya
zamani.

**12** Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie
asianguke. **13** Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya
wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe
kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa
kutokea, ili mweze kustahimili.

**UJUMBE:** Paulo alikuwa akipambana kuwatia moyo Wakorintho wawe waangalifu na wavumilivu katika kazi ya Bwana. Aliwakumbusha baraka zote za kiroho ambazo baba zao walizipata jangwani. Wote walipata baraka sawa; hata hivyo, wengi wao walikufa jangwani kwa sababu ya dhambi yao. Paulo alisema kwamba mambo yale ni mifano kwetu. Yanatuonesha kwamba heti kwa sababu tunapokea baraka za kiroho si hakikisho kwamba tutaurithi uzima wa milele. Hii ndiyo ilikuwa hoja ya msingi ya Paulo.

# NINA NDOTO

Ronald D. Reeves

Pengine maelezo na nukuu hiyo hapo juu itasisitizwa kwa miaka mingi kupitia kumbi za taasisi zinazojitolea kuhifadhi uhuru uliotolewa na Mungu ambao bila shaka kila mmoja wetu amekuja kuuenzi kama raia katika jamii huru. Kwenye miaka iliyopita, nilisikiliza kwa makini sana hotuba ambayo ilibatilisha maneno yaliyo hapo juu. Kama wengine wengi, nina hisia kali kuhusu suala hili, na shauku yangu hakika imechochewa na unyanyasaji wa kihistoria wa watu wetu wowote katika taifa letu na jamii. Kama kiongozi wa harakati za haki za raia katika miaka ya 60 aliunda na kushirikisha ndoto yake kuhusu masuala muhimu ya siku kuhusiana na mrejesho wa jamii huru na yenye usawa, kila mmoja wetu leo, kama mshirika wa kanisa la Agano Jipya, ni lazima tutengeneze na kushirikisha ndoto zetu kuhusu ustawi wa baadaye wa kanisa la Bwana kwenye kizazi chetu.

Wakati umefika, siyo kwa kusanyiko la mtu tu, bali kwa makusanyiko kote ulimwenguni, kuukabili ukweli wa mahitaji ya watu na changamoto, na kuyaelezea kwa nguvu, wakati bado tuna muda, nafasi, nguvu na uwezo wa kufanya hivyo. Inaweza kuwa uongozi kote nchini na kwa ndugu zetu wapendwa wote sio tu kwamba watasikiliza upya na kwa hamu sauti ya watu wanaowatumikia, bali pia watatamani hekima ya kupambanua kati ya safu ya mapendekezo ambayo yanaweza kuwekwa mbele yao. Waheshimiwa viongozi wetu katika kila kusanyiko kwa juhudi waongoze watu wa Mungu kufikia malengo muhimu ya kiroho ambayo ni lazima yaelezwe kama sisi, watu wa Mungu, tuna tumaini lililo jema la mafanikio ya kukamilisha kazi ya Mungu kwenye jamii yetu.

Ndiyo, nina ndoto kwa ajili ya watu wa Mungu. Ninaota siku ambayo watu wote wa Mungu wataabudu pamoja kwa sababu kila

kizuizi kimeondolewa na kimaandiko, bila kujali vizuizi. Ninaota siku ambayo viongozi watumishi kama wazee wamekumbatia makusanyiko wanayoyahudumia badala ya kuponda roho zao, iwe kwa kupanga au kwa bahati mbaya. Ninaota siku ambayo washirika wataitikia uongozi bora wa kiroho kwa kupaza sauti ya roho ya Isaya na kusema ***"Nipo hapa, nitume mimi."***

Ninaota siku ambayo mashemasi kwenye makusanyiko yote ya watu wa Mungu wamepewa majukumu mazito kuwaelekeza na kutekeleza juhudi maalum iliyoundwa ya kufikia jamii kama sote tunavyojitahidi kukamilisha huduma hiyo ya kanisa. Ninaota siku ambayo uongozi wa wazee kote wanawaamini ndugu wanaowahudumia kwamba washirika pamoja na mashemasi, wanachukua mzigo ambao kwa kawaida wazee huubeba, kwa maana ya kwamba wazee watazingatia kuhusu masuala ya kiroho na hatima za roho zilizo chini ya uongozi wao. Ninaota siku ambayo mipango ya kazi haiendeshwi tena kama chanzo cha kuwavutia watoto wa Mungu kufanya kazi ya watoto wa Mungu, yote haya ni kwa sababu sisi kama ndugu katika Kristo tunahamasika wenyewe na tunatumia vipawa ambavyo tumebarikiwa navyo.

Ndiyo, nina ndoto, ninaota siku ambayo roho changamfu ya kusanyiko iliyojitolea kwa ukuaji wa kweli na wa namna nyingi itadumishwa, bila kujali mafanikio ya kihistoria yaliyopatikana. Ninaota siku ambayo utatuzi wa migogoro ni kawaida katika kusanyiko letu badala ya ubaguzi. Ninaota siku ambayo roho ya mtu kujikana nafsi yake kwa ajili ya manufaa ya wengine itaenea sana ndani yetu kiasi kwamba makusanyiko yetu yote yatafanya kazi nzuri tunapofanya kazi ya Bwana, tunapofanya kazi kwa bidii katika uinjilisti.

## NDIYO NINA NDOTO KWA WATU WA MUNGU

Ninaota siku ambayo watu wetu watafahamika kwa uelewa wao wa Biblia, uwezo na shauku ya kumfundisha yeyote kwa wakati wowote. Ninaota siku ambayo ushirika kati ya watu wa Mungu umeendelezwa kulingana na mtazamo wa Agano Jipya kuhusu ushirika.

Ninaota siku ambayo mahitaji ya makundi mengine kwenye kusanyiko letu yanashughulikiwa bila upendeleo.

Ninaota pindi siku ambayo…..ndiyo, nina ndoto, na ninataka wewe pia uote pia! Bado, hili halitoshi. Kuwa na ndoto ambayo haina tumaini la kukamilisha, na kukuza kukata tamaa. Kwa kweli, ninahitaji zaidi ya kukata tamaa ya kukamilisha ndoto. Naomba kwa ujasiri, kupitia uongozi uliowekwa na Mungu na kuthubutu kusema ***"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."*** Tuinuke na kwa ujasiri tuzikabili changamoto za kizazi chetu. Kwa ujasiri tuanze kutenda tulichopaswa kukitenda hapo awali. Tuwe kweli waume na wake wa Imani. Tunamudu kutokuwa na mapungufu.

# MZIZI WA DHAMBI

Bonnie Rushmore

Je! Inaweza kusemwa kwamba kuweka matakwa na matamanio yetu juu ya matakwa ya wengine ni mzizi wa dhambi zote? Kwa kuwa dhambi ni somo la kibiblia, tutatazama vifungu vichache kutoka kwenye biblia kufikia majibu yaliyothibitishwa na Mungu kwa maswali haya.

Kwanza, tunatakiwa kufafanua dhambi. Dhambi ni uvunjaji wa sheria za Mungu (1 Yohana 3:4). Tunatenda dhambi tunaposhindwa kutimiza lolote kati ya amri zote za Mungu. Mtu anaweza kutenda dhambi kwa kuwaza (Mathayo 5:22, 28; 1Yohana 3:15), kwa matendo (Warumi 2:32) na kwa maneno (Wakolosai 3:8-9). Dhambi zote zinaangukia katika vipengele hivi vitatu kwenye maisha yetu. Mtume Yohana alisema, ***"maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia"*** (1 Yohana 2:16). Dhambi zote ni matokeo ya dunia na haiwezi kuhusishwa na Baba yetu wa Mbinguni.

Vifungu vingi kwenye Agano Jipya vimeorodhesha dhambi ambazo mtu anaweza akajihusisha. Hivi vifungu vimeainisha aina za tabia ambazo hazikubaliki na Mungu (Warumi 1:29-32; 1 Wakorintho 5:11; Wagalatia 5:19-21: 2 Timotheo 3:2-4; Ufunuo 21:8).

# KWA NINI LISIWE KANISA LA CHAGUO LA BWANA?

**Maxie B. Boren**

Kwa jinsi ninavyokumbuka, nimewahi kusikia msemo "Jiunge na kanisa la chaguo lako" huu ni mtazamo wa kimadhehebu ya "Kikristo." Wazo ya kuwa kuna makanisa mengi, yote yakimpendeza Mungu. Kwa hiyo, jinsi nadharia hiyo inavyokwenda, watu wanaweza kuamua na kuchagua kanisa lipi la kujiunga. Mtazamo ni kama ule wa wanaohitimu shule wanapochagua vyuo vya chaguo lao.

Watu wengi tayari wanakubaliana na dhana hii katika dini kwa sababu haya ndiyo waliyoyasikia, na pia ndiyo waliyofundishwa kwa muda wote wa maisha yao. Watu wengi hawajui kuhusu kile Biblia inachofundisha kuhusu mada hii na awajali.

Ingawa sio wazingatiaji wa umuhimu wake, lakini watu wanahitaji sana kusikia ukweli! Ukweli ni kwamba Kristo ***"alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake"*** (Waefeso 5:25). Alilinunua kanisa kwa ***"damu yake ya thamani"*** (Matendo 20:28). Mungu alimfanya kuwa ***"Kichwa"*** cha kanisa na katika hilo awe na ***"ukuu wote"*** (Waefeso 1:20-23; Wakolosai 1:18).

Wakati wa Huduma yake binafsi, Yesu alitamka wazi kuwa "atalijenga" kanisa lake (Mathayo 16:18). Ni dhahiri, Bwana alizungumzia **jengo la kiroho**, sio la kimwili, kwa sababu Biblia inazungumza kuhusu **"mawe yaliyo hai"** yaliyopangwa pamoja kama hekalu la kiroho la Mungu. Soma na zingatia vifungu kama 1 Petro 2:5; Waefeso 2:19-22; 1 Wakorintho 3:16-17 na 1 Timotheo 3:16, 17, na 1 Timotheo 3:15. Haya ***"mawe yaliyo hai***" ni watu waliosikia, wakaamini na kutii Injili ya Kristo, ambayo ni nguvu ya Mungu kuokoa (Warumi 1:16). Utii kwa Injili ni kunyenyekea katika amri zilizowekwa wazi kwenye ujumbe kwa wanaoiamini Biblia. Waamini ni lazima watubu, wakiri Imani katika Kristo na kubatizwa ili kuingia ndani ya Kristo na dhambi zao kuoshwa kupitia damu yake. Soma vifungu vifuatavyo kama Marko 16:15-16, Matendo 2:37-38, Matendo 3:19; 17;30; 8:12, 35-39; 10:48; 22:16, 1 Yohana 4:15, Warumi 10:9-10, Wagalatia 3:26-27 na Warumi 6:17-18, 3-9. Hao waamini waaminifu wanazidishwa katika kanisa la Bwana (Matendo

2:47), na kwamba, kanisa ni mwili wa kiroho wa waliookolewa (Waefeso 5:23), mwili wa upatanisho (Waefeso 2:16), ufalme wa kiroho wa Mkombozi (Wakolosai 1:13-14, 18, 24). Kwa taswira nyingine ya kanisa la Biblia imeweka wazi kuwa ni ***"bibi harusi wa Kristo"*** soma Waefeso 5:22-32 na 2 Wakorintho 11:2. Kwa kuwa ***"kila andiko,*** [lina] ***lenye pumzi ya Mungu,"*** (2 Timotheo 3:16; 2 Petro 1:21), je, kuna mtu yeyote anayeweza kuelezea kwa nini Roho Mtakatifu amefafanua sana kuhusu kanisa kama alikuwa hataki sisi tupokee na kutambua uhakika uliotolewa? Yesu Kristo alimchagua bibi harusi wake! Si yeyote tu angefanya! Hilo liko wazi hata mtoto anapaswa kuwa na uwezo wa kuelewa.

Tunaweza kutarajia ulimwengu wa kimadhehebu kujaribu kutetea mtazamo wake wa **makanisa mengi, na kila moja ni zuri**. Jitihada zao ni dhaifu, kwani dhana hiyo ni ya uwongo mtupu! Ukaidi huondoka kutoka katika kile kilichoandikwa (1 Wakorintho 4:6), hata hivyo, utetezi huo pia ilitokea zamani. Wazee wa Efeso walipokea onyo kama hilo ***"tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao"*** (Matendo 20:30). Hili ndilo hasa linalotokea kati yetu leo!

Ni muhimu sana na ni jambo la dharura kwamba turudi kwenye misingi. Tunatakiwa kuhubiri na kufundisha kuhusu **kanisa la chaguo la Bwana.**

**Je! Ulijua?** Mto Yordani una urefu wa maili 200 kuanzia chanzo chake Palestina ya Kaskazini na unapoishia kwenye bahari mfu. Inadondosha wastani wa futi 22 kwa maili na unahudumia sehemu ndogo ya maji duniani?



# Tafuta Katika Biblia

**Martha Rushmore**

1. Nani aliyemwacha Paulo na Barnaba katika safari hii ya umisheni? (Matendo 13:13)
2. Paulo aliitwa jina la mungu gani? (Matendo 14:12)
3. Paulo na Barnaba wakawakung'utia__________ya miguu yao. (Matendo 13:14-51)
4. Ni katika mji gani Paulo alimponya mtu kiwete? (Matendo 14:8-10)
5. Yohana Marko aliuendea mji gani? (Matendo 13:13)
6. __________mshirika wa Paulo. (Matendo 13:2)
7. Ni nani aliyewatuma waende safari hii ya umisheni? (Matendo 13:4)
8. Paulo na Barnaba waliwafungulia akina nani mlango wa imani (Matendo 14:27)
9. Ni mji gani wa Kirumi waliofikia baada ya kupita Pisidia (Matendo 14:24)
10. Paulo jina lake lingine aliitwa nani? (Matendo 13:9)
11. Barnaba aliitwa jina la mungu gani? (Matendo 14:12)
12. Mji waliotokea uliitwaje? (Matendo 13:1)
13. Ni mji gani aliouendea Paulo baada ya kupigwa kwa mawe? (Matendo 14:20)
14. Elima alikuwa nani? (Matendo 13:8)

# Msaada katika Udhaifu Wetu

Wayne Barrier

Wakristo wa karne ya kwanza walifundishwa kwamba watateseka (Warumi 8:17-18; 1 Petro 4:12-13; Yakobo 1:2-3) na kwamba Mungu anafahamu mapambano yetu. Majaribu na dhiki zinaweza pia kutokea kipindi cha kutafuta maendeleo, na zinaweza kuwa baraka kwa mtu anayevumilia kwa uaminifu. Kila siku tunaona mateso na shida; lakini maisha yanaweza kuwa magumu sana, na ndugu (Wakristo) hatupaswi kuwaza na kuufikiria huo ugumu.

Fikiria ahadi nyingi za Mungu kwetu hasa katika kitabu cha Warumi 8:26-39. Kwanza, Paulo aliandika katika Warumi 8:26-28,

> ***Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu. Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.***

Ahadi hizi zinazidi kusisitizwa zaidi tunapoendelea kusoma katika Warumi 8:31-35;

> ***Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye? Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya***

***hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea. Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?***

Tumeahidiwa ushindi katika nyakati hizi. Katika Warumi 8:37-39, Paulo alisema,

***Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.***

Msaada tunaouhitaji katika nyakati zetu za majanga na shida unapatikana na utatolewa, ikiwa ni waaminifu kwa Kristo. Ni baraka ilioje!

***Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, Kando ya maji ya utulivu huniongoza. Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji. Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika.***
***Hakika wema na fadhili zitanifuata Siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.***

**Zaburi 23:1-6**

# Fundisho la Kuishi Kwalo

# SOMO KUTOKA KATIKA YEREMIA SURA 37 – 39

David Conley

Mfalme wa Babeli, Nebukadreza (Ameandikwa pia, Nebukadneza katika Maandiko mengine) alikuwa akifanya mipango ya kushambulia Yerusalemu. Kwa kuwa Babeli lilikuwa taifa lenye nguvu ulimwenguni kwa wakati huo; suala hili liliwasumbua sana wakaaji wa Yerusalemu. Mfalme wa Yerusalemu wakati huo alikuwa Sedekia. Sedekia alikuwa amekosa kumtii Mungu sana. Mungu aliwatuma Wababeli kwenda Yerusalemu kama adhabu kwa sababu ya kutotii kwake.

(Picha)

Sedekia alipata wasiwasi sana baada ya taarifa za siri na kijasusi alizozipata. Taifa la Babeli lilikuwa likijitayarisha kwa mashambulizi makubwa dhidi ya mji wake. Alifanya jambo la hekima zaidi aliloweza kufanya kwa kumwita Yeremia na kumwomba aombe kwa Mungu kwa ajili ya nchi. Hii ilikuwa hatua ya busara sana! Kwa kawaida kwenye hali kama hii watu wangewaita majenerali na wakuu wa vita kuwauliza mpango wa vita!

Lakini Kwa bahati mbaya, Yeremia alikuwa na habari mbaya kwa Sedekia. Mungu alikusudia Wababeli waiadhibu Yerusalemu kwa ajili ya dhambi zake. Jibu la Mungu kwa sala za Yeremia lilikuwa kujisalimisha kwa Wababeli! Sedekia alikuwa amepata jibu la swali lake, lakini halikuwa jibu alilolitaka! Kwa kuwa halikuwa jibu alilolitarajia, je; anapaswa kutii?

Badala ya kumtii Bwana (jambo ambalo hakuwa analifanya), alimhukumu Yeremia kutupwa gerezani, shimoni na majeshi ya mji huo. Baada ya Yeremia kukaa gerezani kwa muda mrefu, Sedekia akamwita na kumwuliza tena, ***"Je, kuna neno lo lote kutoka kwa BWANA? Yeremia akasema, lipo, kwa maana, utatiwa mkononi mwa***

***mfalme wa Babeli."*** Yeremia alimwambia ukweli kwa mara nyingine tena. Sedekia alimtendea Yeremia wema kidogo kwa muda mfupi, lakini baadaye akawaruhusu wanajeshi wake wamtie ndani ya shimo lingine ambamo Yeremia alizama kwenye tope zito!

Yeremia alikuwa karibu kufa mahali hapa palikuwa pabaya sana, kuna wakati mmoja matowashi wa Sedekia walimwomba Sedekia amtoe Yeremia huko. Sedekia, kwa mara nyingine tena, alimtoa Yeremia kutoka gerezani na kumwuliza kama kuna neno kutoka kwa Mungu. Yeremia alimwambia tena kwamba ikiwa angekataa kujisalimisha kwa Wababeli angeadhibiwa, na taifa hilo lingeteketea kwa moto!

Sedekia hakutii. Nebukadreza alishambulia taifa hilo, akawaua watoto wa Sedekia mbele ya macho yake kisha akamtoa macho! Ndipo mji ukachomwa moto, kama vile tu Mungu alivyosema!

Je, tunamtii Mungu pale inapotufaa tu? Je, umepokea jibu la maombi yako lakini hutaki kutii? Je, hatupaswi kumtii Mungu katika mambo yote?

## SARAFU ZA KENNY

"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tulikuwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki, ambayo kwa kupigwa kwake tuliponywa" (1 Petro 2:24). Umewahi kuona mtu mwenye tabia isiyostahili na ukajisemea, "Anastahili kupigwa?" Kweli, Yesu alichukua kipigo ambacho sisi sote tulistahili ili tuachwe huru, tupone na tusamehewe makosa yetu kwa Mungu

# MAONI YA HARAKA KATIKA AYA MUHIMU

## (Wafilipi 3:20-21; Luka 24:39-43)

**Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake** (Wafilipi 3:20-21)

***Miili yetu itafananaje katika siku ya ufufuo?***

Kulingana na kifungu katika Wafilipi, miili yetu itakuwa kama mwili wa Kristo baada ya kufufuka kwake. Chambua kile kilichofunuliwa katika Andiko, ni baadhi ya ukweli upi tunaojifunza?

Mwili ulioonekana na mashahidi ni hakika ulikuwa ni mwili wa Kristo uliofufuka, Katika hali ya isiyoharibika; ***"Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo…Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, Mna chakula cho chote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. Akakitwaa, akala mbele yao"*** (Luka 24:39, 41-43). Kama tu ilivyokuwa kweli pale watu watatu walipomjia Ibrahimu katika Mwanzo 18, ambao walikula chakula walichoandaliwa, Bwana wetu katika mwili wake ulibadilika aliweza kula chakula cha kimwili. Hii haithibitishi kwamba chakula kitahitajika katika dunia mpya, bali inaonesha kwamba mwili wa kiroho unaweza kufanya mambo ya kimwili inapohitajika.


Hata hivyo, bado kulikuwa na utofauti na mwili wa kawaida wa kibinadamu: ***"Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu."*** Katika mwili huu ulibadilika, aliweza kuonekana na kutoweka, hakulazimika kupitia mlangoni.

Wakati inapoonekana malaika – viumbe wa kiroho, sio binadamu waliofufuka, wanaweza kuvaa mwili wowote unaohitajika kwa kazi maalum waliyotumwa, watu waliofufuka wataishi katika miili yao wenyewe, ikiletwa kutoka katika umauti na kubadilishwa kuwa isiyoharibika, kama ule wa Bwana wetu, usiokufa tena.

# Ukristo wa Karne ya 1 Katika Ulimwengu wa Karne ya 21

**Derek Broome**

Nimekulia katika dunia ambayo teknolojia ni kawaida. Tangu wakati nilipozaliwa mpaka siku hii, kamwe sijawahi kuona muda pasipo teknolojia. Sasa, hilo halimaanishi kwamba wazazi wangu hawakunisisitiza nitoke nje. Kwa kweli, katika siku nyingi za kiangazi nilikuwa nje nikifanya kazi, nikikimbia na kucheza mpira. Hata hivyo, bado hadithi ambazo mtu anaweza kusikia kuhusu wakati ambao kabla teknolojia haijatawala ulimwengu, hizo hazikuwa ni simulizi zangu bali nilisimuliwa na watu walioishi katika wakati tofauti na mimi. Zilitoka kwa watu waliopitia maisha tofauti kuliko niliyopitia na pengine sitapitia kabisa.



Ikiwa unapaswa kumchukua mtu aliyeishi miaka mia moja iliyopita na

kumlinganisha na mtu anayeishii leo, basi ungeweza kuona tofauti kubwa katika maisha yao. Mapinduzi ya viwanda, mitambo, madawa na teknolojia yamekuwa ni ya kushangaza. Katika namna nyingi, mapinduzi ya wakati wa sasa, yamebadilisha ulimwengu mzima. Pamoja na hayo, je, kuna upande dhaifu wa teknolojia?

Ulimwengu wetu umekuwa pamoja kuliko wakati mwingine wowote. Simu, intaneti, mitandao ya kijamii, vyombo vya habari, ndege na magari yameboreshwa sana kiasi kwamba chochote mtu anachotaka kufanya sehemu yoyote anaweza kufika kwa haraka. Baada ya kusema haya yote na ni kweli, lakini bado nina swali. Pamoja na muunganiko wote, kwa nini sisi kama watu wanaoishi katika utamaduni wetu wa sasa hatujaunganika? Je, sisi kama Wakristo tunatumia rasilimali iliyopo katika vidole vyetu kwa ajili ya utukufu wa Mungu?

Jaribu kufikiri kwamba wewe ni Mkristo anayeishi katika karne ya kwanza, na mtu kutoka karne ya sasa amekupa nyenzo zote tulizonazo leo. Unadhani ni nini ambacho kingefanikishwa kupitia nyenzo hizo? Haipaswi tena kuchukua siku nyingi kufika popote pale kwa sababu ndege na magari zingeweza kueneza Neno katika ulimwengu kwa haraka na kwa wakati muafaka. Madawa ya kisasa yangeweza kukufanya uishi muda mrefu na kutumia muda zaidi kuhubiri. Kompyuta, simu na vifaa vingine vingekufanya uwasiliane na mamia ya watu kwa umbali wa maili nyingi. Kufuatilia hali za Wakristo wenzako na makusanyiko kungeweza kufanikishwa kwa kubofya kitufe tu.

Unafikiri ni nini ambacho kingefanikishwa kama kungekuwa na Mkristo wa karne ya kwanza anaishi katika ulimwengu wa karne ya 21? Jibu la swali hilo linatakiwa kujibiwa na maisha yetu. Sisi ni Wakristo kama watu wale katika karne ya kwanza. Tumepewa wajibu uleule wa kueneza Neno la Mungu ulimwenguni. Je, tunalieneza Neno kama tunavyopaswa? Je, tunatumia nyenzo tulizonazo? Na tuweke mpango leo hii wa kumwambia mtu fulani kuhusu Kristo. ***“Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana; enendeni kama watoto wa nuru”*** (Waefeso 5:8).

# Paulo Alifanya Nini Huko Arabuni?

Kevin L. Moore



Baada ya kuongoka kwake na kuwa Mkristo, mtume Paulo alitumia miaka yake mitatu ya kwanza ya maisha yake ya Ukristo huko Shamu (Siria) katika mji wa Dameski na nchi iliyopakana ya Arabuni (Matendo 9:3-19; Wagalatia 1:15-18). Arabuni lilikuwa ni jina la Kirumi la Ufalme wa Nabatean, uliotawala kwa takribani miaka arobaini na nane (9 KK – 40 BK) na mfalme Areta IV, aliyetajwa katika 2 Wakorintho 11:32. Katika kipindi cha Kati cha Nabatean (30 KK – 70 BK), mipaka yake ilibadilika lakini ilijumuisha kile ambacho leo inajulikana kama Sinai, Negev, upande wa mashariki wa Bonde Yordani, sehemu kubwa

ya Yordani na sehemu ya Saudi Arabia. Wakati fulani uliungana na miji ya Dekapoli na Dameski, na huenda Paulo hakusafiri mbali kutoka Dameski wakati alipokuwa Arabuni.

Mtume alikuwa Dameski angalau mara mbili: (a) alipoongoka na kuwa Mkristo (Matendo 9:8-19) na (b) aliporejea kutoka Arabuni (Wagalatia 1:15-17). Kuondoka kwake kwa awali kulichochewa na njama ya Wayahudi kutaka kumwua (Matendo 9:23-25), na kuondoka kwake kwa mara ya pili kulichochewa na liwali wa Dameski aliyetamani kumkamata (2 Wakorintho 11:32-33). Katika matukio yote mawili Paulo alitoroka kwa kushushwa chini kwa kikapu kupitia ukuta wa mji.

Iwe mtume (kama Mkristo kijana) alienda Arabuni kwa ajili ya kujitenga na kubadilika au kama mmisionari, taarifa za kibiblia hazisemi, wala hazioneshi kwa kiasi gani kwa miaka mitatu alipokuwa pale. Hata hivyo, kwa mtazamo kumhubiri kwake Kristo mara tu baada kuongoka kwake (Matendo 9:20-22) kuliamsha chuki ya mfalme wa Nabatean (2 Wakorintho 11:32).

Akiwa Arabuni, Paulo huenda hakuwa mwanafunzi pekee wa Yesu huko. Inaonekana Waarabu wa Kiyahudi walikuwepo Yerusalemu katika siku ya Pentekoste wakati maelfu walipoongolewa kwa Kristo (Matendo 2:11, 41) na baadaye wakatawanyika katika nchi nyingine (Matendo 8:4; 11:19), bila shaka inawezekana kwamba kulikuwa na Wakristo washirika huko Arabuni ambao mtume alifanya nao kazi.

Chochote Paulo alichokifanya huko Arabuni, pasi na shaka alikuwa akijiandaa kwa huduma ya maisha kama balozi wa Kristo kwa ulimwengu wa kipagani. Wakati maelezo hayajatolewa bado, tunajua asili ya imani baada ya hapo awali kukutana na Bwana huko Dameski. ***"Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote*** [mitume wengine]***; wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami"*** (1 Wakorintho 15:10).

# JUHUDI KWA AJILI YA MUNGU LAKINI SI KATIKA MAARIFA

**Sunny David**

Akithibitisha shauku yake na kuwajali watu wake wa Kiyahudi, mtume Paulo aliandika waraka wake kwa Warumi kwamba tamaa ya moyo wake na maombi yake kwa Mungu yalikuwa kwamba waweze kuokolewa, lakini baadaye alisema, ***"Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa"*** (Warumi 10:2). Kwa dhamiri hawakuwa waasi kwa Mungu; kwa kweli, walionesha dhahiri bidii yao kwa Mungu katika kuiendea haki ambayo waliamini kuwa itawajia kwa kutii sheria ya Musa (Warumi 9:31-32). Pamoja na hayo, hawakuwa wamefunuliwa kuhusu haki ambayo Mungu huwapa wote ambao wataikubali kwa njia ya imani (Warumi 4:16), hata haki ambayo kwa njia ya imani ya Kristo (Wafilipi 3:9). Ilikuwa ni ujinga wao kwamba haki ambayo huja kutoka kwa Mungu ambayo iliwachochea kuendelea katika juhudi zao za bure ili kupata haki yao wenyewe kupitia dini yao wenyewe, na matendo mema. Hawakuwa wakipinga mapenzi ya Mungu kwa kujua; ni kwamba tu hawakuwa wakielewa mapenzi ya kweli ya Mungu yalikuwa kitu gani. Wakati ikielezwa kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini, juhudi bila ya maarifa ni hatari. Ni kama mtu fulani anayetaka kuendesha ndege bila ya kuwa na maarifa yoyote ya kuendesha ndege. Hilo litawaangamiza wote, ndege na rubani. Kuna jambo kama upofu hivi, linaloongoza vibaya juhudi hiyo.

Katika ulimwengu wa kidini leo hii, kuna jambo kubwa linalosemwa kuhusu Roho Mtakatifu, hususani kuhusiana na hisia wengi wamehusisha na kuongozwa na Roho Mtakatifu katika maisha yao. Watu wengi leo wanaamini kuwa Roho Mtakatifu anatenda kazi leo hii vilevile kama alivyotenda wakati ambapo Maandiko yalikuwa

yakiandikwa moja kwa moja na kwa miujiza. Dhana hii ambayo wengi wanayo leo hii kuhusiana na Roho Mtakatifu inawafanya kuwa na shauku kubwa na bidii. Bila shaka, hili ndilo jibu lao linaloegemea katika hisia zao kuliko katika ufunuo wa Mungu; bidii yao ni bila ya maarifa ya ufunuo ulioandikwa wa Roho Mtakatifu, ambao ni dhahiri katika mahubiri yao yanayokinzana, na mafundisho tata ambayo yamezaa machafuko ya kidini na migawanyiko. Wote wanadai kuongozwa na Roho wa Mungu, lakini wanaamini na kufundisha tofauti. Hawana msimamo wala muunganiko na kile Roho anachokifundisha kupitia Maandiko. Je! Mungu ndiye mwanzilishi wa machafuko (1 Wakorintho 14:33)?

Hoja ni kwamba udhihirisho wa miujiza ya Roho Mtakatifu haupatikani tena kwa mtu yeyote leo hii. Roho Mtakatifu leo anatenda kazi kupitia ufunuo wa Neno la Mungu lililoandikwa, Biblia, na sio moja kwa moja au tofauti na Neno lililoandikwa. ***"Kila Andiko,"*** inasema 2 Timotheo 3:16-17, ***"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."***

Kuna wakati katika historia ambapo wanadamu hawakuwa na Maandiko, maelekezo ya Mungu kwa mwanadamu, katika mtindo wa maandishi kama tulivyo na Biblia leo ambayo kupitia hiyo Mungu anazungumza na watu wote. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania aliandika, ***"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu"*** (Waebrania 1:1-2). Mwana, Kristo, wakati alipokuwa duniani, aliwachagua watu kumi na mbili wawe wasemaji wake. Aliwaahidi kwamba mara baada ya kurudi kwake kwa Baba, atawatumia Roho Mtakatifu ambaye atawaongoza katika kweli yote na kuwafundisha kweli yote. Zaidi sana, Roho Mtakatifu atawafundisha kila kitu ambacho Yesu alikuwa

amewafundisha wakati alipokuwa pamoja nao duniani (Yohana 14:25-26; 16:12-13).

Ahadi hii ilitimia katika siku ya Pentekoste ya Kiyahudi siku hamsini baada ya kufufuka kwa Kristo kutoka kwa wafu (Matendo 2:1-4). Mitume walipewa Roho Mtakatifu ili kuwawezesha kuzungumza lugha ambazo hawakuwahi kujifunza (Matendo 2:6-11), kuwapa nguvu za kutenda miujiza (Matendo 2:43), kulithibitisha Neno na kupata waumini (Marko 16:19-20). Huu ulikuwa ni wakati ambapo kabla Agano Jipya halijaletwa katika mtindo wa maandishi. Pindi lilipokamilika, hata hivyo, hakukuwa tena na haja yoyote ya matendo ya kimiujiza na ufunuo. Kwa hiyo, miujiza ilikoma. Hilo lilikusudiwa kutokea kulingana na 1 Wakorintho 13:8-10, pindi iliyokamili ingefika, hiyo ni, mapenzi kamili ya Mungu kama tulivyonayo leo katika Agano Jipya. Yakobo 1:25 anaeleza kuwa ni ***"sheria kamilifu ya uhuru."***

Kwa hiyo, sasa tunaishi katika wakati amababapo Mungu anazungumza nasi kupitia Mwanawe, Yesu Kristo kwa njia ya Agano lake Jipya (Mathayo 17:5; Waebrania 1:1). Kulingana na Warumi 10:17, ***"Imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo."*** Maagano yote mawili Agano la Kale na Agano Jipya yana mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa kwa ajili ya mwanadamu. Biblia yote iliandikwa kwa uvuvio wa Roho wa Mungu. ***"wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu"*** (2 Petro 1:21). Mungu aliitoa Sheria ya Agano la Kale kwa watu wake aliowachagua, Israeli, kupitia Musa, walioishi kabla ya kifo cha Kristo msalabani. Baada ya kifo chake, ufufuo na kupaa kwenda Mbinguni, Agano Jipya la Biblia liliandikwa, ambalo ni sheria ya Mungu kwetu ambayo tunaishi chini yake leo hii.

Kwa hakika hakuna mtu anayekana umuhimu wa juhudi katika maisha ya watoto wa Mungu. Ni ubora huu unaopaswa kutusukuma mbele tukiwa na nguvu kubwa na shauku ya kutenda mapenzi ya Mungu. Hata hivyo, haitoshi kwa sisi kujua kwamba tuna juhudi, bali kitu fulani ni lazima kizae bidii hiyo na kutia mafuta katika moto wa juhudi katika maisha yetu ya kila siku tukiwa na Mungu. Maarifa ya

Neno la Mungu, sio utendaji kazi wa moja kwa moja wa Roho Mtakatifu, yanapaswa kuzaa juhudi hii. Roho Mtakatifu anawaongoza wana wa Mungu leo hii kupitia Neno la Mungu lililoandikwa katika Biblia, sio tofauti, wala nje ya Neno lililoandikwa. Hivyo, ni muhimu sana watu wasome na kujifunze Biblia, watafakari na kujifunza kupata maarifa ya Neno la Mungu, mapenzi yake, na kuishi kwayo.

Kuna wengi ambao kwa bidii wanamhubiri Kristo leo hii na ambao wanadai kwamba Bwana anafanya miujiza kupitia wao. Wapo kwenye runinga, redio na katika makusanyiko makubwa ya watu kila mahali. Wana bidii na moyo wa dhati katika madai yao kama wale ambao Kristo aliwasema katika kifungu cha Mathayo 7:22-23 akisema, ***“Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.”*** Tatizo lilikuwa nini? Walifanya kila kitu kwa bidii bila ya kutambua mapenzi ya Mungu yalikuwa ni yapi.

Wengi kwa juhudi pasipo ubinafsi kwa bidii humtumikia Bwana, ili waje kumsikia Bwana akisema, katika Siku ile ya hukumu, ***“Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.”*** Uovu ni nini? Kile ambacho kinatendwa si kulingana na sheria, kwa suala hili, ni sheria ya Kristo, ambayo ni Agano Jipya. Onyo hili la Kristo linapaswa kumzuia mtu kwa ghafla mpaka pale atakapokuwa na uhakika wa uwongo ambao alidhani anatenda mapenzi ya Mungu. Ili kufanya mapenzi ya Mungu, ni lazima kwanza mtu ajifunze mapezi yake.

> Warumi 10:2 ***“Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa.”*** Mathayo 22:29 ***“Mwapotea kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu.”*** Hosea 4:6 ***“Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa.”*** Mathayo 15:14 ***“Waacheni hao; hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili.”***

# UNALETA NINI IBADANI?

Patrick Morrison

Agano la kale lilihitaji Wayahudi wote wakiume kwenda Yerusalemu mara tatu kwa mwaka kuabudu na kutoa sadaka, "***Mara tatu kwa mwaka na watokee wanaume wako wote mbele za BWANA, Mungu wako, mahali atakapochagua; katika sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu, na katika sikukuu ya majuma, na katika sikukuu ya vibanda; wala wasitokee mbele za BWANA mikono mitupu***" (Kum 16:16). Ilikuwa lazima kuwa wale waliokwenda Yerusalemu kumwabudu Mungu kutokwenda mbele zake mikono mitupu. Lakini sheria ya kale iliweka matoleo kwa wale ambao hawakuweza kutoa sadaka ya ndama au mwanakondoo kama ilivyokuwa desturi yao (LAW 5:7-11). Tangu watawala matajiri mpaka wale wa hali ya chini wote walipaswa kuja mbele za Mungu kwenye ibada wakiwa na kitu cha kumtolea. Hapo ndipo ulipo msingi halisi wa ibada yetu kwa Mungu. Ibada ni kitu tunachokitoa, kitu tunachokileta mbele za Mungu, na ikifanyika kama yalivyo mapenzi ya Uungu wake, tunatambua kuwa matoleo hayo yatapokelewa na yeye.

Wazo la ibada limepotea kwa wengi katika vizazi vyetu, kwa sababu mara nyingi ni muda wa kuburudishwa. Ibada imekuwa mchezo mwingine wa kushangiliwa, mahali pa kuonekana au kama kitu cha kukitimiza katika orodha ya matukio. Ni aibu kuona wale wanaokiri kuwa wanampenda Mungu wakija kuabudu pasipokuwa na kitu cha kutoa. Wengine hukaa kimya kama makaburi wakati sifa zinaimbwa kwa Baba yetu wa Mbinguni. **Mikono – mitupu!**Wengine hushikilia kwa bidii utajiri waliopewa na Mungu wakati wa kumrudishia unapofika kama yeye alivyotufanikisha. **Mikono – Mitupu**! Wengine wanapeana ujumbe, wanaongea, wanaota ndoto mchanawakati Neno la Mungu linasomwa au kuhubiriwa. **Mikono – mitupu**! Wengine huingia kushiriki mkate usiotiwa chachu, mzao wa mzabibu, wakidhani

wanatimiza meza ya Bwana, na kutoka wakipuuza mambo mengine ya ibada ya Mwenyezi Mungu. **Mikono – mitupu**! Wengine hutokea kwa nadra wakitarajia kila mmoja kuiona jitihada yao kwa kuwepo pale. **Mikono – mitupu**! Ndugu na marafiki, tunawezaje "***kutoa… kwa Bwana Mungu bila kutumia gharama yoyote***" (2 Samweli 24:22)?

Ibada si juu ya mwanadamu. Haijawahi kuwa juu ya mwanadamu. Kamwe haitakuwa juu ya mwanadamu. Ibada ni kupiga goti la kicho kwa Mungu na kuja mbele zake na kile tunachojua kitampendeza. Hatuthubutu kuja mikono – mitupu. "***bas kwa njia yake yeye na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake***" (Waebrania 13:15). "***Bali mimi, kwa wingi wa fadhili zako, nitaingia nyumbani mwako; na kusujudu kwa kicho, nikielekea hekalu lako takatifu***" (Zaburi 5:7), "***Mpeni BWANA utukufu wa jina lake; mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu***" (Zaburi 29:2). "***Njooni, tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele za BWANA aliyetuumba***". (Zaburi 95:6). "***Nitakutolea dhabihu ya kushukuru; na kulitangaza jina la BWANA***" (Zaburi 116:17). "***Nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu, nitalishukuru jina lako, kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa maana umeikuza ahadi yako, kuliko jina lako lote***" (Zaburi 138:2). "***Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo***" (1Petro 2:5). "***Shikeni yaliyo bora, asije akafanya hasira nanyi mkapotea njiani, kwa kuwa hasira yake itawaka upesi, heri wote wanaomkimbilia***" (Zaburi 2:12).

Ibada ya Mungu wa Mbinguni inadai kwamba twende mbele zake na kitu cha kumtolea, kitu ambacho wote tuna uwezo nacho: maombi yetu, sifa zetu, muda wetu, karama zetu, fedha zetu na nafsi zetu!



Mtu mmoja alikuwa ametoka kumaliza kusoma kitabu chake, *baba mwenye nyumba*, wakati amepanda usafiri wa kurudi nyumbani akitokea kazini.

Alipofika nyumbani, akamwendea moja kwa moja mkewe, huku akimnyooshea kidole usoni, akasema, "kuanzia sasa na kuendelea nataka ujue kwamba mimi ndio baba wa nyumba hii na maneno yangu ni sheria! Unatakiwa kuniandalia mlo mzuri usiku wa leo, na nitakapokuwa nimemaliza kula mlo wangu, ninatarajia kifuate kitindamlo cha gharama. Kisha, baada ya mlo wa usiku, utaniwekea maji ya kuoga ili nipumzike. Na nitakapokuwa nimemaliza kuoga, bashiri ni nani atakayenivalisha nguo na kuchana nywele zangu?"

Mkewe alijibu jibu kali, "Ubashiri wangu, ni mwosha maiti!"



Katika kampuni ya kupoza maji, nilijigamba juu ya ulimwengu wa safari za watoto wangu: kijana wangu mmoja alikuwa akifundisha huko Bolivia, mwingine alikuwa akifanya kazi Italia ya kusini na binti yangu alikuwa akihitimisha mwaka wa mwisho wa utafiti katika mradi wake huko India.

Mfanya kazi mwenzangu akanikatisha ghafla. "Vipi wewe?" Aliuliza, "hilo linawafanya watoto wako watake kuwa mbali na wewe!"



Mtoto mdogo kanisani kwa mara ya kwanza aliwaona watu wakipitisha sahani kwa ajili ya changizo.

Walipokaribia kwenye kiti alipokuwa amekaa, mtoto


akasema kwa sauti kubwa kiasi kwamba kila mtu aliweza kusikia: "Baba, mimi usinilipie. Umri wangu ni chini ya miaka mitano!"

Mwalimu mpya alikuwa anajaribu kuweka sawa somo lake la saikolojia. Alianza darasa lake kwa kusema, "Kila mmoja anayedhani kuwa yeye ni mjinga, asimame!" Baada ya sekunde chache, mtoto Larry alisimama. Mwalimu akasema, "Lary, unadhani wewe ni mjinga?" "Hapana mwalimu, lakini sipendi kukuona umesimama hapo peke yako tu!"

**Masomo 11 kutoka katika Safina ya Nuhu**

1. Usichelewe kuipanda safina.
2. Ni bora kumsikiliza Mungu kuliko wanadamu!
3. Weka mpango kabla. Wakati Nuhu alipokuwa anatengeneza safina mvua haikuwa inanyesha.
4. Kuwa imara. Utakapokuwa na umri wa miaka 600, mtu anaweza kukuomba ufanye jambo fulani kubwa sana.
5. Usiwasikilize wakosoaji; wewe endelea na kazi inayotakiwa kukamilika.
6. Yajenge maisha yako ya baadaye juu ya mlima.
7. Kwa ajili ya usalama, safiri mkiwa wawili wawili.
8. Kasi daima ina faida. Konokono walikuwa wameingia ndani pamoja na duma.
9. Unapokuwa na msongo, elea kwa muda.
10. Kumbuka, Safina ilitengenezwa na watu wasio na taaluma; Meli ya Titanic ilitengenezwa na wanataaluma.
11. Haijalishi kuna dhoruba, unapokuwa na Mungu, basi daima kutakuwa na upinde wa mvua ukisubiri.

Je! Uliwahi kujua kwamba ukimkonyeza mbwa usoni mwake anakukasirikia? Lakini ukimwingiza kwenye gari anatoa kichwa chake nje!"



# Je! Unapimaje?

**Nalimngoja Bwana kwa saburi, Akaniiinamia akakisikia kilio changu. Akanipandisha toka shimo la uharibifu, Toka udongo wa utelezi; Akaisimamisha miguu yangu mwambani, Akaziimarisha hatua zangu. Akatia wimbo mpya kinywani mwangu, Ndio sifa zake Mungu wetu. Wengi wataona na kuogopa, Nao watamtumaini Bwana Heri aliyemfanya Bwana kuwa tumaini lake, Wala hakuwaelekea wenye kiburi, Wala hao wanaogeukia uongo. Ee Bwana, Mungu wangu, umefanya kwa wingi Miujiza yako na mawazo yako kwetu; Hakuna awezaye kufananishwa nawe; Kama ningependa kuyatangaza na kuyahubiri, Ni mengi sana hayahesabiki. Nimehubiri habari za haki katika kusanyiko kubwa. Sikuizuia midomo yangu; Ee Bwana, unajua.**

**Zaburi 40:1-5, 9**

# Faida na Hasara

**J. RANDAL MATHENY**

Kipindi chote cha uhai huwa tunapoteza. Iwe ni katika mahusiano au wapendwa wetu, kazi au afya, mali au kutokuwa na hatia, ndoto au usalama, mara kwa mara huwa tunahisi vitu vya thamani kwetu kutoweka milele.

Kupitia vile tunavyopoteza, Mungu anataka kuimarisha mshikamano wetu na yeye. Kwa kupoteza vitu na watu katika maisha haya, tunaweza kujipatia thawabu katika ulimwengu wa roho. Thawabu hiyo haiji hivihivi. Mioyo yetu lazima iache kuupenda ulimwengu huu na kutamani na kuthamini mambo yajayo. Hasara inaweza kutufanya tukawa wakali au wenye majuto, kama tukichagua upande huo.

Kadiri tunavyozidi kusogea katika maisha (hali ya kuuelekea uzee), mkristo anapata zaidi: hekima, shauku kubwa ya kwenda Mbinguni, imani iliyo imara zaidi, utakatifu, upendo wa dhati kwa wengine, mzunguko mkubwa wa familia ya kiroho na kutembea karibu zaidi na Mungu, tukiyataja hayo kwa uchache. Kwa mtazamo huo, mtu anaweza kusema kwamba, kwa mkristo "***Kristo ni yote***" (Kolosai 3:11). Au kama alivyosema Daudi alipoelezea kupotea kwa ulinzi wake, "***sina wema ila utokao kwako***" (Zaburi 16:2).

Basi maswali ninayohitaji kujiuliza ni kama yafuatayo: Je, Mungu ananifundisha nini katika hasara hii? Nawezaje kuwa mwanafunzi mwema kwa sababu ya hasara hii? "Ni wapi nitakapoutambua ubinafsi wangu katika hisia zangu kuhusu hasara hii?" "Bwana yu wapi katika hasara hii?"

Judith Voirst aliyaita maisha kuwa ni mchakato wa "Hasara za lazima". Biblia inatuonyesha namna hasara hizo zinavyoweza kuwa faida za milele.Basi, alichosema Elifazi kitakuwa cha kweli kwetu sisi ambao "hatutaogopa hasara" (Ayubu 5:24).

# HAKUNA AWEZAYE KUUFUGA ULIMI…

**Alvin Jennings**

1. Kuongea sana juu ya nini "nafikiri" (Mihali 18:2).
2. Mtego wa nafsi yake wenye maneno yanayopingana (Mithali 18:7).
3. Umbea huzama ndani na huumiza mioyo (Mithali 18:8; 20:19; 25:9).
4. Kujibu kabla ya kusikiliza au kufikiri (Mithali 18:3, 17).
5. Kauli potofu hutengeneza mpumbavu (Mithali 19:1).
6. Kudanganya na kushindwa kutimiza ahadi (Mithali 19:9; 14:8; 20:25).
7. Mke mkorofi, mgomvi ni sawa na kutona-tona kwa mfereji (Mithali 19:3; 25:24; 27:15).
8. Kufanya mzaha na hekima (Mithali 19:25).
9. Mtu kujisifu (kujivuna) kuhusu matendo yake mwenyewe (Mithali 20:1; 27:2; Mhubiri 2:10-14; Yakobo 3:5).
10. Kuongea sana wakati unapotakiwa kusikiliza (Mithali 20:19; 10:19; Mhubiri 10:14)
11. Kutishia kulipiza ovu kwa ovu (Mithali 20:22).
12. Kulalamika, kunung'unika (Mithali 21:19, 19).
13. Mtu kumnenea mabaya baba au mama yake (Mithali 19:26).
14. Kujisifu mwenyewe (Mithali 25:27).
15. Kutoa jibu la kipumbavu (Mithali 26:4).
16. Kumdhalilisha jirani yako, na kusema nilikuwa nakutania (Mithali 26:18).
17. Sifa za uongo; kejeli (Mitahli 26:28).
18. Kujisifu juu ya utakachokamilisha kesho (Mithali 27:1).
19. Kumsalimia jirani kwa sauti kubwa asubuhi na mapema (Mithali 27:14)
20. Kashfa (Mithali 10:18)
21. Kulaani na kutaja jina la Mungu bure (Kutoka 20:9; 1Wafalme 18:20; Kumbukumbu la Torati 5; Yakobo 3:9-10).

22. Maneno ya kusifu (maneno yanayofanana na laana)."
23. Kukataa ukweli (Mathayo 26:34; Mithali 30:9; 1Timotheo 2:12).
24. Kufundisha na kuhubiri mafundisho ya uongo (2Petro 2:1).
25. Ulimi wa kuganda kwa maneno ya mzaha (Ayubu 30:1).
26. Kunong'ona; kusengenya (Mithali 16:28).
27. Kuzomewa (Yeremia 18:16; 51:37; Maombolezo 2:16).
28. Kukaa kimya unapotakiwa kusema ukweli (1Yohana 4:3).
29. Kushuhudia uongo; kuhukumu kwa uongo (Kutoka 20:16; Mathayo 19:18; Matendo 6:13).
30. Kushindwa kutunza siri (Mithali 11:13).
31. Maneno ya kukatisha tamaa (Hesabu 32:19; Kumb. 1:28).
32. Kubishana juu ya mambo yenye shaka (Warumi 14:1; Ayubu 6:25).
33. Mabishano ya kawaida yasiyo na msingi huchochea ugomvi (Mithali 6:14; Hesabu 32:19; Kumb. 1:28).
34. Kutenganisha kile ambacho Mungu amekiuanganisha katika ndoa (Mathayo 19:6).
35. Kutowaheshimu na kuwakemea watu wenye umri kubwa (Ayubu 15:10; 1Timotheo 5:1).
36. Kuwabagua maskini (Yakobo 2:3-4).
37. Kikashfu jina tukufu la Yesu (Yakobo 2:7-8).
38. Kuongea wakati uliopasa kusikiliza; ni vibaya (Ayubu 15:17; 16:1-2).
39. Kulaani wanadamu na kumbariki Mungu aliyewaumba (Yakobo 3:9).
40. Kuikana imani katika Kristo (Mathayo 10:32 – 33).
41. Kumwita mtu mpumbavu (Mathayo 5:22).
42. Kulitaja jina la Mungu bure; mfano "Mungu wangu" (Kutoka 20:7; Kumb. 5:11).
43. Kutokusema; "Mungu akipenda nitafanya hivi … (Yakobo 4:15).
44. Kushindwa kutimiza ahadi, viapo (Mhubiri 5:4; Hesabu 30:2-3; Ayubu 22:27).
45. Kuwakosoa matajiri (Mhubiri 10:20).
46. Kuvunja ahadi (Mithali 4:5-7).

# SHUKURUNI KWA KILA JAMBO

**Ramond Elliott**

Katika 1 Wathesolonike 5:18 mtume Paulo aliandika, "***Shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu***" Mhubiri kwa jina la Martin Rinkhard aliandika wimbo, "Sasa Sote Tunamshukuru Mungu Wetu" utumike kama kuonyesha shukrani na familia yake wakati wa chakula. Kwa hali isiyo ya kawaida asili ya wimbo huu wa sifa uliandikwa wakati Miaka Thelathini" wakati mhubiri akiendesha takriban misiba arubaini kwa siku, ukiwemo wa mke wake mwenyewe. Hata hivyo licha ya vita na mapigo, aliweza kutoa shukrani kwa Mungu kwa baraka zake. Aya ya kwanza ya wimbo wake ni kama ifuatavyo:

**"Sasa sote tunamshukuru Mungu wetu, Kwa moyo**
**na mikoni, na sauti, Aliyefanya vitu vya ajabu,**
**Ambaye katika yeye ulimwengu wake unafurahia;**
**Ambaye kupitia mikono ya mama yetu, Ametubariki,**
**kwa zawadi za upendo zisizohesabika, Na badoni wetu leo."**

Hadithi hii ya ukweli inanistajabisha lakini hainishangazi. Inaonyesha kuwa katika nyakati za hali mbaya na ngumu, watu wanaomwamini Mungu wanaweza kupata fursa ya kutoa shukrani mioyoni mwao.

Kinyume chake, taifa linabarikiwa sana kwa wingi wa nyenzo na vitu vya kimwili, kuna tabia ya mwanadamu kusahau chanzo cha baraka hizo. Mtu fulani ameeleza kwamba ukosefu wetu wa kutoa shukrani kwa Mungu kwa baraka tunazopata tutakuwa kama wanyama

wanaokula mahindi yaliyodondoka duniani bila hata kujua chanzo cha chakula chao. Somo liko dhahiri na linaeleweka. Mara nyingi watoto wa Mungu wana uwezo zaidi wa kufanya maombi, dua, maombezi kuliko kushukuru. Taifa ambalo linapobarikiwa sana kwa wingi wa nyenzo na vitu vya kimwili kuna uwezekano mkubwa wa kusahau chanzo cha baraka hizo. Mwandishi Yakobo alitangaza kuwa "***kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli chakugeuka-geuka***" (Yakobo 1:17). Mtunga Zaburi anatutia moyo katika jambo hilo kwa majibu yake akiwa mpokeaji wa baraka za Mungu, "***Nimrudishie BWANA nini kwa ukarimu wake wote alionitendea? Nitakipokea kikombe cha wokovu; Na kulitangaza jina la BWANA; Nitaziondoa nadhiri zangu kwa BWANA, Naam, mbele ya watu wake wote. …nitakutolea dhabihu ya kushukuru; Na kulitangaza jina la BWANA***; (Zaburi 116:12-14, 17).

Watoto wa Baba wa Mbinguni inawapasa kukumbuka kila siku baraka zinazomiminika kutoka kwenye mkono wake uliojaa neema. Hasa kuwe na ufahamu wa "***baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo***" (Waefeso 1:3). Kila siku ni siku ya shukrani kwa waliokombolewa. Tusisahau kamwe dhabihu zilizotolewa na baba zetu na wapendwa wetu ili kutuhakikishia uhuru tunaoufurahia sasa. "***Na wamshukuru BWANA kwa fadhili zake, Na maajabu yake kwa wanadamu***!" (Zaburi 107:8). "***Tuje mbele zake kwa shukrani, tumfanyie shangwe kwa Zaburi***" (Zaburi 95:2).

**"Msifuni Mungu, kwa baraka zinazomiminika**
**kutoka kwake; Msifuni yeye, viumbe vyote hapa chini;**
**Msifuni yeye aliye mwenyeji wa Mbinguni;**
**Msifuni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu;"**

# ULINZI WA WAZAZI WACHAMUNGU

DARRELL SURRETT

Kuna wakati fulani, kila mtu anafanya maamuzi ambayo yako nje ya mapenzi ya Mungu na nia kwa watoto wake. Hivyo tunamhitaji Yesu kwa ajili ya msamaha kwetu, na watoto wetu hawako tofauti. Mambo wanayoyapitia huzaa matunda yaliyoghoshiwa na matokeo ya maamuzi waliyoyafanya. Maamuzi haya wakati mwingine yanaweza kutuletea maumivu sana sisi kama wazazi tunapoyachunguza. Tunaona mambo zaidi ya yalemaumivu wanayoyapata watoto wetu. Pia tunachunguza dalili, miundona mienendo ambayo inaweza kufichua matatizo ya ziada ya msingi.

Kwa Haruni, maadhimisho haya bila shaka yalikuwa magumu na yenye maumivu sana. Katika Hesabu 10:1-3 Nadabu na Abihu walifanya maamuzi yaliyowagharimu maisha yao. Si kwamba Haruni alipoteza watoto wake wawili tu, bali pia hasara ilitokana na dhambi iliyotangazwa hadharani. Je, wewe kama mzazi unawezaje kupokea maagizo ya Mungu baada ya tukio kama hilo? Haruni alinyamaza katika hukumu ya Mungu kwa watoto wake. Aliumia sana, lakini alibaki mtiifu. Ni rahisi kwa wazazi kuwatetea watoto wao mara moja, kinyume na kutoa hukumu ya haki na isiyo na upendeleo. Nakosa maneno ya kutosha kukuonya jinsi hii inavyoweza kuwa hatari. ***"Mrudi mwanao, kwa maana liko tumaini, wala usiikaze nafsi yako kwa kuangamia kwake***" (Mithali 19:18).

Wazazi wengi wanapenda watoto wao wafanye mema, lakini badala kuruhusu nidhamu ichukue nafasi ilikuyafikia matokeo hayo, mara nyingi wanafanya majadiliano katika kujaribu kuwasamehe. Matokeo yake nikwamba watakuwa ni watoto ambao watafanya maamuzi yale yale ya kuwagharimu ya kutokutii kama Nadabu na

Abihu. Hata hivyo, ni wazazi wachache wanaotaka kuhubiriwa kuhusu jinsi ya "***kumlea mtoto katika njia impasayo***" (Mithali 22:6).

Watoto wako wanaweza kuona maelekezozo yako kama hayana maana, na yana maana basi ni maagizo dhaifu, na huenda yamepitwa na wakati. Wanaweza wakawa na haraka ya kukatisha maonyo yako na, "najua Baba", kwa kujaribu kuzuia mjadala wa kina wa nia zao, au kufanya haraka ili kurudi kwenye jambo walilokuwa wanalifafanya. Kibaya zaidi, wanaweza kukupotosha kwamakusudi ya ubinafsi na dhambi. Hatuwezi kuwa wajinga, na wao hawawezi kutufanya tuwe hivyo!

Hatuwezi kuwaona watoto wetu kila wanapokwenda, kuwafanyia maamuzi yao au kuwalinda masaa ishirini na nne kwa siku. Utafika wakati ambapo hawatalindwa na uangalizi wetu wa moja kwa moja au kuhifadhiwa na nyumba zetu, na hawatakuwepo kwa ajili ya sala kuzunguka meza yetu ya chakula cha jioni. Kwa hiyo tunafanyeje? Nadhani unaweza kuwa na turubai lililopakwa ya Mhubiri 12:1 juu yake, inayosema, "***Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja siku zilizo mbaya, wala haijakaribia miaka utakaposema, mimi sina furaha katika hiyo***" na uwape waende nalo wanapotoka kwenda chuoni, lakini kuna kitu kinaniambia linaweza lisifike kwenye ukuta wa chumba cha kulala. Nalijua hili; Ingawa tunaweza tusiwe na udhibiti juu ya maamuzi wanayofanya watoto wetu, siku kwa siku, Mungu ametupa nguvu kuu ya kuwalinda, kuwafundisha, kuwaandaa na kuwakinga.***Ushawishi!*** Ushawishi unaoungwa mkono kwa miaka (pengine miongo) ya kimungu, uzoefu wa uzazi na maarifa. Una uthibitisho wa upendo wako kwa mtoto wako kwa kumbukumbu zinazoonekana. Usiogope kuwakumbusha. Una ushuhuda wako unaoonyesha namna Mungu alivyojidhihirisha kuwa mwenye rehema nyingi kwako na kuwa ni mwenye kuweza kuchukuliana na udhaifu wako. Mkumbushe mtoto wako mambo haya. Unalo sikio la mototo wako! Inawezekana kuyatia nguvu maneno yakomapenzi magumu (ukiondoa funguo, kuziondoa kimwili kutoka kwenye mazingira ya dhambi, kukataa pesa, n.k), na ni lazima ushinde

majaribu ya kufanya mwanga wa kuangazia dhambi zao, ili kwamba usifanyike kuwa mtu wa kwanza kuziwezesha hizo dhambi! Pale wazazi wanapoenda zaidi ya sehemu wanayopaswa kuishia katika malezi yao – kuwa wagumu sana wepesi sana – hatimaye watoto wao hulipa gharama. Usiwe na hatia juu ya mambo ya mambo hayo.

Kuna wakati mtu mmoja aliniambia katika miaka yangu ya mwanzo kama kiongozi katika jeshi, "Hakuna haja ya kukasirishwa na maamuzi ambayo askari wako waliyafanya au kupaza sauti yako. Waambie ni nini unataka kifanyike, halafu waache wafanye maamuzi yao. Matokeo ni ya kwao wenyewe, haijalishi". Wazazi ambao humtumikia Mungu aliye hai wanajaribu kuwasaidia watoto wao kuepuka matokeo mabaya ya milele na, hatimaye, kuwasogeza karibu na Mungu. Hata hivyo, kutoa maelekezo kwa sauti kali, na mafundisho vurugu hakupelekei matokeo yanayotamaniwa. Waelekeze watoto wako kuishi kama Mungu anavyoonyesha, wape rasilimali zitakazowawezesha kufanya hivyo (pamoja na mfano), na umwombe Baba.

Neno la Mungu hutuonya tusiwachokoze watoto wetu, "***wasije wakakata ama***" (Wakolosai 3:21, Waefeso 6:4). Unapaswa kuwa mtu ambaye watataka kukujia pale ambapo wengine na ulimwengu pia ukiwashusha. Wanapokujia, unaweza kuwaelekeza kwa Mungu mmoja wa kweli aliye mbinguni ambaye amekupitisha kwenye magumu yako yote.

Natamani daima ningekuwepo karibu kuondoa maamuzi yoyote mabaya ambayo mwanangu huyafanya, lakini ukweli ni kwamba, siwezi. Kama Haruni, tunaweza kujikuta tuko kimya mbele za Mungu kwa muda. Hatuna nguvu juu ya maamuzi yao, ila tuna kiwango kikubwa kizuri cha ushawishi, kwa maneno yetu, kwa kuwa vielelezo sisi wenyewe na kwa ujumla wa maisha yetu. Usiogope kuutumia ushawishi. Mungu alikupa huokwa sababu hii, kwa ajili ya mwongozo ao na hatimaye wokovu (Kum. 6:4-9).

# KUZIJENGA NDOA NZURI

**Dan R. Owen**

Kinachofuatia kwenye Kanisa ambalo Yesu alilifiani ndoa. Ndoa ni taasisi takatifu sana. Ndoa ni sehemu ya mpango wa Mungu kwa jamii ya wanadamu na ni ya muda mrefu kama ulivyo uumbaji. Ni tofali la msingi kwa ujenzi wa jamii ya wanadamu kama Mungu alivyoipanga. Hivyo, inabakia kuonyesha umuhimu kwamba Kanisa linapaswa kuweka jitihada nyingi katika kuwasaidia watu kujenga ndoa nzuri. Kujenga ndoa nzuri kunahitaji mambo kadhaa ambayo ni ufunguo. Zingatia haya:

**Kwanza, kuzijenga ndoa nzuri hugharimu ahadi ya agano.** Kupitia Malaki, Mungu aliwaambia watu wake kwamba yeye ni sehemu ya muunganiko wa ndoa na kwamba ndoa ni agano takatifu.Ahadi ya agano ni ahadi inayojitokeza kutokana na msukumo wa maadili ya watu wanaohusika. Kwa kuwa ahadi ya kweli hujitokeza kutoka kwa Mungu,kuingia katika agano la ndoa kupo katika msingi wa mahusiano na Mungu. Watu wenye ahadi ya namna hii hufanya kile kinachogharimu kuijenga ndoa nzuri kwa kuwa ni mapenzi ya Mungu, na kunafanya yawepo mahusiano na Mungu. Kwa kuwa ahadi katika ndoa husaidia wokovu wa roho zetu, basi ni jambo linalopaswa kuzingatiwa sana na ni maamuzi ya mtu binafsi. Ahadi ya agano ni msingi wa ndoa nzuri.

**Jambo linalofuata, kuijenga ndoa nzuri hugharimu upendo.** Mtu haangukii tu katika upendo wa jinsi hii. Mtu anakuwa na upendo wa aina hii kwa kuchagua. Upendo wa jinsi hii unaweza kutolewa hata pale ambapo hakuna upendo uliopokelewa. Upnedo huu nivitendo na hautegemei namna mtu anavyojisikia katika siku fulani. Upendo huu hufuatisha upendo wa Kristo aliyetupenda kwanza tukiwa wenye

dhambi. Upendo wa aina hii ni uvumilivu na kusamehe. Upendo huu hujitokeza kutokana na ahadi ya agano. Ni uchaguziwa kutafuta mambo mazuri na yaliyo bora kwa ajili ya mwingine katika maisha.

**Kuijenga ndoa nzuri hugharimu jitihada za makusudi.** Ili kuwa na ndoa nzuri, watu ni lazima wajitahidi kuwa na mawasiliano mazuri, wakijifunza kuelezea hisia zao na kuwa wasikilizaji wazuri. Kuwa na ndoa nzuri, wanandoa wanapaswa kuzingatia historia ya uzoefu wa pamoja ambayo itawapa msingi wa pamoja. Wanandoa ambao wanafanya mambo pamoja, wanafanya miradi pamoja na kwenda sehemu mbalimbali pamoja hupita kwenye njia moja katika maisha. Pia wanandoawanapaswa kuzingatia maridhishano katika tendo ndoa, wakiipa nafasi maalum ya uhai sehemu hii ya ndoa, wakati huo huo huo wakimweka shetani mbali na ndoa yao.

**Kwa kupitia hayo yote, kujenga ndoa nzuri kunahitaji maombi sana.** Maombi ya bila kukoma hutusaidia kumtumaini Mungu. Huimarisha mahusiano mazuri ya pande zotekwa kila mmoja na Mungu, kitu pekee ambacho huimarisha ahadi kwa upandewa kila mmoja. Maombi huleta baraka nyingi za Mungu zinazohitajika sana katika mlingano. Baraka hizi zinaweza kufanya mabadiliko muhimu katika ndoa.

Kama umedhamiria kujenga ndoa nzuri, itagharimu ahadi ya agano, upendo wa agape na jitihada thabiti katika kujenga mawasiliano mazuri, ushirikishwanaji wa uzoefu na mambo ya ndani ya kimapenzi. Umakini wamambo haya, ukijumuishwa pamoja na maombi mengi, vitafanya ndoa zetu ziwe katika hali ambayo Mungu alikusudia ziwe!

**Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake;**

**Waefeso 5:22-25**

# Utakatifu na Heshima Ndilo Jina Lako

Dennis Gulledge

Cheo cha kidini “Reverend” kwa kawaida hutumiwa kwa watu wenye umuhimu sana kama ubunifu wa kutambua heshima ya mhudumu au mhubiri. Katika haraka ya watu kuongeza cheo cha heshima kwa watu walio wa tabaka la kikuhani katika ulimwengu wa kimadhehebu, wameenda mbali zaidi ya pale Biblia inapoishia kwa kufanya hivyo. Hakuna mhubiri anayepaswa kuruhusu kuitwa “Reverend” au aina nyingine yoyote ya cheo. Neno “mtakatifu” pia hutumiwa vibaya kama cheo kwenye umuhimu wa kidini kama katika “Kiti Kitakatifu.” Wengine hutumia hata neno “Ndugu” kama cheo. Kinachofanya vyeo hivi visiwe sahihi ni kwa sababu hakuna tofauti ya “makasisi na watu wa kawaida” katika Kaisa la Kristo. Yesu alitakaza vyeo vyote vya heshima katika dini (Mathayo 23:8-9).

Katika kukataa kwao kutumia cheo “Reverend [Mheshimiwa wa kuogopwa]” kwawanadamu, ndugu katika Bwana wenye nia njema mara kwa mara hutumia Zaburi 111:9 na kusema kwamba huu ndio wakati pekee neno hilo limetumika ndani ya Biblia, na kwa msisitizo, kwamba limetumika hapa tu kumrejea Mungu, si mwanadamu. Tatizo ni kwamba hoja hii ni ya kweli tu kulingana na mfano namna lilivyotumika. Neno “Reverend” huonekana mara moja tu katika Biblia toleo la ***King James***.Neno la kiebrania ilikotoka tafsiri ya “Reverend” limeonekana zaidi ya mara mia tatu katika Agano la kale.

Ni kweli kwamba Neno “Reverend” limetokana na neno la kiebrania *yare*. Neno hili limetokea mara 373 katika Agano la kale. Limetafsiriwa katika toleo la *King James* kama “Ogopa” (mara 76), “Hofu” (mara 1), “wasiwasi” (mara 242) “Hofu kubwa” (mara 5), “kutisha sana” (mara 2), “ya kutisha” (mara 24), “Heshima ya kutisha” (mara 1), “Kutisha mno” (mara 1), “matendo ya kutisha” (mara 1),

"Utisho" (mara 1), "mambo ya kutisha" (mara 4), "kuogopa" (mara 1), "kuogopesha" (mara 2) na "kuweka kwenye hofu" (mara 2).

Katika Mwanzo 19:30, Ruthu "aliogopa (yare) kuishi katika Soari." Neno hili limetumika mara mbili katika Kumbukumbu La Torati 28:58, "…***upate kulicha jina hili la fahari na utisho, BWANA, Mungu wako***." Muundo wa*yare* umetumiwa katika Isaya 18:2 kuelezea Waethiopia kama "*wa kutisha*". Daudi alitumia muundowa*yare* katika Zaburi 139:14 kusema, "***nimeumbwa kwa jinsiya ajabu ya kutisha***." Matendo yako ni ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana".

Maneno "Mtakatifu" na "Reverend" hayatumiki kama vyeo kwa Mungu, bali kama maneno yanayoelezea tabia yake. Zaburi 111:9 ni kifungu kinacholiinua jina la Mungu. Jina la Mungu linastahili heshima na hofu ya Mungu. Ni wapi palipo na heshima ya kina ambayo kwayo tunapaswa kujisikia kulielekea jina la Mungu Mwenyezi? Je, inathibitika miongoni mwetu pale tunapotamka jina lake, pale tunapomkaribia katika kuabudu na pale tunapoishi mbele Zake?

# SARAFU ZA KENNEY

***"Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi kwa hao wa matamanio kwa wokovu"*** (Waebrania 9:28).

Kristo atakuja tena, ila hatakuja kujiweka dhabihu kwa ajili ya dhambi, kama alivyofanya wakati wa kwanza. Atakuja kuwahukumu wale waliotii Injili yake na kuwaadhibu wale ambao hawajatii Injili. Wokovu ni kutoka kwenye nini? Kifo cha pili.

**David R. Kenney muhubiri Kanisa la Kristo lililoko Wadsworth, Ohio, USA**

# *MSAKA TONGE*

## Kitabu cha Yona

**Rebecca Rushmore**

1. Je! Mungu alimwamuru Yona aende mji gani?
2. Je! Yona alijaribu kukimbilia mji gani?
3. Je! Yona alifanya nini baada ya samaki kummeza?
4. Je! Ni nini kilimfanya samaki amtapike Yona nchi kavu?
5. Je! Mji ambao Yona alikwenda kuhubiri ulikuwa mkubwa kiasi gani?
6. Je! Ni siku ngapi Yona alisema kuwa zimebaki kabla Mungu angeuangamiza mji?
7. Je! Yona alijisikiaje baada ya watu wa mji kutubu?
8. Je! Yona alimwomba Mungu achukue nini kutoka kwake?
9. Taja vitu vitatu ambavyo Mungu aliviandaa ili kumfundisha Yona somo.
10. Je! Ni watu wangapi ambao Mungu alisema waliishi katika mji?

**[Tafadhali tenga muda, usome kitabu cha Yona kisha ujibu maswali hayo na kujiwekea alama]**

# UONGO MKUU WA SHETANI

**Gary C. Hampton**

Yesu alimwita Shetani "***mwongo tangu mwanzo***" na baba wa waongo (Yohana 8:44). Alililejea tukio lililoandikwa katika Mwanzo 3 pale Shetani alipo mdanganya mwanamke. Kuna baadhi ya masomo muhimu kwa ajili yetu katika kisa hiki cha kuhuzunisha.

**Shetani aliweka mkazo kwenye katazo badala ya upaji** (Mwanzo 3:1).Alimfanya Hawa azingatie tunda tu katika bustani ambalo hakutakiwa kula. Leo, kuna watu ambao wanalia kwa sababu ya vitu wasivyokuwa navyo. Badala ya kufanya hivyo, tunahitaji kuweka mkazo juu ya kutoa shukrani (Wathesalonike 5:18).Hata hivyo, Mungu ametupatia zawadi kubwa kuliko zote (2Wakorintho 9:15, Warumi 8:32).

**Shetani aliukana uhalisia wa laana ya mauti** (Mwanzo 3:4). Baba wa uongo alimwita Mungu Baba mwongo (Mwanzo 2:17). Watu wengine leowanaishi kana kwamba hakuna kifo, kama vile yule tajiri kwenye mfaano wa Yesu (Luka 12:16-21). Kila mmoja anapaswa kutambua kwamba, pamoja na maendeleo makubwa katika dawa, kila mmoja ana miadi na kifo (Waebrania 9:27).

**Shetani alizipinga fadhili za Munguzenye upendo kwa kusema Mungu alimnyima mwanadamu uwezo wa kukifikia kitu kizuri** (Mwanzo 3:5). Tunapaswa kutambua kuwa Mungu ni mwema na ni chanzo cha kila zawadi njema (Zaburi 136:1, Yakobo 1:17). Mungu na Neno lake wamelamiwa kuwa wapinzani wa mwanamke walipomfanya kuwa taji la uumbaji (Mwanzo 2:22-23). Mke mwema anasifiwa, na waume wanaamriwa kuwapenda wake zao kwa maneno yenye nguvu sana (Mithali 31:10, Waefeso 5:25-28).

**Shetani alisema mwanadam angeweza kuweka sheria yake mwenyewe**kwa kumwambia "***utakuwa kama Mungu***" (Mwanzo 3:5b). wengine wangependa tuamini kuwa tunaweza kujiwekea njia yetu

wenyewe ya wokovu. Yesu alisema lazima tufanye mapenzi ya Baba (Mathayo 7:21). Paulo alisema Mungu hataupa nafasi tena ujinga, bali anasisitiza kwamba watu wote watubu (Matendo 17:30). Njia ya kuyaendea maisha mapya ni kuzikwa pamoja na Kristo katika ubatizo na kufufuliwa ili kuishi maisha mapya (Warumi 6:3-4).

Upuuze uongo wa Shetani. Ishi kila siku kulingana na mapenzi ya Mungu, ukijua kwamba hiyo ndiyo njia ya kuingia Mbinguni.

**Mambo 25 Ambayo Shetani Hawezi Kuyafanya**

**Tim Childs**

1. Kutamani Mungu asiwepo.
2. Kupunguza nguvu za upendo wa Mungu.
3. Kutuhamisha na kutupeleka mahali pasipofikiwa na Mungu na upendo wake.
4. Kumchanganya Mungu ili asiweze kuwajua walio wake.
5. Kumjaribu Mungu ili atende uovu.
6. Kubadilisha tabia ya Mungu.
7. Kumfanya Mungu adanganye.
8. Kumshinda nguvu Mungu.
9. Kuuangamiza uzao wa kifalme.
10. Kukifanya kilicho cha ukweli kuwa cha uongo, na cha uongo kuwa cha kweli.
11. Kuishinda kweli ya Mungu iliyofunuliwa.
12. Kumlazimisha Mungu kuwa shirika na wanaokumbatia mafundisho ya mashetani.
13. Kuiba Neema ya Mungu, rehema, upendo na ustahivu.
14. Kuidhoofisha nguvu ya Injili ya Kristo.
15. Kunilazimisha kwa nguvu nimtende Mungu dhambi.
16. Kuzuia njia ambayo Mungu ameiandaa kwa matumizi yangu wakati majaribu yanakuja.
17. Kunijaribu kupita niwezavyo kustahimili na kupinga.
18. Kuniondoa kwa nguvu kutoka kwenye ulinzi wa macho ya Mungu na neema ya kuokoa.
19. Kusababisha kanisa Bwana wetu ulimwenguni likome.
20. Kuzuia ujio wa Yesu tena.
21. Kuzuia wafu wasifufuke kwa amri ya Yesu.
22. Kubadilisha kiwango cha Neno la Mungu ambacho watu wote watahukumiwa kwacho.
23. Kuzuia watoto wa Mungu waaminifu wasiende nyumbani kwenye mji wa Mbinguni.
24. Kuwakinga malaika na wafuasi wake na ghazabu na adhabu ya mwenyezi Mungu.
25. Kubadilisha hatima ambayo Mungu amemwandalia.

# Mfano Wa Epafra

**Neal Pollard**

Inavyoonekana, Epafra aliishi katika eneo ambalo sasa linaitwa Uturuki maeneo fulani kusini mwa ukingo wa mto Lycus karibu na Kolosai au Laodikia. Kulikuwa na jumuya kadhaa katika eneo hili ambazo zilikuwa na makusanyiko ya watu wa Bwana. Kwa kweli, eneo hilo linaweza kuitwa "Ukanda wa Biblia" wa zamani wa Asia.

Mungu alipoongoza mchakato wakulikusanya Agano Jipya lililovuviwa, likaandikwa, fundisho la Kristo lililofunuliwa kwa mikono ya waandishi kama vile Paulo lilienea kwa haraka. Nyaraka (Barua) zilizovuviwa zilipelekwa kwenye idadi kubwa ya makusanyiko yaliyokuwa yakikutana Asia ndogo na Ulaya Mashariki, na katika maeneo ya Palestina, Misri na Afrika Kaskazini. Katika nyaraka hizi zilikuwemo amri nyingi zisizo na idadi. Ufunuo mpya, mifano ya mwenendo katika ibadanakanuni za kuchukuliwa kutoka kwenye vielelezo na wasifu, kuonya, kukemea na kutia moyo vyote vilifanyika kupitia njia hizi tofauti.

Mmoja wa watu ambao Roho alimsukuma Paulo kuwazungumzia, ambaye kwa namna fulani hajulikani kwa wanafunzi wengi wa Biblia, ni Epafra. Amekosewa na watu wengi kwa kudhani ni Epafrodito aliyesifiwa na Paulo katika kitabu cha Wafilipi. Hata hivyo, Epafra anastahili kuigwa kwa sababu kadhaa.

**Epafra alifanya mpongowa maombi kwa ajili ya ndugu zake**. Katika maneno ya pongezi, Paulo aliandika, "***Epafra, aliye wa kwenu, mtumwa wa Kristo, ana wasalimu akifanya bidii kwa ajili yenu katika maombi, ili mpate kusimama wakamilifu na watimilifu katika mapenzi yote ya Mungu***" (Wakolasai 4:12). Paulo alisema alikuwa akiwapigania katika maombi. Hakuwaombea tu, bali alifanya hivyo kwa bidii kubwa.

Ingependeza kujua ni mara ngapi na ni wakristo wangapi ambao hawalitaji Kanisa tu katika maombi yao bali wanaomwomba na kumsihi Mungu kwa ajili ya ndugu zao mbele ya kiti cha rehema. Epafra alitaka Mungu awape nini watumishi wenzake? Inaonekana alitaka "***wakue katika neema, na maarifa ya Bwana wetu Yesu Kristo***" (2Petro 3:18). Alijali kuona wakiwa waaminifu na wakikua. Aliithibitisha ibada hiyo kwa maombi. Inapendeza kuona ndugu mume au mke anachukua orodha mahususi ya wakristo na kwenda nayo kwenye chumba cha maombi, akitaja majina yao mbele za Baba kwa unyoofu wa moyo na kumsihi kwa niaba yao. Je, hiyo ndiyo sababu Yakobo aliwahakikishia Wakristo, "***kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii***" (5:16)?

**Epafra alikuwa na shauku kubwa kwa ajili ya ndugu zake**. Paulo, katika waraka kwa Wakolosai, aliandika zaidi juu ya Epafra, "***kwa maana namshuhudia, ya kwamba ana bidii nyingi kwa ajili yenu, na wale walio katika Laodikia, na hao katika Hierapoli***" (Wakolosai 4:13). Moyo wake ulikuwa pamoja na watu wa Mungu! Epafra alikuwa ni mkristo aliyependa undugu (Waebrania 12:1). Neno lililotafsiriwa "***juhudi***" katika Wakolosai 4:13, katika lugha yake ya awali, linamaanisha hisia yenye shauku kwa ajili ya mema au mabaya, ikitegemea muktadha. Muktadha hapa unaonyesha wazi kwamba Epafra alikuwa na aina hiyo nzuri ya juhudi ambayo ilimvuta ajitolee Kwa ndugu zake.

Kwa vitendo, mtu atawafanyia nini ndugu ambao ana hisia shauku nao?Ndugu anapokosea, je, hatamtafuta (Yakobo 5:19-20)?Mkristo mwenzake anapokuwa mpweke au amevunjika moyo, Je, hata muinua (Waebrania 12:12-13)? Pale mkristo mwingine anaposimamia ukweli, licha ya ukusoaji wa Ulimwengu, je, hatamsifu kwa ujasiri (1Wakorintho 1:2)?

**Epafra alikuwa mtumishi mwaminifu kwa ndugu zake katika Kristo**. Paulo aliandika, "***Kama mlivyofundishwa jifunza na Epafra, mjoli wetu mpenzi, aliye mhudumu mwadilifu wa Kristo***" (Wakolosai 1:17) Lipsicomb alishikilia kwamba Epafra alianzisha Kanisa la Kristo la

Kolosai. Kuna uwezekano kwamba alifungua hata milango ya nyumba yake mwenyewe, Epafra bila shaka alilipenda Kanisa la Bwana na akawa tayari kwa ajili ya hilo. Kama “***mhudumu,***” Epafra aliwatumikia ndugu. Akiwa mwaminifu, aliliimarisha Kanisa kwa imani yake. Akiwa “***wa Kristo***”, aliwaonyesha watu wa Bwana ni kiasi ganiYesu alimaanisha kwake.

Yesu alifundisha yote mawili ukuu wautumishi (Mathayo 23:11) na umuhimu wa uaminifu (Mathayo 24:25). Uaminifu kwa Kristo lazima ujidhihilishe katika kuwatumikia wengine (Yohana 13:12-17). Ukomavu katika Kristo unamwelekeza mtu kwenye hitimisho hilo. Upendo unapokamilishwa, mtoto wa Mungu hujitahidi ndani ya kusanyiko lake ili kuendeleza afya ya kiroho na ukuaji wa wengine. Epafra lazima atakuwa “***amemuonja***” Bwana (1Petro 2:3).

Ndugu walikuwa pamoja na Epafra katika maombi yake, katika moyo wake na katika majukumu yake. Paulo alimsifia kwa watu (Wafilipi 23) pamoja na makusanyiko yote (Wakolosai 1:7, 12-13), ni dhahiri, kwa kwa sababu alikuwa tawi linalozaa matunda katika shamba la mizabibu la Kristo. Wakristo wengi wanaoiga maisha ya maombi, upendo na utumishi wa Epafra kwa kurejelea Kanisa watasaidia kukuza umoja wa kibiblia (Yohana 17:20-21) na upendano wa ndugu (Yohana 13:35) unaosisitizwa sana na mwokozi wetu.

## RUBI ZA ROBISON

Katika matendo 12, mtawala wa kiyahudi aitwae Herode alipokea sifa kutoka kwa watu kama mungu. Hakuwakemea, kwa hiyo Mungu wa kweli alimpiga hata akafa. Katika matendo 14, watu wa Listra walianza kuwaabudu Paulo na Barnaba kama miungu. Wale wakristo watumishi walirarua nguo zao na kuwakemea watu kwa ujasiri, wakisema, “***Akina bwana, mbona mnafanya haya? Sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi; …*** (aya 15). **Mungu ndiye pekee anayestahili kuabudiwa. Wanadamu wote wameumbwa sawa.** Hoja hizi zote ni lazima ziwekwe ndani yetu na kuongozwa na kweli.

# Vipi Kuhusu Mwizi Msalabani?

**Brian R. Kenyon**

Tunapojifunza ulazima wa ubatizo na washiriki wa madhehebu fulani, hoja iliyozoeleka wanayoileta ni ya "mwizi Msalabani". Mara nyingi wanauliza, "vipi kuhusus mwizi Msalabani? Hakubatizwa, kwani alibatizwa? Hapo inaonyesha kwamba, kama mwizi Msalabani hakubatizwa, na bado aliahidiwa na Yesu kuwa Paradiso, basi hatuhitaji kubatizwa. Je, mwizi Msalabani anathibitisha kwamba ubatizo si wa lazima kwa ajili ya wokovu? Ebu tufikirie juu ya tukio hili namna linavyohusiana na wokovu.

## Mpangilio

Mazungumzo kati ya Yesu na mwivi Msalabani yalitokea mwokozi alipokuwa anasulibiwa (Luka 23:39-43). Kulikuwa na wahalifu wawili waliosulibiwa pamoja na Yesu siku ile mbaya (Yohana 19:16-18). Mwanzoni, wahalifu wote wawili walikufuru (Mathayo 27:44, Marko 15:32). Lakini mmoja wao akapata mabadiliko ya moyo. Kabla hatujamfikiria, angalia Luka anachosema juu ya Yule mwingine, "***Na mmoja wa wale wahalifu walioangikwa alimtukana, akisema; Je, wewe si Kristo?Jiokoe nafsi yako na sisi***" (Luka 23:39). "kufuru" maana yake nena vibaya dhidi ya (Marko 3:28-29; Yohana 10:36; Matendo 13:45; 1Wakorintho 4:13). "***Je, wewe si Kristo?...***" Maneno haya yalisemwa katika hali ya kejeli sawa tu na wale waliopita karibu na msalaba walivyonena (Mathayo 27:39-44). Kinyume na haya, yule mhalifu mwingine, akimjibu, akamkemea, akisema, "***wewe***

***humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu, bali huyu hakutenda lolote lisilofaa***" (Luka 23:40-41). Mhalifu huyu alionyesha moyo wa toba. "***Wewe humwogopi Mungu***?" Inaonyesha kwamba mhalifu huyu alitambua kuwa kuna Mungu. Huenda hii pia ikawa ni utambulisho kwake kwamba Yesu ni Mungu (Ling Yohana 1:1-3)! Mhalifu huyu mwenye toba alikiri kuwa yeye pamoja na yule mhalifu mwingine walistahili kupata hukumu ya kifo (Matendo 25:11). Pia alitambua kuwa Yesu hakutenda kosa lolote.

Baada ya kumkemea Yule mhalifu mwingine, mwivi msalabani "***akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako***" (Luka 23:42). "***Unikumbuke***" hapa pana wazo la nikumbuke daima! "***utakapokuja katika ufalme wako***" inaonyesha kwamba mhalifu huyu alikuwa anayajua madai ya Yesu juu ya kuanzisha ufalme wake (Mathayo 16:18-19). Hii inaonyesha kuwa alikuwa myahudi, tena mwanafunzi wa Yohana, ambaye alikuwa amesikia mahubiri na mafundisho ya Yesu (Marko 1:15), au inawezekana alikuwa mtu wa mataifa, aliyajua mashtaka aliyopelekewa Yesu (Luka 23:10-11), majibu ya Yesu (Yohana 18:33-37), dhihaka walizokuwa nazo maadui wakimpeleka Yesu msalabani (Mathayo 27:27-31) na anuani iliyowekwa juu ya msalaba wa Yesu (Yohana 19:19). Kwa namna yoyote ile, huyu mwizi alijua kwamba kifo haukuwa mwisho, na alitaka akumbukwe baada ya maisha ya kidunia.

Kumhakikishia mwivi aliyetubu Msalabani, "***Yesu akamwambia, 'Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja name peponi'***" (Luka 23:43). "Leo" maana yake sasa hivi, kama vile kusema, "huna haja ya kungoja mpaka ufalme uje". "Paradiso" (pepo) ni neno la kihistoria la kiajemi ambalo kihalisia lina maana "hifadhi" au "bustani" (matukio mengine ya neno hili yapo tu katika 2Wakorintho 12:4; Ufunuo 2:7). Yesu alimhakikishia mhalifu huyu furaha ya wokovu ambao ungeambatanishwa "***nami*** [Yesu]***Paradiso***."

## Suluhisho

Je, mwivi Msalabani amethibitisha kuwa ubatizo si wa lazima kwa ajili ya wokovu? Kwa kujibu swali hili, mambo matatu ni lazima yazingatiwe. Kwanza fikiria juu ya nasaba, [yaani mwongozo mzuri]. Tukio hili lilitukia wakati Yesu anakufa msalabani. Yesu hakutaka ubatizo ufanyike kwa wote mpaka baada ya kufufuka kwake (Mathayo 28:18-20). Marko 16:15-16). Yesu aliishi na pia alikufa chini ya sheria ya Agano la Kale (Wagalatia 4:4-5). Agano lake Jipya halikuwa na nguvu mpaka baada ya kifo chake: "***maana agano la urithi lilipo, lazima iwepo mauti yake aliyelifanya. Kwa kuwa agano la urithi lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu: kwa kuwa halina nguvu kabisa ukiwa yu hai yeye aliyelifanya***" (Waebrania 9:16-17). Hivyo, mwivi msalabani hakubanwa na amri, "***Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu***" (Matendo 2:38).

Pili, fikiri juu ya mwivi. Kama ilivyosemekana mwanzoni, uwezekano upo kwamba huyo alikuwa mwanafunzi wa Yohana, hivyo alibatizwa ubatizo wa Yohana (Mathayo 3:1-6). Inawezekana kwa wafuasi wa Mungu kubadilika na kuwa wahalifu (1Petro 4:15). Iwe alikuwa mwanafunzi wa Yohana au la, bado ukweli uko wazi: alionyesha toba, ambayo daima inakuwa ni sharti la msamaha (Ling., Isaya 55:7; Ezekeil 18:21; Yona 3:4-10; Zaburi 34:18; Luka 13:3,5)!

Tatu, fikiria juu ya ukamilifu wa kutokuwa na upendeleo kwa Yesu. Mara nyingi kulingana na tukio hili watu watasema, "Yesu anaweza kumsamehe yeyote anayetaka kumsamehe," kama vile kusema kwamba kwa matakwa yake Yesu angeweza kumsamehe mwizi kwa sababu alikuwa mwana wa Mungu (Yesu). Wazo kama hilo si la kweli na linaendana na mafundisho ya Kelvin! Yesu hawezi kwenda tofauti na mapenzi ya Baba yake (Yohana 5:19; 7:16; 8:28; 12:49; Ling Mathayo 20:23) wala hawezi kulikana neno lake mwenyewe (2Tim. 2:13). Kwa maana Yesu kujiamria kumsamehe mwivi kungemfanya aonekane ana upendeleo, kwa maana ya kwamba "***anawapendelea watu***", lakini Yesu hayuko hivyo (Matendo 10:34)!

## Wokovu

Mwivi msalabani ni mfano wa hali ya juu wa msamaha wa Mungu. Hata mhalifu kama yeye anaweza kusamehewa pale masharti ya Mungu juu ya msamaha yanapotimizwa (Ling. Sauli wa Tarso, 1Timotheo 1:12-15). Hata hivyo mwivi msalabani si kielelezo chetu cha wokovu leo. Aliishi na kufa chini ya sheria ya Agano la Kale. Sharti moja ambaloni la lazima kwa wokovu wa mwivi msalabani na wokovu na wetu ni toba (Matendo 17:30), inatakiwa kuwa ya namna ya "***huzuni ya Mungu***" (2Wakorintho 7:10). Yesu alitoa hitaji la ubatizo baada ya kifo chake kama sehemu ya sheria ya Agano Jipya (Marko 16:15-16; Ling. Matendo 10:48). Hivyo, kama mtu aliye nje ya Kristo ana toba ya kweli, atabatizwa atakapojua kwamba Mungu anautaka ufanyike (Mathayo 28:19-20). Jibu la Petro kwa wale Wayahudi waliotubu siku ya Pentekoste walioliza "***Tufanyeje***". Lilikuwa "***Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu***" (Matendo 2:38).Aya chache baadaye Luka aliandika, "***Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa***" (Matendo 2:38). Je, watu hawa kweli wangetubu kama hawakulipokea "kwa furaha" Neno la Mungu na kutaka kubatizwa? Ebu tufuate mfano wa toba wa mwivi, halafu tufanye anachotaka Yesu. Je, tumebatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi? Kama hapana, kwa nini tufasifanye hivyo leo?

***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu"***

# Je,Wanahitaji Kujua Nini Kabla Hawajabatizwa?

**Wes McAdams**

Naamini mara nyingi tunawabatiza watu kabla hawajafundishwa kikamilifu. Lakini mara nyingi imekuwa vigumu kutambua jambo ambalo mtu anapaswa kujua kabla hajabatizwa. Kwa kuwa ubatizo ni hatua ya mwanzo tu, wale wanaobatizwa wanalazimika tu kuwa na uelewa wa mambo ya msingi juu ya thiologia, mafundisho na matendo ya kikristo. Ingawa kuna swali kwamba ni nini hasa kinachoanzisha "uelewa wa msingi"? watu wanahitaji kuelewa nini kabla ya kubatizwa? Kwa kweli siwezi kutoa jibu la uhakika kwa swali hilo lakini labda mambo yafuatayo yatakusaidia unapofikiria juu ya swali hili.

## MATAZAMIO YA PINGAMIZI

Kwanza, najua mtu atauliza, "vipi kuhusu wale watu siku ya pentekoste, towashi wa kushi au Kornelio? Haionekani kama walifundishwa sana kabla ya ubatizo wao." Hilo swali muhimu sana. Kwa hiyo, katika matazamio ya swali hilo kuulizwa, ngoja niendelee na nilitaje.

Jibu ni rahisi tu, wayahudi wa karne ya kwanza, waongofu (watu wa mataifa waliofanyika kuwa wayahudi [kwa sababu ya dini]) na wacha Mungu (mataifa ambao hawakufanyika kuwa Wayahudi, lakini walimwabudu Mungu) walikuwa na ufahamu juu ya Mungu, dhambi, upatanisho, masihi Yule ajaye, na Ufalme wake ujao. Kwa kuwa kweli wayahudi waliokusanyika siku ya pentekoste (Matendo 2) huenda walikuwa na ufahamu zaidi kuhusu Mungu wa Biblia kuliko walivyo wakristo wengi waliokomaa leo.

Petro alipoelezea kwamba walikuwa wananena kwa lugha kwa sababu, “***Jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli,***” watu walielewa alichokimaanisha. Walielewa kwamba hukumu ilikuwa inakuja juu yao kwa sababu walikuwa “***wamemsalibisha na kumuua***” Bwana Yesu Kristo. WWalielewa kwamba walihitaji kujiokoa na kizazi chenye ukaidi (Matendo 2:40), kitu ambacho kiliwafanya waulize, “***Tutendeje ndugu zetu***?” (Matendo 2:37), na ndiyo maana watu 3,000 kati yao waliitikia Petro aliposema, ***“Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu***” (Matendo 2:38).

Kuna tofauti kubwa kati ya kumfundisha mtu wa karne ya 21 na kumfundisha myahudi (au mtu yeyote aliyefuata dini ya kiyahudi) katika ulimwengu wa karne ya 1. Hiyo haimaanishi kwamba ichukue miaka ya mingiili kumwandaa mtu kwa ajili ya ubatizo, bali inamaanisha kuwa watu wanahitaji kuwa na uelewa wa kutosha wa mambo machache ya msingi kabla hawajaingia kwenye maji.

## Wanahitaji kujua kuhusu Yesu

Jambo la kwanza kabisa, ubatizo unapaswa kupata msukumo wa upendo wa Yesu. Ubatizo unapaswa kuwa jibu la kile ambacho Yesu alikifanya Msalabani. Kana mtu anaelewa tu kuwa anahitaji kubatizwa ili aende mbinguni baada ya kufa lakini hana uelewa wa msingi kwamba Yesu ni nani na amefanya nini, basi atakuwa hana ufahamu anaouhitaji ili abatizwe.

Towashi wa kushi “alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu” (Matendo 8:27). Ni wazikwamba alielewa kuhusu sadaka, labda alielewa hata kuhusu ujio wa Masihi. Kwa hiyo, Filipo alipanda kwenye gari, akianza na fungu la maandiko katika Isaya, “***akamhubiri habari njema za Yesu***” (Matendo 8:35). Filipo akamwambia kwamba Masihi alishakuja na kwamba amefanyika kuwa sadaka ya mwisho kwa ajili ya dhambi.

Watu wanahitaji kusikia **habari njema kuhusu Yesu**. Huenda wanahitaji kuelewa jambo juu ya urithi wake wa Ibrahimu na Daudi,

Uungu wake, hali yake ya kuvaa mwili, kifo chake cha kujitoa dhabihu, ufufuo wake, utawala wake katika mkono wa kuume wa Baba, na kwa umuhimu zaidi, upendo wake. Wanahitaji kuelewa kwamba damu yake inaleta vitu kama**Ukombozi, Upatanisho, Msamaha na Utakaso.** Naam, najua hayo ni masomo ya kina, lakini ni vipengele vya lazima katika Injili. Sambamba na hilo, siyo magumu kama unavyoweza kuyadhania. Ukitumika muda zaidi, naamini kila kipengele kinaweza kuelezewa kiasi gha kumfanya hata mtoto mdogo aweze kuyaelewa. Mimi bado natia shaka kwamba tunakuwa na haraka kutaka kuwapeleka watu kwenye maji, ubatizo wao unakuwa na mwitikio zaidi kutokana na kubembeleza kwetu kuliko mwitikio wa kifo cha Kristo. Watu wanahitaji kujua habari za Yesu kwa usahihi kabla hawajabatizwa.

## Wanahitaji kujua kuhusu kupotea kwao

Kabla mtu hajabatizwa anahitaji kujua kuwa ana hatia mbele za Mungu. Anahitaji kujua, kwa sababu amechagua kujiunga na ubinadamu wa dhambi katika uasi dhidi ya Mungu, amekufa katika makosa na dhambi zake (Waefeso 2:1). Anahitaji kujua "***amemuudhi Mungu***" na ***ataadhibiwa sawa sawa na mtu mwingine yeyote***" (Waefeso 2:3).

Anahitaji kuelewa kwamba hawazi kufanya jambo lolote mwenyewe ili kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zake. Hawezi kufuta maovu aliyoyafanya kwa kutenda matendo mema mengi. Tumaini pekee ni Mungu kumrehemu na kumwonyesha neema. Njia pekee itakayotokea ni kupitia kwa Yesu.

Ubatizo hauna maana kwa mtu ambaye anafikiri, "mimi ni mtu mwenye heshima zangu. Sidhani kwamba Mungu ananiona kama mwovu au mtenda maovu" ni pale tu ambapo "***huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu inapoleta wokovu***" (2Wakorintho 7:10) ambao mtu anakuwa tayari "***kumwomba Mungu kwa dhamiri njema***" (1Petro 3:21) katika ubatizo.

Ubatizo ni kumwomba Mungu – kwa imani – aziondoe dhambi za mtu kupitia nguvu za damu ya Yesu Kristo (Matendo 2:38; 22:16; Warumi 6). Watu hawawezi kuwa tayari kubatizwa mpaka watakaijua hali ya kupotea kwao.

## Wahitaji wajue kujitoa kwao

Mwisho, lakini si kwa umuhimu, watu wanapaswa kujua kuhusu mahali wanakoingia Yesu alisema, kwanza inampasa mtu "ahesabu gharama" (Luka 14:25-33) kabla hajafanyika kuwa mwanafunzi wake. Wana wanahitaji kuambiwa jambo linalotegemewa kutoka kwao na mambo watakayoyaacha kama wanafunzi wa Yesu.

Wale wanaobatizwa si kwamba waishie kuelewa kuwa wanaifia dhamabi tu (Warumi 6:1-7), bali pia wanahitaji kuelewa jambo kuhusu Kanisa. Matendo 8:12 inasema, "***Lakini walipomwamini Filipo akizihubiri habari njema za Ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa wanaume na wanawake***." Ni lazima tuwafundishe watu kuhusu Ufalme na wajibu unaotakiwa katika ufalme huo.

Miongoni mwa mambo mengine yanayompa nafasi mtu kuongolewa kwa Kristo, ni kufundishwa mambo ya Kristo. Hawawezi kuwa tayari kujikabidhi kwenye mtindo wa maisha ya kikristo mpaka ajue maana yake.

## Mwisho

Kuna mambo mengi zaidi ambayo yangeweza kuzungumzwa kuhusu swala hili, lakini sitaki kutia hamasa kuwa mtu anakuwa msomi wa Biblia kabla ya kubatizwa. Ukweli wa mambo ni kwamba uamuzi wa kubatizwa usizingatie hisia au msukumo wa uinjilisti. Uamuzi wa kubatizwa unapaswa kuzingatia hali ya mtu kufundishwa maana ya kuwa mwanafunzi wa Yesu (Mathayo 28:18-20).

# Mambo Manne Katika Ukristo

**Mark N. Posey**

## Utangulizi

1. Napenda kuwa Mkristo! Ni jamno la kupendeza sana hapa ulimwenguni. Ni nini kinachofanya Ukristo uwe wa kuvutia sana na wakufurahisha?
2. Jibu: Kuna mambo manne ambayo wakristo huyafurahia. Ebu furahia kanuni zifuatazo.

**I. Msamaha (Mathayo 1:21; Luka 19:10; Yohana 1:29)**

A. Kwa nini tunahitaji msamaha?
   1. Jibu: dhambi hututenga mbali na Mungu (Warumi 3:23; Isaya 59:1- 2
   2. Je, umewahi kutengwa na familia yako kwa kipindi cha muda mrefu? Huzuni, upweke na kukata tama vikiwa ndani yako. Hebu fikiri kutengwa mbali na Mungu kwa sababu ya dhambi. Inatisha ukitafakari.

B. Hata hivyo, Yesu alikufa ili kumpatanisha mwanadamu na Mungu (2Wakorintho 5:18-21) na kutoa msamaha wa dhambi kwa wale ambao hutubu na kubatizwa (Matendo 2:38). Asante Mungu kwa msamaha.

**II. Baba.**

A. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba "***Baba yetu uliye Mbinguni***" (Mathayo 6:9).
   1. Baba yetu wa Mbinguni anatujali, anatupenda na anatubariki (Waefeso 1:3).

2. Nina rafiki ambaye baba yake alikufa. Siku moja alisema, natamani ningeweza kuzungumza naye”

B. Wakristo wanaweza kuzungumza na Baba yao wa Mbinguni kupitia Yesu kila dakika ya kila siku. Asante Mungu kwa kuwa Baba yetu.

**III. Familia.**

A. Wakristo wamebarikiwa kuwa na familia ya kiroho.

1. Upendo, kujali na kuguswa na baraka tele “***kwa wale walio na Imani na kuiona ni ya thamani***”
2. Familia ya Mungu ndio mfumo mkuu wa msaada duniani. Tunafungamana pamoja katika Yesu Kristo.

B. Siku moja tutafurahia muunganiko mkuu wa familia huko Mbinguni. Je, uko tayari kwaajili ya siku hiyo ijayo?

**IV. Baadaye.**

A. Mbingu inaelezewa kama tuzo na urithi.

1. Ni “***urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa… kwa ajili yenu***”. (1Petro 1:4).

B. Mbingu inaweza kuwa kitu utakachopata baadaye endapo utaishi kwa uaminifu kwa Bwana kuanzia hapa hadi umilele.

1. Kifo kinaleta hitimisho kwa sababu hugonga muhuri hatima zetu.
2. Je, mwelekeo wako wa baadaye ni wa furaha au huzuni?

# Kupambana Na Utawala

**Jeremy W. Barrier**

Kanisa la kwanza lilikua haraka kutoka kundi dogo, lililoonekana halina maana silo katika maeneo ya milima ya Palestina hadi kufikia kuwa kundi lililostawi na kukua lenye rasilimali nyingi za watu na fedha zilizoenea sehemu nyingi katika ulimwengu wa Mediterrania. Kanisa la kwanza lilishinda changamoto lilizokabiliana nazo katika ukuaji. Kanisa la kwanza lilipata shida ya utawala,jambo ambalo lilizuia ukuaji wao katika miaka ya mwanzoni.

Walipambana na utawala

> ***Baada ya siku kadha wa kadha Paulo akamwambia Barnaba, "Haya! Mrejee sasa tukawaangalie hao ndugu katika kila mji tulipolihubiri neno la Bwana, wa hali gani".Barnaba akaazimu kumchukua Yohana aliyeitwa Marko pamoja nao. Bali Paulo hakuona vema kumchukua huyo aliyewaacha huko Pamfilia, asiende nao kazini. Basi palitokea mashindano baina yao hata wakatengana; Barnaba akamchukua Marko akatweka kwenda Kipro. Lakini Paulo akamchagua Sila, akaondoka, akiombewa na wale ndugu apewe neema ya Bwana***. (Matendo 15:36-40).

Katika sura ya kumi na tano ya kitabu kinachoitwa***Matendo ya Mitume***, tunasoma juu ya "kutokukubaliana" kulikotokea kati ya viongozi wawili wa Kanisa la kwanza-Barnaba na Paulo. Watu hawa wawili walikuwa na uhusiano wa karibu na kufanya kazi pamoja kwa miaka mingi, na inaonekana walikua timu yenye nguvu na yenye ushawishi. Walianzisha makanisa katika kisiwa cha Kipro na pia katika

sehemu mbalimbali kuzunguka eneo la kati la Uturuki. Walikuwa wametumia muda mwingi sana, mchana, usiku, usiku, majuma na miezi pamoja ili kwamba waweze kuona pengine mmoja wao angekuwa na jambo la kusema. Kufikiria kwamba wangekuwa nahali ya kuto kukubaliana kiasi hicho juu ya watenda kazi haikuweza kueleweka.

Angalia maelezo machache juu ya kutokukubaliana huku. Mara ya kwanza walikubaliana kwamba, kazi, malengo na vipaumbele vilivyowekwa, vilikuwa vizuri na vilihitajika vitendeke; yaani walishawishika kwa pamoja kwamba walihitaji kurudi na kuimarisha makanisa sehemu zote walizotangaza Injili. Kutokukubaliana kwao kulikuwa katika maelezo ya mpango mzima. Hawakukubaliana kama Yohana Marko aambatane nao au la.

Katika Matendo 13:13, baada ya Paulo, Barnaba na Yohana Marko kumaliza tu kampeni kuu ya kwanza katika safari yao ngumu sana, inaonekana Yohana Marko, kwa sababu zisizotajwa, aliona kwamba kazi ya kampeni ngumu sana, naye alirudi Yerusalemu. Tunaona kutoka Matendo 15 kwamba Paulo alilichukulia hili kuwa usaliti kwenye kazi tu,bali pia ni usaliti binafsi dhidi yake yeye na Barnaba. Paulo anamuelezea Yohana Markokamamtu "aliewatelekeza." Yohana Marko alionekana kama msaliti.

Lakini, Barnaba ambayealiwatambua watu wenye uwezo, alikuwa mwenye huruma kuliko Paulo. Vile vile Sauli (sasa anaitwa Paulo) alikuwa hana marafiki na ilikuwa vigumu kushughulikiamambo mapema katika huduma yake, lakini Barnaba alimvumilia, akamwandaa na hatimaye akamkuza Paulo mpaka kufikia hatua ya kuwa mhudumu mkuu. Kwa namna hiyo hiyo, Barnaba alikuwa akifanya kazi na Yohana Marko, ambaye hakuwa msaliti, ila tu alihitaji muda zaidi kukua kama mtu na kama kiongozi.

Hata hivyo, kutoelewana kulikuwa ni kwa hali ya juu kiasi kwamba kulizua matatizo katika uhusiano wa Paulo na Barnaba hata wakaachana katika kutekeleza mipango yao. Barnaba akamchukua Yohana Marko, nao wakasafiri moja kwa moja kwa meli hadi mahali

ambapo Yohana Marko alishimdwa kupafikia hapo awali. Ninajiuliza ikiwa Barnaba angempa Yohana Marko fursa ya kukabiliana na hofu yake moja kwa moja na kuona mema waliyofanya huko Kipro na pia kukabiliana na hofu yake kwamba angeweza kama angeweza kuona kwamba matatizo yake hayawezi kutatuliwa.

Paulo, kwa upande mwingine, alishikanjia mpya na kuanza kutembelea makanisa yaliyokuwa Uturuki. Ingawa kifungu hakitupi maelezo yote, kilichowazi ni kwamba Paulo na Barnaba waliendelea kutekeleza kazi ya Kanisa licha ya tofauti za maoni kuhusu jinsi inavyotakiwa kufanyika. Kwa maneno mengine, bado walifanya kazi, na hawakuruhusu tofauti zao katika mitindo ya utawala kuzuia kazi.

Kama mawazo ya baadaye, kuna maelezo mawili katika maandishi haya ambayo yananivutia. Katika mstari wa 40, maelezo ya kwanza yanahusiana na ndugu waliowatuma: kifungu kinasema kwamba waliidhinisha jitihada za Paulo kuondoka na Sila. Andiko linasema kwamba "walimsifu"; kwa maneno mengine walizikubali juhudi hizo. Hata hivyo, walimsifu hasa "kwa neema ya Mungu". Kwa nini jambo hili? Katika hatua hii, tunaweza kudhani kwamba Paulo alikuwa pengine sababu ya msingi ya mgogoro huu na utengano. Hata hivyo, ndugu walimtendea Paulo "kwa neema" na kuzikubali jitihada zake nzuri, wakiipongeza kazi yake, bidii yake, utume wa Mungu na walitumaini kuona kwamba kazi bado inasonga mbele. Hata hivyo, iliwabidi "kuneemesha" matendo yake, na kutoa kiwango fulani cha msamaha kwake. Walimtolea Paulo, kile ambacho hakuwa tayari kumpa Yohana Marko.

Ukisoma sehemu nyingine ya kitabu cha Matendo, hatuwezi kujua kama Pauo, Barnaba na Yohana Marko waliwahi kufanya kazi kwa karibu tena kama timu ya watu watatu. Kwa kweli, wasomaji wengi wa Biblia leo wana mtazamo kwamba Barnaba na Paulo hawakufanya kazi kwa ukaribu tena. Walakini, maelezo madogo ya sehemu ya pili yanafaa kuzingatiwa. Tunajua kwamba msamaha na uponyaji lazima vilifanyika miongoni mwao. Baada ya hayo yote, hatimaye Paulo alimjaribu Yohana Marko tena, na punde si punde

akagundua kwamba Barnaba alikuwa amesema sahihi kuhusu Marko. Katika 2Timotheo 4:11, Paulo alimwandikia mfanyakazi mwenzake kijana aitwae Timotheo, alisema “***umtwae Marko umlete pamoja nawe, maana ananifaa kwa utumishi***.” Paulo, ambaye alihitaji sana neema ya ndugu zake, hatimaye alifikiri jinsi ya kutoa neema hiyo kwa wengine.

Katika kuhitimisha, wakati Kanisa likikua kwa kasi katika karne ya kwanza, hii haimaniishi kwamba halikuwa na sehemu yake ya matatizo, tunaona Paulo na Barnaba walitofautiana katika masuala ya utawala, maswala ya watenda kazi na mambo mengine mengi. Hata hivyo kwa kuendelea kuwa waaminifu kwa Mungu na neema yake, walijifunza jinsi ya kutendeana wema. Na kwa sababu hiyo, kazi iliendelea kukua. Ikiwa wafuasi wa Yesu leo wanaweza kutendeana wema kama tulivyoona katika mfaano huu kutoka kwa waamini wa kwanza, basi pengine tutaona ukuaji zaidi pia.

***Baada ya siku kadha wa kadha Paulo akamwambia Barnaba, “Haya! Mrejee sasa tukawaangalie hao ndugu katika kila mji tulipolihubiri neno la Bwana, wa hali gani”.Barnaba akaazimu kumchukua Yohana aliyeitwa Marko pamoja nao. Bali Paulo hakuona vema kumchukua huyo aliyewaacha huko Pamfilia, asiende nao kazini. Basi palitokea mashindano baina yao hata wakatengana; Barnaba akamchukua Marko akatweka kwenda Kipro. Lakini Paulo akamchagua Sila, akaondoka, akiombewa na wale ndugu apewe neema ya Bwana*.** (Matendo 15:36-40).

# Jibu la Hotuba Juu ya Ala za Muziki

**Cecil May Jr**

Nilisikiliza kwa makini na kuandika mahubiri ya mtu ambaye ninamwona kuwa rafiki na ndugu akisema kwamba muziki wa Accapella [bila vyombo] ni mapenzi yake, lakini tukibishana kuwa hakuna kitu chochote katika Biblia kinachokataza matumizi ya muziki wa ala katika ibada kwa Mungu. Hili si jambo geni kwake. Ameeleza haya mara nyingi hapo awali, na nimemjibu hadharani kwa maandishi hapo awali. Hii ni mara ya kwanza ambayo ninafahamu kwamba ametoa sababu za kuamini kama anavyoamini. Hapa kuna sababu zangu za kimaandiko, za busara na za kihistoria za kutofautiana naye.

Nasikitika kuona hatujapata fursa, au hatujaitmia fursa kukaa pamoja na kujadili suala hili kwa upendo wa kila mmoja, wa Mungu na wa maandiko. Anakiri "kujitolea umwamba kwa maandiko" na kwa imani kwamba jambo muhimu zaidi la kuuliza katika kuamua mwendo wa hatua ni "Biblia inasema nini?" Naamini ni mkweli katika hilo, lakini pia ninaamini amekosea katika usomaji wake na matumizi juu ya suala hili.

- **Suala la Wokovu?**

Swali la kwanza linaloulizwa siku hizi ni, "Je, muziki wa ala ni suala la Wokovu? "Je, swali linamaanisha nini? Ni njia ya kusema, "Siamini kuwa Mungu anajali kwa njia moja au nyingine kuhusu vyombo vya muziki? Ikiwa ni hivyo, naomba kuwa tofauti kama nitakavyoonyesha. Au, je, ina maana Mungu atamhukumu mtu kwenda jehanamu kwa sababu tu ya kumwimbia sifa kwa kutumia vyombo vya muziki? Kwa maana hiyo, swali linalenga mtu ambaye ni sawa na asiye na dhambi katika jambo lolote jingine, isipokuwa anaabudu kwa

kutumia muziki wa ala. Je, hilo litamfanya asiokolewe? Kwa kweli hakuna mtu kama huyo.

Wakati ni haki yetu kuhukumu ikiwa mafundisho ni ya kweli au ya uongo(Mathayo 7:15-16), na kama kitendo fulani ni sahihi au si sahihi (Wagalatia 5:21), si haki yetu kuamua nani aokolewe na nani asiokolewe? (Warumi 14:4). Swali, "Je, ni suala la wokovu? Wengi wanaonyesha kutokuelewana kuhusu asili ya Wokovu. Watu wanaopotea hawapotei kwa sababu ya dhambi fulani moja wanayofanya au jukumu fulani wanaloshindwa kufanya. Wanaume na wanawake wanaokolewa kwanza kabisa, kwa sababu wako ndani ya Kristo, halafu kwa sababu "***wanatembea nuruni"***(1 Yohana 1:7), kwa sababu "***wao wanaenenda si kwa kuufuata mwili bali Roho***" (Warumi 8:14), kwa sababu ni "***waaminifu"*** (Warumi 4:12).

Kutembea katika nuru haimaanishi kwamba hutendi dhambi kamwe (1 Yohana 1:7). Mungu atawahukumu wakristo, si kwa tendo moja la mtu binafsi, bali kwa uaminifu wetu kwa ujumla, mtindo wetu wa maisha, mpangilio wa mawazo yetu (Wakolosai 3:1-2). Mungu pekee ndiye anayeweza kufanya hukumu hiyo. Sisi hatuwezi. Nimependa jinsi G. C. Brewer alivyoelezea:

***Hatutumii muziki wa ala katika ibada kwa sababu hakuna mamlaka katika Agano Jipya. Huu ndio msimamo tunaouchukua na hili ndilo suala kati yetu na wanaotumia vyombo. Kitu kingine chochote ambacho kinaweza kuletwa kwenye mjadala hakina umuhimu na utata. Hili ndilo suala. Si swali la nani atahukumiwa au nani hatahukumiwa. Si swali la jinsi baadhi ya watu walivyo wema na waaminifu wanaotumia vyombo vya muziki wa ala katika kuabudu- wema na watu wanyoofu kwa mamilioni wananyunyiza watoto wachanga, kuungama kwa makuhani na kuhesabu shanga katika sala, nk. Si swali la kiasi gani mtu anaweza kuwa na makosa na bado akaokolewa, au makosa ya mambo mengi ambayo tunaweza kufanya ambayo Mungu hajaidhinisha na bado tukawa wakristo. Ni swali la nini Agano Jipya linatuidhinishia kufanya katika ibada na nini halijaidhinisha.Tunapotii Neno la Mungu tunakuwa na***

***ahadi za Mungu-pamoja na wokovu wa milele. Tunapokataa au kushindwa au kupungukiwa na mapenzi ya Mungu/makusudi ya Mungu, Mungu atatuhukumu. Tunaambiwa tusihukumiane sisi kwa sisi***. (A Medley on the Music Question or a Potpourri of Philology. Nashville: Gospel Advocate, 1948, 12-13)

Wengine wanasema, "Ikiwa Mungu hakutaka muziki wa ala katika ibada za kanisani, hakika angejua jinsi ya kusema hivyo". Badala yake, Biblia inaonyesha wazi kwamba, wakati Mungu alipotaka muziki wa ala utumike katika ibada alijua namna ya kuuomba, na alifanya hivyo. Matumizi ya vyombo ni tendo lililohitajika katika ibada za Agano la Kale, kama vile kufukiza uvumba, kutoa dhabihu za wanyama, na kucheza. Kwa hiyo, sio mfano wa kuimba, na sio kanuni ya kutafsiri kuchagua njia moja ya Agano la Kale ili kutumia na kuacha nyingine bila kutumika.

Wito wa mara kwa mara wa kuimba pamoja na ukimya kamili wa Agano Jipya juu ya sifa za ala za muziki unaonyesha kwamba Mungu aliondoa kimakusudi muziki wa ala katika sifa na kuabudu katika Agano Jipya. Mitume daima walitofautisha vipengele vya kimwili vya ibada ya Agano la Kale na ibada ya kiroho ya Agano Jipya. "***Maana sisi tu tohara, tumwabuduo Mungu kwa Roho, na kuona fahari juu ya Kristo Yesu, wala hatuutumainii mwili***" (Wafilipi3:3). Tohara ya kimwili inalinganishwa na tohara ya kiroho, ambayo ni kukatwa au kuondolewa kwa mazoea ya dhambi (Wakolosai 2:18). Mwandishi wa Waebrania alitofautisha shambulio la hisia za kimwili ambalo humpata mtu anayeingia hekaluni na usahihi wa ibada ya kiroho. "***Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake. Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana; maana sadaka kama hizi ndizo zimpendezazo Mungu"*** (Ebr 13:15-16). Tunapaswa kufundishana na kuonyana katika Zaburi, nyimbo na Tenzi za Rohoni. Ninaweza kufanya hivyo kwa sauti yangu. Siwezi kufanya hivyo kwa kinanda, gitaa au mfumo wa ngoma za kisasa.

- **Vyombo vinaamriwa na kuthibitishwa katika Agano Jipya**.

Ombi la kwanza la mhubiri wetu lilikuwa kwa yale ambayo Agano la Kale linasema kuhusu muziki wa ala. Matumizi ya ala za muziki yaliamriwa waziwazi kuwa sehemu ya ibada ya hekaluni. Mungu aliwaambia Walawi wavitumie, watumie vyombo ganina wapi pa kuvitumia(1 Nyak 5:11-14; 7:6; 29:25-28). Kumbuka kwamba vilikuja hekaluni kwa uhusiano wa karibu na sadaka za kuteketezwa na sadaka za dhambi. Zaburi ya 150 inaomba sifa pamoja na shukrani kamili.

***"Haleluya.Msifuni Mungu katika patakatifu pake; Msifuni katika anga la uweza wake.Msifuni kwa matendo yake makuu; Msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake. Msifuni kwa mvumo wa baragumu; Msifuni kwa kinanda na kinubi; Msifuni kwa matari na kucheza; Msifuni kwa zeze na filimbi; Msifuni kwa matoazi yaliayo; Msifuni kwa matoazi yavumayo sana. Kila mwenye pumzi na amsifu Bwana. Haleluya.***" (Zaburi 150:1-6).

Zaburi inataka ala za muziki zitumike hekaluni(Patakatifu, aya 1). Kama marejeleo katika historia pia yalivyo, na inajumuisha kumsifu Bwana kwa ngoma, tendo la Agano la Kale la kumsifu na kumwabudu Mungu.

Kuna msisitizo mkubwa katika Agano Jipya kuhusu mabadiliko ya maagano. Mabadiliko ya maagano yalihusisha hasa mambo yanayohusiana na ibada. Yesu Kristo ndiye Kuhani wetu mkuu, na kila mkristo ni Kuhani(Ufunuo 1:6). Hatuna haja ya ukuhani wa Walawi au wa Haruni kama mpatanishi; sisi wenyewe tunamkaribia Mungu kwa ujasiri kupitia Yesu Kristo(Waebrania 4:16). Yeye ndiye dhabihu yetu; hatuna haja ya kutoa dhabihu za wanyama safi. "***Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani***" (Waefeso 2:14-15). Kristo alifuta matakwa ya sheria, akaiondoa na kuiogongomea msalabani. Matokeo

yake, hatupaswi kuhukumiwa kwa sikukuu, mwandamo wa mwezi au sabato(Wakolosai 2:14-17).

Ibada ya Agano la Kale mara nyingi huitwa ya kimwili wakati baada ya Agano Jipya ni ya kiroho(Wafilipi 3:2-6).Ibada ya hekaluni ilikuwa ni utendaji uliobuniwa ili kuchochea hisia. Kulikuwa na harufu ya uvumba, nyama inayoungua na damu inayotiririka. Kung'aa kwa dhahabu, fedha na shaba na uzuri wa kuvutia wa zulia zuri ulikutana na macho. Sauti za kondoo wakilia na kulia kwa ng'ombe zilisikika. Wacheza muziki walicheza mbele za Bwana, na kwaya za Walawi waliovaa mavazi meupe wakaimba kwa kusindikizwa na tarumbeta, kinanda, kinubi, matari, filimbi, na matoazi yenye sauti kuu-uimbaji mzuri sana ukikusudia kugusa kila njia ya utambuzi wa hisia.

Kwa tofauti kubwa kanisa la Agano Jipya linapaswa kuabudu katika roho na kutokuwa na imani katika mwili (Wafilipi 3:3). Katika Waebrania, ibada ya dhabihu ya kimwili ya Agano la Kale inalinganishwa na dhabihu ya Yesu ambaye alikufa nje ya kambi. Makuhani wa Agano Jipya(Kila mkristo) wanahimizwa***"Tuna madhabahu ambayo wale waihudumiao ile hema hawana ruhusa kula vitu vyake. Maana wanyama wale ambao damu yao huletwa ndani ya patakatifu na kuhani mkuu kwa ajili ya dhambi, viwiliwili vyao huteketezwa nje ya kambi. Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango. Basi na tutoke tumwendee nje ya kambi, tukichukua shutumu lake***" (Waebrania 13:10-13). Mambo ya ibada ya kiyahudi ambayo pia yalipaswa kujumuishwa katika ibada ya Kikristo yamebainishwa. Kuimba kulikuwepo. Muziki wa ala haukuwepo. Ala za muziki zilikuwa maarufu katika ibada ya hekaluni, kwa ujumla zilitumiwa katika ibada ya kipagani na katika maonyesho pia. Zilijulikana na kupatikana, pia zilitakiwa zitumiwe katika ibada ya kikristo, lakini hazikutumiwa. Kutokuwepo kwake katika ibada ya Agano Jipya "si kwa bahati mbaya" zaidi kuliko uvumba, kucheza mbele za Bwana au kutumia mboga chungu za mlo wa pasaka katika karamu ya Bwana.

Kuna ushahidi mwingi wa Agano Jipya kwa muziki wa sauti na sio ule wa muziki wa ala. Yesu na mitume kumi na mmoja(bila Yuda Iskariote) waliimba wimbo walipokuwa wakitoka katika chumba cha juu ambako Bwana alianzisha Meza ya Bwana(Math 26:30; Mk 14:26). Yakobo alihimiza kuimba kama njia ya kuonyesha furaha, na sala kama mwitikio sahihi wa jambo(mateso) (Yakobo 5:13). Paulo aliwahimiza wakristo kumwimbia Bwana neema mioyoni mwao (Wakolosai 3:16), na kuimba na kushangilia mioyoni mwao kwa Bwana(Efe 5:19). Wakristo wanapaswa kufundishana na kuonyana kwa kuimba (Wakolosai 3:16; Waefeso 5:19).

Baadhi ya marejeleo ya kuimba huuweka muziki mahususi kwenye mikusanyiko. Unabii katika Zaburi 22:22 uliotamkwa katika Waebrania 2:12, unatoa taswira ya Kristo katika kusanyiko la watu wake akiimba sifa kwa Mungu pamoja nao. Wakotintho waliimba katika kusanyiko, naye Paulo anawakumbusha kwamba kusanyiko ni la kuwajenga watakatifu na kuwasihi waimbe kwa maneno yanayoeleweka(1 Kor 14:15).

Makusudi ya uimbaji yanaonekana katika Agano Jipya: Kumsifu Mungu (Waebrania 2:12), kumshukuru Mungu (Waefeso 5:19-20; Wakolosai 3:16-17), kufundishana na kuonyana (Wakolosa 3:16) na kukiri imani katika Kristo (Waebrania 13:15, tafsiri halisi). Vyombo vya muziki havifanyi mambo haya.

- **Vyombo vya muziki mbinguni?**

Inasemekana kwamba ala za muziki katika ibada ya Agano la Kale na ala za muziki mbinguni zinaonyesha wazi kwamba Mungu hazichukii ala za muziki. Bila shaka hakuna anayeshikilia kwamba Mungu anazichukia ala za muziki. Aliamuru matumizi yake katika ibada ya Agano la Kale pamoja na mambo mengine mengi ambayo hayakuamriwa katika Agano Jipya. Vipi kuhusu vinubi mbinguni? Vinubi vimetajwa mara tatu katika kitabu cha Ufunuo. “***Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za mwana-kondoo, kila mmoja wao ana kinubi,***

***na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu***” (5:8). “***Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni, kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi kuu.Na hiyo sauti niliyoisikia ilikuwa kama sauti ya wapiga vinubi, wakivipiga vinubi vyao***” (14:2). “***Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamaana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake walikuwa wamesimama kando-kando ya hiyo bahari yay a kioo, wenye vinubi vya Mungu***.”

Kati ya matukio hayo matatu, moja halisemi juu ya vinubi halisi bali "***sauti kama sauti ya wapiga vinubi wakipiga vinubi vyao***". Ufunuo ni "Apocalyptic" iliyoandikwa kwa ishara na alama, zikifafanua mambo ya kiroho kwa kuzungumza juu ya vitu vya kimwili vinavyojulikana zaidi. Mbinguni, hatutavaa tena miili yetu ya nyama bali miili ya kiroho, isiyoweza kufa, isiyoharibika na yenye utukufu (1 Wakorintho 15:42-43). Sijui "***mwili wa kiroho***" ni nini, zaidi ya maelezo yake katika maandiko. Sitarajii, hata hivyo, kutembea kihalisia kwenye barabara ya dhahabu, katika jiji lililopambwa kwa kila aina ya mawe ya thamani(Ufunuo 21:19-21). Sitarajii kuona bakuli halisi za dhahabu zilizojaa uvumba, au bahari ya kioo iliyochanganyika na moto au vinubi halisi.

- **Psallo?**

Inasemekana kwamba Psallo, mojawapo ya maneno ya kigiriki yaliyotafsiriwa "***kuimba" au "kuimba sifa"*** katika Agano Jipya, kwa hakika inamaanisha "*kuimba kwa kuambatana na ala*". Etymolojia yake inatokana na "*kung'oa*" na inatumika katika tafsiri ya Kiebrania(septugiant) kumaanisha "***kuimba kwa kuambatana na ala***". Maana, ingawa, haijaamriwa na etymolojia; imedhamiriwa na matumizi ya sasa. Kufikia nyakati za Agano Jipya, ilikuwa imefikia maana ya "***kuimba***". Kila toleo linalotambulika kwa hivyo hutafsiri(haipingwi kuwa neno hilo haswa linamaanisha "***kuimba bila ala*"** kwa ufafanuzi. Inamaanisha tu "*kuimba*". Haisemi, "*hakuna ala*", haijumuishi vyombo vya muziki.Wala haiidhinishi vyombo vya muziki).

Neno ‘psallo’limetumika mara tano katika Agano Jipya, ikijumuisha mara mbili katika mstari mmoja huo huo.

**"*tena ili Mataifa wamtukuze Mungu kwa ajili ya rehema zake; kama ilivyoandikwa, Kwa hiyo nitakushukuru kati ya Mataifa, Nami nitaliimbia jina lako*"** (Rum 15:9). **"*Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia*"** (1 Kor 14:15). **"*mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu*"** (Efe 5:19). **"*Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? Na aombe. Ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi*"(**Yak 5:13)

Wakati mmoja inaweza kuwa na maana ya **"*cheza*"** au **"*kung'oa*"**, chombo cha **"*kung'olewa*"** kimebainishwa. Kuimba wimbo(psallo) kwa Bwana kwa moyo wako wote.

- **Sheria za ukimya**

Msemaji wetu anabainisha kwa usahihi kwamba ukimya pekee haukatazi. Tunafanya mambo mengi ambayo hayajakatazwa katika maandiko bila kipingamizi. Tunajejenga na kukutana katika majengo ya kanisa, tunatumia vitabu vya nyimbo na PowerPoint, na tunakaa kwenye viti vilivyofunikwa, ambavyo hakuna hata kimoja kilichotajwa katika maandiko au kilichojulikana na kanisa la kwanza. Ni pale tu amri mahususi inapotolewa ndipo ukimya kuhusiana na mambo yanayofanana unakataza matumizi yake.

Ikiwa katika kuhubiri imesemwa kwamba ukimya unakataza, weka alama hiyo hadi kuzungumza kwa mkato. Ukimya hukataza tu wakati kunapokuwa na mwelekeo maalumu, pamoja na ukimya kuhusu aina zinazolingana za mambo. Sio ukimya mwingi kama amri maalumu inavyokataza. Mfano wa kawaida ni safina ya Nuhu. Mungu alisema, ***"Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami***" (Mwa 6:14), hakuna anayeonekana kujua sasa "mvinje" ni aina gani ya mti, lakini Mungu alijua na Nuhu alijua, **"*Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu, hivyo ndivyo alivyofanya*" (**Mwa 6:22).

Ni wazi, kama Mungu angesema tu, "***Jifanyie safina*"**, nyenzo yoyote ingetumika. Kwa sababu alitaja***"mti wa mvinje*"**, kutumia aina nyingine yeyote ya mbao kungekuwa kutotii. Agano Jipya linatumia amri maalumna ukimya kwa njia hii haswa. Makuhani kutoka kabila ya Yuda wamepigwa marufuku kwa sababu Walawi wametajwa(Ebr 7:12-14).

Kumbuka, "***kuhusu kabila hilo*** [Yuda]***Musa hakusema lolote kuhusu makuhani***."

"***Maana ukuhani ule ukibadilika, hapana budi sheria nayo ibadilike,maana yeye aliyekuwa hayo alikuwa mshirika wa kabila nyingine, ambayo hapana mtu wa kabila hiyo aliyehudumia madhabahu. Maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambayo Musa hakusema neno lo lote juu yake katika mambo ya ukuhani***" (Webrania 7:12-14).

Katika Agano Jipya lote, **"*kuimba*"** kunapewa kibali cha kitume, na hivyo kupata kibali cha Mungu. Wakati mwingine marejeleo ni kwa wakristo binafsi wanaoimba sifa, kama Paulo na Sila katika gereza la Filipi(Matendo 16:25). Wakati mwingine inazungumza juu ya wakristo kujengana katika ushirikawa pamoja (1 Wakorintho 14:15). Kila marejeleo ya wakristo kuabudu na kumsifu Mungu kimuziki hubainisha kuwa walikuwa wakiimba. Kwa vyovyote vile vyombo vya muziki vingetajwa kuwa vilikuwepo au kutumika.

- **Ni nini kingine kilichoingia kupitia mlango huo huo?**

Viongozi wa marejesho wa mwanzonimwa karne ya kumi na tisa, kinyume na inavyosemekana, walijua kwamba kanuni yao iliyopitishwa ni, "***Sema pale Biblia inaposema na nyamaza pale Biblia inaponyamaza***" ingesababisha baadhi ya mazoea ya kawaida kukatazwa. Thomas Campbell, katika ***"tamko na anwani yake***" yenye ushawishi, alisema "***ikiwa atakubali maoni kwamba kitu chochote cha kidini kinakubalika kwa Mungu mradi tu kinatolewa kwa uaminifu na hakijakatazwa, mlango unafunguliwa kwa mazoea mengine mengi ambayo yule anayehimiza msimamo huo kuhalalisha muziki wa ala***

***kuenda hataki kabisa***". Alipohimiza kwamba hakuna chochote kitakachoamriwa kama sharti la ushirika ambalo halijaelezwa waziwazi katika maandiko; Alexander Campbell alipinga, "***Ikiwa kanuni hiyo itafuatwa, ubatizo wa watoto wachanga unapaswa kuachwa***".Thomas hakufikiria hivyo wakati huo, lakini alisema "***bila shaka, ikiwa ubatizo wa watoto wachanga haupatikani katika maandiko, hatuwezi kuwa na uhusiano wowote nao***"(Richardson, Memories of Alexander Campbell, Vol 1, 236-238). Baada ya mafundisho zaidi, makundi yote mawili, pamoja na wengine walianza kufundisha kwamba ubatizo wa kibiblia ulikuwa kuzamishwa katika maji mengi kwa watu wazima wanaoamini, na walizamishwa, ingawa walikuwa wamenyunyiziwa walipokuwa watoto wachanga.

Kunyunyiza watoto wadogo kwa ajili ya ubatizo, kama vile muziki ilivyo upande wa ala, hakukatazwi waziwazi katika maandiko na kunafanywa sana na madhehebu mengi. Ni msingi gani wa kupinga unyunyiziaji wa watoto wachanga unaoachwa kwa yule anayekubali muziki wa ala kwa msingi kwamba haujakatazwa moja kwa moja?

Biblia haiko kimya kuhusu mpangilio wowote wa uongozi wa kanisa lenye mzee anayesimamia zaidi ya kanisa moja. Kwa kuwa Biblia inabainisha waangalizi ndani ya kila kusanyiko na iko kimya kuhusiana na mpangilio mwingine wowote, tunahitimisha kuwa huo ni mpango uliokusudiwa na Mungu kwa ajili ya uongozi wa kanisa la mahali pamoja [kusanyiko]. Wengine wanaoamini kuwa ukimya unaruhusu, wana waangalizi(Maaskofu) wanaosimamia zaidi ya kusanyiko moja, na kundi moja lina askofu wa ulimwengu wote(Papa) juu ya kanisa zima. Mapapa na maaskofu wa kimajimbo wanakuja chini ya hoja sawa na muziki wa ala: Biblia haikatazi waziwazi.

Mbali na mtindo wa Kiaskofu wa uongozi wa kanisa, pamoja na uaskofu wake wenye mamlaka ya kimadaraja, "***kucheza mbele za Bwana***", kufukiza uvumba, na sala kwa watakatifu waliofariki ni miongoni mwa mazoea mengine ambayo si tu yanaweza kuingia chini ya mkumbo huo huo, bali wamefanya hivyo na wanaendelea kufanya hivyo. Kwa sasa inatekelezwa kwa misingi ya mantiki hiyo.

Kuhusu matukio yaliyorekodiwa au yaliyoandikwa ya Agano la Kale inasema, "***Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani***"(1 Wakorintho 10:11).

"***Na Nadabu na Abihu, wana wa Haruni, wakatwaa kila mtu chetezo chake, wakatia moto ndani yake, wakatia na uvumba, nao wakatoa moto wa kigeni mbele ya Bwana, ambao yeye hakuwaagiza. Kisha moto ukatoka hapo mbele za Bwana, nao ukawala, nao wakafa mbele za Bwana. Ndipo Musa akamwambia Haruni, Jambo hili ni hilo Bwana alilolinena, akisema, Nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, nami nitatukuzwa mbele ya watu hao wote. Haruni akanyamaza kimya***"(Law 10:1-3)

Nadabu na Abihu walijifunza kwamba Mungu Mtakatifu anataka kuabudiwa kwa vitu vitakatifu. "***Vitu vya kigeni***" au "***Vitu visivyoinishwa***" si vitakatifu. Mungu sio Mtakatifu tu, Mungu ni "***Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu***". Jinsi tunavyomuabudu katika sala, katika meza ya Bwana na katika kuimba, ni ***"jambo kubwa***".Tunapaswa kuwa "waabudu wa kweli"(Yohana 4:23).

"***Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli***"(Yohana 4:24).

- **Je, vifungu vya uimbaji katika Waefeso na Wakolosai ni vya kusanyiko au mtu binafsi?**

Kanisa la Efeso liliamriwa, "***mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu***"(Waefeso 5:19), Wakolosai walipaswa, ***"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu"***(Wakolosai 3:16). Msemaji tunayerudiana wengine wanasema kwamba vifungu hivi vinarejelea tendo la mtu binafsi na havitumiki kwa utendaji wa kusaniko. Kama hiyo ingekuwa kweli, bado ingekuwa kweli kwamba

kila marejeleo ya kusifu na kuabudu ya muziki katika Agano Jipya ni kuimba.

Kuna ushahidi wa kutosha hata hivyo, kwamba tofauti ya mtu binafsi dhidi ya kusanyiko haipo katika vifungu hivi. Nyaraka za Paulo, isipokuwa zile zilizoandaliwa kwa watu binafsi kama vile Timotheo, Tito na Filemoni, ziliandikwa kwa makanisa na zilikusudiwa kusomwa na kuzingatiwa na makanisa. Nyaraka tano za mwanzo zinataja kanisa au makanisa katika Salamu.

Wagalatia imeandikwa, ***"kwa makanisa ya Galatia"***(Wagalatia 1:1), ambayo ni makusanyiko ya Antiokia, Pisidia, Derbe, Listra, na Ikonia ambayo yalianzishwa na Paulo na Barnaba katika safari yao ya kwanza ya kimisionari.Nyaraka kwa Wathesalonike zote, 1 na 2 zimeandikwa, "***kwa kanisa la Wathesalonike***"(1 Wathesalonike 1:1 na 2 Wathesalonike 1:1), na Wakorintho wa kwanza na wa pili zimeandikwa, "***kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho***"(1 Wakorintho 1:1; 2 Wakorintho 1:1).

Barua tatu za Paulo zinazofuata, Wafilipi, Wakolosai, na Waefeso ziliandikwa kutoka Rumi wakati wa kifungo ambacho Luka anakielezea mwishoni mwa kitabu cha Matendo(Matendo 28:31-32). Wafilipi waliandikiwa, "***kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu, walioko Filipi, pamoja na maaskofu na mashemasi***" (Wafilipi1:1). Ikiwa ni pamoja na viongozi wa kusanyiko, katika anuani inaashiria wazi kwamba Paulo analiandikia kusanyiko la Filipi. Paulo kwa Wakolosai aliandika, "***kwa ndugu watakatifu, waaminifu katika Kristo, walioko Kolosai. Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu***" (Wakolosai 1:2) na waraka kwa Waefeso aliandika, ***"kwa watakatifu walioko [Efeso] wanaomwamini Kristo Yesu***" (Waefeso 1:1).Waraka kwa Wakolosai umeweka wazi kwamba Paulo anatarajia nyaraka hizi zitakapopokelewa, zisomwe kwa makanisa (Wakolosai 4:6).

Ni wazi kwamba hakuna mtu katika kusanyiko anayeweza "***kufundishana na kuonyana***" peke yake.Baadhi ya watu huchukuliwa. Rejea ya msingi ni kwa kusanyiko lililokusanyika kwa ajili ya kujengwa na kuabudu, ambapo inategemea wangesikia pale nyaraka zikizomwa.

- **Je, hakuna kielelezo cha kuabudu?**

Hata wale wanaokwepa mifumo na kukemea mielekeo wanakiri kwamba kuna mifumo ya kufuatwa katika maandiko. Inafahamika karibu kote ulimwenguni kwamba Kristo anapaswa kuwa kielelezo chetu katika mwenendo na mtazamo. Kuna makosa matatu yanayoenea kuhusu mifumo: (1) Majaribio ya kuweka vielelezo ambavyo maandiko hayavihitaji; (2) Msisitizo wa kipekee wa kielelezo cha mikusanyiko ya kusanyiko na (3) Kukataa kwamba kuna kielelezo kinachokuwepo kwa ajili.

- **Kielelezo Cha Muundo**

Wengine huona vielelezo ambavyo havikukusudiwa. Hoja hapa ni kwamba si lazima kukataa kwamba kuna vielelezo katika maandiko kuhusu kazi na ibada inayokubalika ili kutambua kwamba baadhi ya vielelezovinavyodaiwa havifungi. Katika uchanganuzi wa mwisho, muundkielelezo hakifungi kwa sababu nadhani ni kitu kingine katika maandiko si cha kubahatisha na kisichofunga kwa sababu mtu mwingine anafikiri hivyo. Maandiko yanachosema ni kweli ikiwa tunaelewa au tunaamini au la.

Nukuu iliyojulikana sana kutoka siku za mwanzo za harakati ya marejesho inasomeka, "***Ingawa makisio au makato kutoka kwenye msingi wa maandiko, yanapofikiriwa mwa haki, yanaweza kuitwa kweli fundisho la Neno Takatifu la Mungu, lakini hayafungamani rasmi na dhamiri za Wakristo. Mbali zaidi kuliko wanavyoona uhusiano huo, na kwa dhahiri wanaona wako hivyo, kwa maana imani yao haipaswi kusimama katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu na ukweli wa Mungu***"(Thoms Campbell. Declaration and address).

Hiyo ni lazima iwe hivyo, isipokuwa mtu yuko tayari kukabidhi mamlaka juu ya imani yake kwa mhubiri, mhariri, au mwinadamu mwingine. Tunapaswa kuwashawishi, kuwaonya wale tunaowaona kuwa wamekosea, lakini hatuna uwezo wa kulazimisha mtu yeyote kuamini au kutekeleza upatanifu wa mitazamo yetu.

- **Kielelezo cha Maisha**

Wakati ombi la vielelezovya kibiblia linakaribiana kabisa na vilelezovya muundo wa makusanyiko na mambo kama vile tengenezo na shughuli za kusanyiko, wasikilizaji kuhitimisha kimakosa kwamba hayo ndiyo mambo pekee, au angalau ya msingi, ambayo Bwana anahusika nayo.

Matukio ya hukumu ya Yesu yanalenga jinsi wanafunzi wake wanavyopaswa kuwahudumia wenye uhitaji. Hotuba ya mlimani inanatilia mkazo wa kimsingi kwa tabia, motisha na utambuzi wa utegemezi wetu kwa Bwana zaidi kuliko sisi wenyewe. Mifano yake inatukumbusha kwamba tunapaswa kuwa majirani kwa yeyote aliye na uhitaji na kushangilia watenda dhambi wanapoitikia na kutubu.

Waandishi wa Agano Jipya wanapokuja kwenye sehemu ya "Tutaishije basi" katika nyaraka zao(Tazama kwa mfano; Warumi 12-14; Waefeso 4-6; Wakolosai 3-4) kimsingi hawalengi hasa mipango mikusanyiko na makusanyiko.Mtazamo wao uko katika maisha ya kila siku. Wanasisitiza maadili, uaminifu, na roho ya kujali. Mpangilio wa vielelezokwa ajili ya maisha yetu katika Kristo ni nyumbani (Mume/mke, wazazi/watoto) na mahala pa kazi (Bwana/mtumishi au mwajiri/mfanyakazi). Mfano huo ni pamoja na uaminifu kwa mwenzi wa ndoa na kutendewa na kwa haki na uaminifu mahali pa kazi, kufanya kazi kana kwamba mtu anafanya kazi kwa Bwana.

Katika maisha ya kusanyiko, kielelezo cha kibiblia kinasisitiza kuwakubali walio dhaifukwa sababu Kristo alitukubali tulipokuwa dhaifu. kinarekebisha usemi wetu, kinakataza uongo, kashfa, mazungumzo machafu, na yenye kupotosha na mizaha isiyofaa, badala yake kinaleta mazungumzo yaliyojaa neema, mambo yaliyokolea munyu ambayo huwatia moyo na kuwajenga wasikilizaji. Inakazia mitazamo, juu ya kuondoa ugomvi, na uovu, na kuvaa fadhili, huruma, na roho ya kusamehe. Kupuuza kipengele hiki cha kielelezo cha kibiblia ni kutoa risasi kwa wale wanaofikiri kuwa kielelezo hauhusiani na maisha na kupuuza kile ambacho Biblia inasisitiza kimsingi.

Ndugu wengine walio katika mduara ulioshikana wa ushirika, wakiwemo wale wanaokubaliana nao kabisa kuhusu masuala fulani, wanaonekana kupuuza kuendelea kwa ukosefu wa uaminifu na uasherati ndani ya idadi yao mradi tu wahusika wawe "wazuri" katika masuala hayo. Hakika hakuna mtu anayefundisha kwamba haijalishi jinsi watu wanavyotenda mradi tu mafundisho yao ni sahihi, babali wasikilizaji wanaweza kupata wazo hilo kila wakati kipengele cha mtindo wa maisha cha muundo wa Biblia kisipozingatiwa pamoja na vipengele vingine vinavyochukuliwa kuwa "mafundisho."

## V. Kielelezo cha kusanyiko

Wale wanaokataa kile wanachokiita 'ukielelezo' daima wanakataa vipengele maalum vya kielelezo cha mikusanyiko ya kimakusanyiko [kikanisa] ambavyo vimefundishwa na kutekelezwa na makanisa ya Kristo kwa miaka mingi. Yule ambaye mahubiri yake ninayapitia anakanusha kwamba kielelezo cha kibiblia kinabainisha uimbaji na hivyo kuzuia upigaji wa ala.

Je, kuna kielelezo cho chote katika Agano Jipya kwa ajili ya mikusanyiko [mikutano] yetu? Je, Kuna jambo lolote katika Biblia linaloonyesha ni nini Mungu atapendezwa nacho tunapokusanyika ili kumwabudu na kujengana sisi kwa sisi, au Kuna jambo lolote tunalochagua kufanya ambalo hutufurahisha na kutufanya tujisikie vizuri kuwa tunakubalika kama shughuli ya mkusanyiko? Je, ni muhimu kuuliza kuhusu kile tunachokifanya kama ibada katika mikusanyiko yetu, "Hivi hili ni la kibiblia?" Msemaji wetu anasema ndiyo. Je, tunapaswa kujiuliza kama kile tunachokaribia kufanya kinaweza kuonyeshwa kutoka kwenye maandiko kuwa kinakubalika kwa Mungu? Anasema, "Jambo muhimu zaidi la kuuliza katika kuamua njia ya kutenda ni "Biblia inasema nini."

Tena, nukuu kutoka kwa mwanzilishi katika siku za mwanzo za jaribio huko Marekani la kurejesha kazi za kiutume lilikuwa:

"Basi, wale wanaopinga kwamba hakuna utaratibu ulioidhinishwa na Mungu wa ibada ya kikristo katika mikusanyiko ya

kikristo, kufanya wakati huo huo, na lazima bila kuepukika kudumisha, kwamba hakuna machafuko, hakuna makosa, hakuna uvumbuzi, hakuna uovu, katika ibada ya kanisa la kikristo-hapana kamwe haiwezi kutokea. (Alexander Campbell, "A restoration of the ancient order of things")

## VI. Mafundisho ya kibiblia ya mkusanyiko

Kuna fundisho la Agano Jipya la kukusanyika. Tumeamriwa tusiache kukusanyika pamojakwa sababu kuonyana pamoja na hali ya kutiana moyo na inatolewa na kupokelewa katika mikusanyiko hiyo(Ebr 10:24-25). Mwelekeo kamili wa kiutume kwa ajili ya uendeshaji wa mikusanyiko hii unapatikana katika waraka wa kwanza kwa Wakorintho. "Lugha ya mkusanyiko" huanzia katika 1 Wakorintho 11:17 ambapo Paulo alianza kusahihisha tabia ya wakorintho kuhusu Meza ya Bwana. Zingatia nimara ngapi "mnapokusanyika". "***Lakini katika kuagiza haya, siwasifu, ya kwamba mnakusanyika, si kwa faida bali kwa hasara. Kwa maana kwanza mkutanikapo kanisani nasikia kuna faraka kwenu; nami nusu nasadiki; kwa maana lazima kuwapo na uzushi kwenu, ili waliokubaliwa wawe dhahiri kwenu. Basi mkutanikapo pamoja haiwezekani kula chakula cha Bwana***;"(1 Wakorintho 11:17-20).

Hii inatuambia Meza ya Bwana ni katika kusanyiko. Wakorintho walikuwa wameiharibu karamu hiyo kiasi kwamba hawakuweza tena kukusanyika kwa ajili hiyo. Maana yake hapo, ni kwamba walipaswa kukusanyika pamoja kula Chakula cha Bwana. Hiyo inakubaliana na desturi ya kanisa la Troa ambao pia walilitekeleza hilo chini ya uongozi wa kitume, “***siku ya kwanza ya juma***…***tumwkutana ili kumega mkate***” (Matendo 20:7).

Katika sehemu iliyosalia ya sura ya kumi na moja, Paulo alinukuu maneno ya Yesu alipokuwa akianzisha huduma ya Chakula cha Bwana kama vile Mathayo, Marko na Luka walivyoandika, akitukumbulisha kwamba kusudi la chakula cha Bwana lilikuwa ukumbusho wa mwili na damu ya Bwana. Milo ya kukidhi njaa zetu inapaswa kuliwa,

"***nyumbani,***"alisema (1 Wakorintho 11:24, linganisha na mstari wa 22). Kwa kuwa mara nyingi walikutana majumbani mwao, mwelekeo hauonekani kuwa katika kituo gani wanapaswa kula, lakini badala yake "***si katika mkusanyiko.***" Kinyume na kile ambacho wanadumisha katika vitabu maarufu vya sasa kuhusu Chakula cha Bwana, kwangu inaonekana kwamba kula Chakula cha Bwana kama sehemu ya chakula cha ushirika [cha kawaida] ndicho anachokataa Paulo hapa.

Milo ya ushirika ni mizuri, na imeidhinishwa, lakini haipaswi kuwa sehemu ya mkusanyiko au Chakula cha Bwana. Mada inayofuatia Chakula cha Bwana katika 1 Wakorintho ni matumizi na matumizi mabaya ya karama za kiroho. Wakorintho wa kwanza sura ya 14 inarudi kwenye mada ya kusanyiko, wakati "***kanisa ambalo linakusanyika pamoja***"(aya 23) na ***"mnapokutana pamoja***"(aya 26).1 Wakorintho 14 ina maagizo yanayohusu karama za kimiujiza za kiroho, hasa lugha ya kinabii. Haya ni sehemu tena ya uzoefu wa kanisa la siku hizi, na wengine wanapendekeza kwamba maagizo katika sura hii ni kwa ajili ya mkusanyiko maalum unaoitwa kwa ajili ya matumizi ya karama hizo na kwa hiyo haitumiki katika mikusanyiko yetu. Hata hivyo, kuna uwezekano mkubwa zaidi kwamba karama hizo zingetumika wakati wowote namahali popote pale wale waliokuwa nazo walipokusanyika na kwamba 1 Wakorintho 14 inazungumza mwenendo katika mkusanyiko wa kawaida wa kanisa.

## VII. Tena, ni sura ya "kukutanika pamoja" (Mkusanyiko)

Kufundisha, kuhubiri, kutoa unabii(mafundisho yaliyovuviwa) vilifanyika katika mkusanyiko (1 Wakorintho 14:3,19), kama ilivyokuwa wakati Paulo alipohubiri katika kanisa kule Troa walipokuwa wamekusanyika kwa ajili ya kuumega mkate (Matendo 20:7). Maombi pia yalifanyika katika mkusanyiko (1 Wakorintho 14:15). Maombi yanapaswa kutolewa kwa lugha inayoeleweka ili wote waliopo waweze kusema "Amina" kwa kile kiongozi anachosema, na hivyo kuifanya sala inayoongozwa yao wenyewe (1 Wakorintho 14:16). Hiyo inaakisi kile

tunachokiita mtu mmoja huongoza sala, lakini wote wanasali pamoja naye na kila mmoja akiifanya sala kuwa yake.

Waliimba kwenye mkusanyiko(1 Wakorintho 14:15). "***Basi, ndugu, imekuwaje? Mkutanapo pamoja, kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga***"(1 Wakorintho 14:26). Inapendekezwa kuwa "***kila mmoja awe na wimbo***", tunarejea kwenye upekee; tukitazama nyuma kwa mtu mmoja anaomba kwa sauti na wengine kwenye kusanyikona wengine kwenye hufanya ile sala kuwa yao wenyewe. Hii inarejelea kwenye uimbaji kwamba mtu mmoja huchagua na kuongoza wimbo na wengine humfuata wakiimba pamoja naye. Inaleta maana sana kwamba mkiimba kwa sauti, kiongozi kuimba kwa awamu na kusanyiko linamwitikia, mfumo huo ulikuwa wa kawaida katika kanisa la kwanza.

Katika sehemu nzima, hoja inatolewa kwamba baadhi ya mambo ni ya kibinafsi, hayastahili kufanyika katika mkusanyiko [kama kanisa].Chakula cha kawaida cha kukidhi njaa si cha kusanyiko(1 Wakorinho 11:3). Kunena kwa lugha, ingawa wakati huo ilikuwa karama ya kweli ya Roho Mtakatifu, haikupaswa kutumika katika mkusanyiko isipokuwa kuwe na mkalimani, na si zaidi ya watu wawili au watatu waliopaswa kunena (1 Wakorintho 14:28). Wanawake ambao kwa hakika wanaruhusiwa kusema katika sehemu nyingi na katika hali nyingi, hawakuruhusiwa kunena katika mikusanyiko (1 Wakorintho 14:34).

Mtume yuko katika uchungu wa kutukumbusha kwamba maagizo yake si maoni yake tu. Alisema, "***Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana***"(1 Wakorintho 14:37).

Kufuatia mjadala wa mkusanyiko 1 Wakorintho 14, mada inayofuata katika waraka ni ufufuo(sura ya 15). Hiyo inafuatwa mara moja na amri kuhusu matoleo [changizo]. "***Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na***

***aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja***"(1 Wakorintho 16:1-2). Huu ulikuwa mchango maalumkwa madhumuni fulani. Paulo alitaka makanisa ya watu wa mataifa yayasaidie makanisa ya kiyahudi kule Yudea wakati wa uhitaji wao na njaa, lakini pia kusaidia kuimarisha mshikamano kati ya makanisa ya kiyahudi na ya mataifa.

Wengine wanafikiri jambo hili ni kuwaambia wakristo kuweka akiba nyumbani, lakini hilo haliendani na muktadha. Kama wote wangeweka wangetenga zawadi zao wakazihifadhi nyumbani, ni lazima kungekuwa na michango baada ya Paulo kufika Korintho, mchango wa namna ambayo alitaka iepukwe.

Neno "changizo" (kwa Kiyunani [Kigiriki]: Logeia) linaonekana kurejelea tu makusanyo yanayofanywa na halaiki ya watu, sijambo linalofanywa na mtu mmoja mmojakibinafsi(Everett Ferguson. The church of Christ: A biblical Ecclessiology for today Grands Rapids Eerdmans, 1996,240). Hii inatiwa nguvu na ukweli kwamba Paulo aliwahimiza "kukamilisha" makusanyo ambayo walikuwa wameyaanza (2 Wakorintho 8:6). Hii ina maana kwamba kulikuwa na kiasi kilichokusanywa na kujulikana ambacho kilikuwa hakijakamilika.Hiyo pia haina maana kutaja siku fulani ya kuongezwa kwa fungu katika kila nyumba. Sababu dhahiri ya kutaja siku, hasa kwa kubainisha siku ya kwanza ya juma, siku ya Bwana, siku ambayo Kristo alifufuka toka kwa wafu, ni kwa sababu walikuwa wanakusanyika siku hiyo. Ndivyo ilivyokuwa. Kwa hiyo, lilikuwa tukio la kimantiki kuchangia mfuko, ambao katika jambo hili hatimaye ungepelekwana Paulo pamoja na wengine kwa watakatifu wa kiyahudi.

Hilo linaonyesha kwamba tukio ambapokanisa lote la Korintho lilikusanyika pamoja ili kushiriki Chakula cha Bwana ilikuwa siku ya kwanza ya juma, kama ilivyofanyika Troa. Hii haikuwa amrikwa kanisa la Korintho tu, bali hata makanisa ya Galatia na Makedonia yalikuwa yamepokea maagizo sawa. Kwa kuwa iliamriwa, na siku husika ilichaguliwa, wakati kusanyiko linapotambua mahitaji yake, njia iliyoidhinishwa na kimitume ya kutimiza mahitaji hayo ni kwa changizo

ya siku ya kwanza ya juma. Huko Korintho, Galatia, na Makedonia mchango ulifanyika kwenye mikusanyiko [ya makusanyiko yao] [ya makusanyiko yao].

Basi katikamkusanyiko [siku ya kwanza ya juma], chini ya mwongozo wa kitume, kulikuwa na Chakula cha Bwana, mahubiri, maombi, uimbaji na changizo(michango) ili kukidhi mahitaji yaliyotambuliwa. Walifanya na mambo mengine ambayo hayakuwa mabaya kwao, lakini hayakupaswa kuwa sehemu ya mkusanyiko. Mambo hayo ni pamoja na chakula kwa ajili ya njaa, kunena kwa lugha, na wanawake kunena.

Ingekuwaje ikiwa kutaniko lingekusanyika jumapili asubuhi na wote wakacheza hadi jioni ili kuonyesha furaha yao, na wanapokuwa wamechoka sana katika muziki wakaenda nyumbani? Je, ingekuwaje kama mwingine atakusanyika kusikiliza mziki wa symphony orchestra? Je, ikiwa mwingine atachoma mishumaa yenye harufu nzuri? Itakuwaje kama kusanyiko la asili la Marekani litavuta bomba la amani kama tendo la ibada ya kiroho kwa muumbaji? Je, shughuli zote hizi au zozote kati ya hizi zinakubalika katika mkusanyiko? Je, lolote kati ya hayo litakuwa "***sadaka ya manukato, dhabihu yenye kukubalika na kumpendeza Mungu***"(Wafilipi 4:18)

Je, Kuna aina yoyote ya mwelekeo au kielelezo cha mikusanyiko ambacho mambo haya si sehemu yake? Je, mtu ye yote kwa hakika, afanye lolote lililo sawa machoni pake mwenyewe na Mungu atarajiwe kuwa na shauku nalo, ikiwa ameonyesha au hajaonyesha dalili hata kidogo kwamba anatamani mambo haya?

Je, Uzia anapigwa kwa ukoma kwa ajili ya kutoa uvumba ambao makuhani pekee ndio walipewa mamlaka ya kufanya hivyo(2 Nyak 26:16-21) ana lolote la kusema kuhusu mambo haya? Je, kuteketezwa kwa Nadabu na Abihu kwa moto kwa sababu, "***walitoa moto usioidhinishwa ambao Mungu hakuwa amewaamuru***" (Law 10:1-2).

Ibada ya Hekalu ya Agano la Kale ilikuwa na mwelekeo wa hisia, kuanzia kufukiza uvumba hadi kuchomwa kwa nyama, mafuta na ngozi kwenye madhabahu, hadi muziki wa okestra na kwaya. Ilipewa ishara

ya tohara, ikaitwaitwa ibada ya kimwili, wakati ibada ya Agano Jipya inapaswa kuwa katika roho(Wafilipi 3:3). Maagizo ya ibada ya Agano la Kale yalikuwa mifano na vivuli; Kweli, uhalisia vilikuwa bado kuja. Ibada ya Agano Jipya ni katika Kweli. Kitabu cha Waebrania kinaonyesha tofauti:

"***Msichukuliwe na mafundisho ya namna nyingine nyingine, na ya kigeni; maana ni vizuri moyo ufanywe imara kwa neema, wala si kwa vyakula, ambavyo wao waliokwenda navyo hawakupata faida. Tuna madhabahu ambayo wale waihudumiao ile hema hawana ruhusa kula vitu vyake. Maana wanyama wale ambao damu yao huletwa ndani ya patakatifu na kuhani mkuu kwa ajili ya dhambi, viwiliwili vyao huteketezwa nje ya kambi. Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango...Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake. Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana; maana sadaka kama hizi ndizo zimpendezazo Mungu***(Waebrania 13:9-12,15-16).

Tofauti na uvumba na mziki wa vyombo, tunatoa tunda la midomo yetu kuwa dhabihu yetu ya sifa. Tofauti na matoleo ya kuteketezwa ya wanyama, tunaweka miili yetu wenyewe juu ya madhabahu kwa dhabihu iliyo hai tunapofanya mema na kushiriki pamoja na wengine. Tunaabudu katika roho na kweli si katika mwili na kivuli.

## VIII. Kielelezo na uhalalishaji

Vielelezoviliyoainishwa hapa si vya kimamlaka katika msingi kwamba mimi ndiye niliyevitambua na kuviandika. Agano Jipya ndilo taarifa pekee iliyo kamili na yenye mamlaka juu ya kielelezo chetu. Alichofunga Mungu kimefungwa juu ya kila mmoja wetu, tuwe tunafahamu au hatufahamu. Sina mamlaka ya kumfungia mtu ye yote kitu chochote. Nimeelekeza kwa baadhi ya vile ninavyoamini maandiko yanatuambia ni mapenzi ya Mungu. Kila mtu anapaswa kuangalia

ushahidi wa maandiko na kujiamulia mwenyewe ni nini kilicho kweli na atakifanyia nini.

Kuwepo kwa kielelezo cha kiroho kilichoidhinishwa na Mungu kwa ajili ya ibada, au kwa ajili ya mambo mengine ambayo hatujayagusia, hatukatai injili ya neema. Hakuna hata mmoja wetu aliye mkamilifu, iwe kwa matendo yetu au katika ufahamu wetu. Wengine wako mbele zaidi katika mchakato wa kukomaa kuliko wengine.

Wengine wamepata fursa nyingi za kujifunza kuliko wengine.Wengine walipata fursa zaidi za kujifunza kuliko wengine.Hatujaokolewa kwa sababu tunafuata kikamilifu kielelezo cha maandiko. Tunaokolewa kwa dhabihu ya Kristo, kupitia imani yetu kwake. Walakini, vielelezokama hivi vya maisha na mwenendo, katika mikusanyiko na nje ya mikusanyiko, vinatuambia jinsi Bwana wetu anavyotaka tuishi. Tunapotambua kwamba ametuokoa kwa kifo chake, tunapoamini kwamba maandiko ni ufunuo wake mwenyewe na mapenzi yake, na wakati wa shukrani tunachunguza maandiko kwa mapenzi yake kwa ajili yetu, yote kwa sababu tunataka kumpendeza yule ambaye alikufa kwa ajili yetu, huo sio uhalali. Ni imani inayofanya kazi kupitia upendo.

## IX. Historia inazungumza

Kusudi moja la kuimba kama ibada ni kuonyesha umoja wa watu wa Mungu waliokombolewa katika kanisa. Tunapaswa kuwa na nia moja "***ili kwa nia moja tuwe na kauli moja***" tumtukuze Mungu wetu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo(Warumi 15:5-6).

Ingawa inaonekana sasa kwamba ibada ya ala ni jambo la kawaida, hiyo haikuwa kweli daima, na sasa jambo hilo halipo katika upande wa Mashariki wa ulimwengu. Kwa karne nyingi, makusanyiko ulimwenguni kote kwa sauti moja yalitoa tunda la midomo yao kama sifa kwa Mungu. Leo, wale wanaopinga muziki wa ala wanashutumiwa kuwa wanaleta mgawanyiko, lakini hiyo ni katika ulimwengu wa magharibi tu na katika karne za hivi karibuni. Uimbaji [wa mdomo] ulikuwa ndio muziki pekee makanisani kwa muda wa miaka elfu moja,

na organ ilipoanza kutumika kwa mara ya kwanza katika makanisan yaliyohusiana n aroma, ilipipigwa tu kabla na baada ya liturugia (tunaweza kuita “huduma ya ibada”). Ilikuwa miaka mingi baada ya hapo kabla ya uimbaji wa ala kuwa sehemu ya ibada.

Historia hiyo ni ushahidi thabiti kwamba kuachwa kwa ala za muziki katika Agano Jipya kulikuwa kwa makusudi, si kwa bahati mbaya. Makanisa ya mashariki, yanayoitwa makanisa ya Orthodox, yanaendelea na kutumia muziki wa sauti pekee, na yanatawala katika ulaya ya mashariki na katika sehemu nyingi za Asia. Muziki wa ala haukuwa wa kawaida katika makanisa mengi ya Kiprotestanti hadi karne ya kumi na tisa na juu ya upinzani mkali. Maandishi yanayoonyesha upinzani dhidi ya ala katika ibada kwa sauti na misemo yenye nguvu zaidi kuliko utakayopata katika andiko hili bado yapo na mara nyingi yamenukuliwa kutoka kwa watu kama vile John Calvin, mwanzilishi wa makanisa ya Presbyterian (miaka ya 1500), John Wesley, Anglikana na mwanzilishi wa Umethodist-miaka ya 1700), Methodist Commentator na Adam Clarke (mwanzoni mwa miaka ya 1800) na Baptist Charles H. Spurgeon (mwishoni mwa miaka ya 1800)..

Makanisa ambayo yalikuwa katika harakati za marejesho yaliunganishwa kwenye muziki mikusanyikompaka hapo chombo kilipoanzishwa. Muziki wa capella bado unakubaliwa na wote kuwa wa kimaandiko na unaokubalika. Vuguvugu la umoja halipaswi kuachana na msimamo unaojulikana kuwa sawa kwa upande ambao suala la kibiblia halijafanywa.

Hakika, "Cappella" ambayo sasa inafafanuliwa kama "bila kuambatana na ala" maana yake halisi ni "kama kanisani". Tangu mwanzo, muziki kanisani haukuwa na ala.

## X. Mawazo Kufungia kuhusu Kanisa la Kristo.

Kanisa la Bwana lilianza siku ya Pentekoste, kufuatia kufufuka kwa Yesu na kupaa Mbinguni. Petro alihubiri Injili ya ondoleo la dhambi kupitia ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu. Watu walihukumiwa kwa dhambi, "***wakachomwa mioyoni***" na kuuliza "***Tutendeje ndugu zetu?***". Petro aliwaambia, "***Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo,***

***mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu***"(Mdo 2:37-38). Watu elfu tatu waliitikia vyema wakabatizwa, wakasamehewa na kuongezwa na Bwana katika kanisa lake.

Msingi wa ombi la marejesho ni "**Tukisikia yale waliyosikia, na kuamini yale waliyoamini, na kuyafanya kwa moyo yale waliyoyafanya, tutapokea yale waliyoyapokea, msamaha wa dhambi na kipawa cha Roho Mtakatifu, na kuwa wakristo, walioongezwa katika kanisa la Kristo**". Watu leo wanaweza kuitikia kwa njia ile ile na kupata baraka zile zile. Wakati watu kadhaa wanafanya hivi na kuungana pamoja "kufanya mambo ya Biblia kwa njia za kibiblia", wao ni kanisa, kusanyiko la Kristo.

Baadhi yao wanaweza kuwa wanajiingiza katika dhambi za siri, wengine wanaweza kufichua mawazo ya kimadhehebu kwa usemi wao na wanaweza kuwa na roho ya kimadhehebu, lakini kama David Lipscomb alivyosema kwa umaarufu, "***Madhehebu ya watu wengine hayanifanyi Mimi kuwa mdhehebu***". Kila mtu aliyekombolewa anahamishwa kutoka ufalme wa giza na kuingizwa katika ufalme wa Kristo (Wakolosai 1:13). Wote waliookoka walioongezwa kwenye kanisa lake(Matendo 2:47; 5:11). Wote wanaobatizwa katika Kristo wanakuwa watoto katika familia ya Mungu. Wengine wanaitumia nafasi hiyo kwa njia tofauti; lakini ninajaribu kutumia maeleza ya kibiblia kuelezea mambo ya kibiblia.

Ninaposema "kanisa la Bwana", "Ufalme" au "kanisa la Kristo", ni kwamba ninajumuisha na ninamaanisha[nazungumzia kitu kitu kimoja]. Kanisa la Kristo lilianza siku ya Pentekoste katika karne ya kwanza. Warejeshaji wa karne ya 19 hawakuanzisha kanisa la Kristo. Tunawashukuru kwa sababu waliwakumbusha watu kwamba wanapaswa kurudi kwenye Biblia tu, wakiweka kando kanuni za imani za kibinadamu, majina ya Madhehebu na chochote kisicho cha kibiblia kinachogawanya. Tunapaswa kuendelea hivyo leo. Si kazi yetu, hata hivyo, kurejesha kanisa la miaka ya 1950. Ni kazi yetu, kikamilifu iwezekanavyo, katika kila enzi kurejesha kanisa la Agano Jipya kama mitume walivyofanya ili kulitengeneza. Tuirudie Biblia!